

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 1 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. ANNE K. MALECELA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOBINU):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka 2010/2011 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. SALVATORY N. MACHEMLI (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ujenzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 338

Hitaji la Maji Bendera

MHE. ANNE K. MALECELA aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Bendera katika Jimbo la Same Mashariki hawajawahi kupata maji ya bomba tangu nchi ipate Uhuru, hali inayosababisha wategemee maji ambayo si salama kwa maisha ya binadamu hata kama yakichemshwa:-

Je, ni lini Serikali itawaonea huruma Wananchi hao ambao wameonesha kukata tamaa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Bendera iliyopo katika Jimbo la Same Mashariki, inaundwa na Vijiji vitatu vya Bendera, Majengo na Mga du. Wananchi wa Kata hii wanapata maji kupitia visima viwili; kimoja kirefu kinachotumia nguvu ya umeme na kifupi kinachotumia pampu ya mkono. Aidha, Kijiji hiki kimepata tena visima vingine viwili virefu kutokana na kuwa miongoni mwa vijiji kumi vilivyochaguliwa kutekeleza Mradi wa Kitaifa chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira, ambapo zimetengwa shilingi milioni 957.8 katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012, kwa ajili ya Programu hii. Maji yanayopatikana katika visima hivyo viwili ni lita 54,000 kwa saa na upo mpango wa kujenga miundombinu ya kusambaza maji hayo kwa bomba maeneo mbalimbali kwenye Kata yote mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Mgandu kimewekwa pampu ya kusukuma maji inayotumia dizeli, yaani *generator* ambayo imefungwa Kijijini hapo na maji yameanza kusambazwa kwenye vituo vya jamii. Ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 60,000 umekamilika na vituo vinane vya kuchotea maji ya ulazaji wa bomba urefu wa mita 10,390 unaendelea. Ujenzi umepangwa kukamilika Julai, 2011. Katika mwaka 2011/2012 pampu hiyo itabadilishwa kwa kufunga pampu inayotumia umeme. Aidha, Kijiji cha Majengo kwa sasa kinapata maji kutoka visima vifupi viwili vilivyoko katika Vitongoji vya Lasa na Mrango.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kuipatia Kata ya Bendera maji ya bomba zinaendelea kwa kupitia Mradi wa Mwanga - *Same Water Supply* ambao utahudumiwa maeneo ya Nyumba ya Mungu - Mwanga na Same. Mradi huu unatekelezwa chini ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Manispaa ya Moshi. Katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012, zimetengwa shilingi milioni 269.5 kwa kazi hiyo.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa masikitiko sana niseme hili jibu siyo sahihi. Mimi ni Mbunge wa Same Mashariki na vijiji vyote hivi ni vya kwangu.

(i) Kwa kuwa Kijiji cha Bendera kuna kisima kirefu ambacho kimewekwa na mama aliyenifadhili anayeishi Uholanzi, Mama Anna Marima, mimi mwenyewe nikaweka umeme na kisima kile hakikufanya kazi hata siku moja; na kwa kuwa Kijiji cha Majengo nimepewa ufadhili na Waarabu, nikaweka pesa mimi mwenyewe, nikaweka umeme, wataalam wakasema yale maji kutumia binadamu, nikahamisha kile kisima nikakipeleka Mgando; sasa je, Waziri kwa sababu jibu hili siyo sahihi; swali la kwanza unaonaje, baada ya kipindi kifupi tu twende wote Kata ya Bendera umedanganywa na wataalam waliokujibu?

(ii) Kwa kuwa ahadi zimekuwa zinatolewa; hii ni mara ya tatu nipo Bungeni hapa kuhusu Kata ya Bendera; Serikali itanipa lini ahadi ya ukweli na inayotekelezeka? Ninaomba majibu. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi ninatoka Mkoa wa Kilimanjaro; hilo la kwanza, lakini pili, nimezungumza na hao watu wote ambao nimewaeleza hapa. Mimi kusimama hapa nikaanza kupingana na Mbunge ambaye yeye anatoka kule, ambaye anajua yuko kwenye *centre* ya tatizo lenyewe, siwezi kufanya. Mheshimiwa Malecela kama yeye ana *input* hii aliyoleta hapa, anatuambia kwamba, tumedanganya majibu haya asubuhi ya leo nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji, nimezungumza pia na *engineer* wa maji na wana-*appreciate* kwamba, kweli kuna matatizo kama anavyosema katika Kata ya Bendera. Tunakubali kabisa kwamba lipo, ndiyo maana ipo katika jibu nililolitoa hapa. Sasa imetolewa rai hapa, Mheshimiwa Mkuchika, yupo hapa ndiyo Kiongozi wangu na Waziri Mkuu yuko hapa akisema hata sasa hivi tutoke twende Bendera tukaangalie jambo hili, mimi niko tayari, wala sina tatizo kabisa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoieleza, mimi nime-sight hapa nimesema Wilaya hii tunayoizungumza Wilaya ya Same kwa ujumla wake, hela zote na mipango yote hii niliyoieleza, acha Bendera sasa kwa maana hiyo Bendera tumemaliza tumesema kwamba tutaondoka twende wote tufuatane, ni shilingi 2,948,471,473.70 ndizo zilizotengwa kwa ajili ya jambo hili. Kwa hiyo, hata kama anaona kwamba jambo hili linaonekana kwamba halifanyiwi kazi sana, ninataka niahidi hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, jitihada hizi ni kubwa. Mwisho, maji yale yanayopitia pale Mwangi, yanatoka Nyumba Mungu yanakwenda mpaka Same, yanapita Kiberenge, maji haya ni mradi mkubwa na ndiyo ambayo tunaamini kwamba ni *reliable*. Mimi ninarudia tena kusema kwamba, niko tayari kwenda na Mama Malecela mpaka huko, wale ni watani wangu mimi sitaki wapate tabu, tutakwenda kusaidiana katika jambo hili.

SPIKA: Msiende kabla Bunge halijaisha. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Kwa vile matatizo ya Same Mashariki hayatofautiani na Kata ya Mawindi Wilayani Mbarali, ambao wana mradi wa maji kutoka Mto Mpeng'o ambao utagharimu zaidi ya shilingi bilioni nane na watu hawajawahi kupata maji ya bomba toka nchi hii ipate Uhuru. Je, Serikali ipo tayari kuwasaidia kwa sababu fedha zinazopelekwa Halmashauri haziwezi kukidhi kumaliza Mradi huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilufi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Maji atakapokuja kuleta Bajeti yake hapa, haya mambo yote anayozungumza Mheshimiwa Kilufi, yataonekana katika Bajeti. Kwa hiyo, ninamwomba avute subira, hata haya mengine ambayo tunayazungumzia hapa na Mheshimiwa Anne Kilango, yote yataonekana katika Bajeti ile yatajionesha wazi wazi. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi itakuja katika Bajeti inayokuja.

Na. 339

Matatizo ya Maji Ifakara, Mlimba na Idete Gerezani

MHE. ABDUL R. MTEKETA aliuliza:-

Katika Kata za Ifakara, Mlimba na Idete Gerezani kuna tatizo kubwa la maji na Serikali imeazimia kupeleka huduma ya maji Vijijini kwa asilimia 60:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupeleka maji maeneo hayo?
- (b) Je, mpango huo utatekelezwa lini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ilitenga shilingi milioni 218 kwa ajili ya Miradi inayotekelezwa chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Visima 13 vya mfano vimechimbwa katika vijiji vinane. Vijiji hivyo na idadi ya visima vikiwa kwenye mabano ni kama ifuatavyo:-

Mlimba A kisima kimoja, Mlimba B kimoja, Signali visima viwili, Idete visima vitatu, Namwawala visima viwili, Kamwene kisima kimoja, Viwanja Sitini visima viwili na Matema kisima kimoja. Aidha, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Halmashauri imepanga kutumia shilingi milioni 830 kwa ajili ya kukamilisha kazi ya kusanifu na kujenga miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingine sita vinavyotegemea chanzo cha maji ya mserekeo, yaani *gravity*, ambapo katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012 zimetengwa shilingi milioni 160, fedha za ruzuku za maendeleo ya Serikali za Mitaa. Hatua iliyopo sasa ni Mhandisi Mshauri kukamilisha uandaaji wa taarifa ya mwisho ya usanifu na vitabu vya zabuni ili kazi ya ujenzi wa miundombinu ianze ifikapo mwezi Septemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Ifakara ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kilombero. Halmashauri imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012 ili kutekeleza Mradi uliopo wa kuchimba visima virefu na kufunga pampu za kuvuta maji. Pia Halmashauri imewasilisha maombi maalumu shilingi milioni 400 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa Mradi wa Maji Mserekeo katika Mto Lumemo, maeneo ya Kiburugutu ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea Mji wa Ifakara wakati ya Kampeni ya Urais.

MHE. ABDUL R. MTEKETA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Waziri, ninapenda kuuliza swali moja la nyongeza. Halmashauri imeomba shilingi milioni 400 kwa sababu ya kazi za upembuzi ya kupata maji ya mteremko kutoka katika Mto Lumemo Kiburugutu. Je, Serikali itatoa lini hela hii? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mteketa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza hapa, Bajeti ya Wizara ya Maji bado haijaja hapa, itakuja, *unfortunately*, Mheshimiwa Naibu Waziri hayupo amekwenda India na Mheshimiwa Waziri mwenyewe pia kama tulivyoielezwa yuko kwenye matibabu. Ninaamini kabisa kwamba, wakati watakapokuja na ile Bajeti yao, fedha hizi sasa kwa sababu nimemwuliza Mkurugenzi Mtendaji na tumeona kwamba, itabidi tsubiri mpaka watakapokuja ili tuweze ku-*declare* kwamba, zimepatikana. Haya ni maombi maalumu wanayozungumzia hapa ya shilingi milioni 400.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwanza, ninataka kusema kuwa, ninaamini Serikali ni moja; Waziri akiwepo au asipokuwepo tutegeme majibu ya kutosha kabisa. Baada ya kusema hayo, ninataka kusema tatizo la maji kwa nchi yetu ni kubwa sana na kila Mbunge atakayesimama hapa atasema matatizo ya maji, hata kule kwangu Tandahimba, jirani Newala, Mtwara Vijijini na maeneo mengine ya nchi maji ni tatizo. Tuambiwe hapa, Serikali imejianda vipi kumaliza tatizo hili, maana Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005/2010 ilisema ingemaliza tatizo la maji kwa asilimia 65 vijijini?

SPIKA: Mheshimiwa Njwayo, hilo ndiyo kabisa limsubiri Waziri wa Maji, kwa hiyo, tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii.

Na. 340

Tatizo la Mipaka kati ya Hifadhi ya Mikumi na Wananchi

MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMEIR aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani kutatua tatizo la mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na Wananchi wa Maeneo Jirani na Hifadhi hiyo hasa kata za Mikumi na Ruhembe?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdusalaam Selemani Amer, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni kweli kumekuwepo tatizo la migogoro ya kugombania mipaka kati ya Hifadhi ya Mikumi na Wananchi waishio kando kando ya Hifadhi hasa Kata ya Mikumi na Ruhembe. Migogoro hiyo kwa njia moja au nyingine, inatokea kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua tatizo la mipaka, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ilituma wataalam kwenda Hifadhi ya Taifa Mikumi kuanzia tarehe 12 Julai, 2010 hadi tarehe 17. Ili kushirikiana na Wananchi na Wataalam wengine katika kuhakiki mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na Vijiji vya Lumango, Ruhembe, Kihelezo na Kitete Msindazi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunajibu maswali, sasa kama kila mtu anaongea hakuna anayesikia hapa.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Kazi ambayo ilikamilika tarehe 10 Februari, 2011, katika Taarifa iliyowasilishwa na Wataalam waliohusika na uhakiki huo, ilibanika kuwa Kijiji cha Ruhembe kimeingia ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kwa ekari ya 2,762, tofauti na Tangazo la Serikali Na. 121 la tarehe 13 Juni, 1975, lililoanzisha Hifadhi ya Mikumi. Kijiji cha Kihelenzo kimeingia ndani ya Hifadhi ya Mikumi kwa ekari 194, pia ilidhihirika kuwa, *Mikumi National Park* imeingia katika Kijiji cha Kitete Msindazi kwa ekari 4,972.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo hayo, Serikali itafanya tathmini ya maeneo ya hifadhi zake ili kuhakiki mipaka na kuondoa migogoro inayoendelea kujitokeza mara kwa mara. Katika Hifadhi ya Mikumi, tathmini itafanywa kwenye Vijiji viwili vya Lumango na Kihelezo, ambayo yanahitajika kurudishwa Hifadhini. Pia kupima eneo la ukanda wa kilomita moja la *buffer zone* kati ya Hifadhi ya Mikumi na vijiji vitatu ambavyo hakuna ukanda huo, yaani vya Lumango, Kihelezo na Kitete-Msindazi. Maeneo yote yatapimwa na kuwekewa alama za kudumu, yaani *beacons* za karibu karibu ili kubainisha mipaka ya hifadhi kama ilivyohakikiwa katika Tangazo la Serikali Na. 21 la Mwaka 1975.

MHE. YUSUPH ABDALLAH NASSIR: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa niaba ya Mheshimiwa Abdulsalaam Sharia Ameir...

SPIKA: Hapana hili ni la kwako.

MHE. YUSUPH ABDALLAH NASSIR: Haya ni ya kwangu, ni lini Serikali itakwenda kutoa tathimini halisi ya upimaji huu?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwenye yale maeneo ambayo yako nje ya hifadhi na ramani inaonesha kwamba, yalikuwa hifadhini, tumekubaliana kwamba, tumeshawaruhusu Wananchi waendeleo kuyatumia. Kwa yale maeneo ambayo yamo ndani ya Hifadhi, tumekubaliana katika Mwaka wa Fedha ambao umeshaanza mwezi Julai, 2011, fedha zimetengwa kama tutakavyowasilisha kwenye bajeti yetu, kwa ajili ya kufanya kazi ya tathmini pamoja na kuwalipa Wananchi fidia pale ambapo italazimika kufanya hivyo.

Na. 341

Mapato Yatokanayo na Mlima Kilimanjaro

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA aliuliza:-

Jimbo la Vunjo limebahatika kuwa na Mlima Kilimanjaro unaoitangaza Tanzania Duniani kote na kuleta Watalii wengi kutoka Duniani kote kote ambao huliongezea Taifa mapato:-

(a) Je, vijiji vinavyopakana na Mlima huo vinafaidikaje na Mlima huo?

(b) Je, kwa nini Wakenya wanapanda Mlima huo kwa nyuma wakidai ni wao na kuikosesha Tanzania mapato bila kuchukuliwa hatua zozote?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifadhi la Taifa limeweka utaratibu wa kuwanufaidha Wananchi wanaoishi katika vijiji vinavyoizunguka Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro kupitia ujirani mwema. Utaratibu huo umewalenga Wananchi moja kwa moja kwa kuchangia Miradi ya Maendeleo, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kijamii (kama vile Shule, nyumba za walimu, miradi ya maji na kadhalika). Kupitia Idara ya Ujirani Mwema, kila Hifadh ya Taifa inatenga 7% ya bajeti ya matumzi ya kawaida ya mwaka kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa miradi hiyo, ambapo Wananchi wanatakiwa wachangie utekelezaji wa Miradi hiyo, ambapo Wananchi wanatakiwa wachangie 30% na hifadhi ichangie 70%. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2006/2007 hadi mwezi Juni, 2011, TANAPA imechangia kiasi cha Shilingi 1,468,681,302 kwa ajili ya kuendeleza Miradi ya Maendeleo ya Jamii kwa vijiji vinavyoizunguka Mkoa wa Kilimanjaro. Maeneo yaliyonufaika na michango hiyo ni pamoja na Siha, Rombo, Mwanga, Hai na Manispaa ya Moshi na Moshi Vijijini.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na taratibu za Hifadhi ya Taifa Tanzania, kila Hifadhi ina malango maalum ya kuingia na kutoka kwenye Hifadhi ya Kilimanjaro. Lango ambalo hutumiwa na watalii kupanda Mlima Kilimanjaro upande ambao Mheshimiwa Mbunge ameusema (na baada ya kupata kibali ambacho hutolewa Marangu) ni Rongai ambapo sehemu hiyo ipo ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Hivyo, Serikali haina taarifa za Wakenya kupanda Mlima Kilimanjaro kwa njia nyingine tofauti na hiyo ambayo sisi tunaitambua. Tunaomba Watanzania na hasa wanaoishi Mkoa wa Kilimanjaro, ikiwa na Mheshimiwa Mbunge mwenyewe tushirikiane katika kubainisha watu wanaopenya kinyume na taratibu ili tuweze kuchukua hatua.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Pamoja na majibu yake mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Swali la kwanza kuhusu kiasi kinachotolewa kuendeleza wale Wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro. Hapa amesema TANAPA inatoa 7% kwa miaka mitano, sawasawa na shilingi 1.4 billion. Mimi ninachotaka kuuliza ni kwamba; 1.4 billion kwa miaka mitano kwa kazi kubwa tunayofanya sisi watu wa Kilimanjaro kulinda mlima ule, moto ukiwaka kwenye mlima tunakwenda kuuzima na tumepewa kazi leo ya kuwafuatilia watu wanaoingia kinyemela kuja kufanya utalii kupitia Kenya na kupanda miti. Mimi ninachotaka kusema ni kwa nini tunapewa 7% na kwa nini isiwe 30% ili tuweze kuendelea kuulinda mlima ule na uendelee kuwa na manufaa kwa Watanzania na tuendelee kuwavutia watalii wengi?

(ii) La pili, kuna Barabara ya Kilema Kaskazini, ambayo nilishaongea na Mheshimiwa Waziri, tuiimarisha kwa kujenga ili uwe ni mlango mwingine wa kuingiza kwenye Mlima Kilimanjaro? Kwa leo unasemaje Mheshimiwa Waziri?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Mrema, kwa kukubali ombi letu la kushirikiana na sisi katika kusimamia wale wanaopenya, ninaomba kujibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumesema mchango ambao tumekuwa tukiutoa ni 7% ya bajeti ya matumizi, kiasi ambacho ni kidogo na kwa kweli Mheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro, tumekuwa tukizungumza nao kuhusu suala hili mara kwa mara. Tarehe 6 Julai, 2011 nilijibu swali namba 190 la Mheshimiwa Freeman Mbowe, ambalo pia lilikuwa linazungumzia suala hili hili na baada ya swali hilo na kabla tulikuwa tumeshaanza kuwashauri Wananchi wa Halmashauri zinazozunguka mlima ule, ziwe na utaratibu ambao tutakubaliana nao, utakaowawezesha kupata mapato ya moja kwa moja kwa kuanzisha tozo tofauti na ambayo sisi tunatoza kwa ajili ya uhifadhi.

Faida ambazo zipo ni zaidi ya hii 7% ambayo tunachangia. Kwa takwimu tulizonazo, Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro inatoa *guides* au kazi ya waongoza watalii ambao wameajiriwa zaidi ya 400 na wanapata zaidi ya shilingi bilioni 1.9 kwa mwaka. Kuna wapagazi zaidi ya 10,000 ambao wanapata Dola za Kimarekani milioni 4.8 kwa mwaka, zaidi ya shilingi bilioni 7. Kuna wapishi

ambao wako zaidi ya 500, ambao wanapata zaidi ya shilingi milioni 500,078. Hizi ni baadhi tu ya faida ambazo zipo kwa Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro. Hoja ya msingi ya kuangalia namna gani tuweze kuboresha mchango wetu kwenye eneo hilo, tumeichukua na tulishaanza mazungumzo kuhusu suala hilo.

Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusu suala la kuboresha suala la Kilema, nimeshawasiliana na Uongozi wa *KINAPA* ili waweze kuweka kiasi fulani cha fedha kwenye bajeti yao, kwa ajili ya kushirikiana na Wananchi wa Kilimanjaro, kuboresha barabara hiyo. Kwa hiyo, hilo tunalifanyia kazi.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa njia ya kwenda Mlimani kupitia Rongai Rombo ni fupi sana ukilinganisha na njia nyingine; na kwa kuwa njia hizi zinawasaidia Wananchi kupata mafao mbalimbali kama kupitia wapagazi, wapishi na kadhalika; je, Wizara haioni kwamba umefika wakati sasa wa kuitangaza njia ya Rongai ili Wananchi wa Rombo nao wapate faida zinazotokana na kuwahudumia watalii?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tumekuwa tukifanya jitihada kubwa za kutangaza Mlima Kilimanjaro na niseme tu kwa bahati wageni walio wengi wanakuja nchini kwa ndege na wengine wanaingilia Kenya. Wanapoingilia Kenya na hivi wanavyojenga Uwanja wa Ndege jirani kule itakuwa ni rahisi zaidi kwa watu kutumia njia ya Rongai. Kwa hiyo, pamoja na kutangaza mlima, tutaongeza jitihada za kutangaza njia ambazo ni *convenient* zaidi kwa wageni kama Mheshimiwa Mbunge alivyopendekeza.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa agizo la kuzuia wageni kupanda Mlima Kilimanjaro moja kwa moja kutokea nchi jirani lililenga kuuthibitisha ulimwengu kwamba Mlima Kilimanjaro uko Tanzania; na kwa kuwa Waziri amesema kuna fununu kwamba watu wanapanda Mlima Kilimanjaro kutokea nchi ya jirani; je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu jambo hili?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la nyongeza la Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na ombi ambalo nimelitoa kwa Watanzania, kushirikiana na Wizara yangu kusimamia maliasili za nchi kama Katiba yetu ya Nchi, Ibara ya 27 inavyotaka na kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wamekubaliana, tutaendelea kuchukua hatua za kisheria pale ambapo kunapatikana ushahidi wa kutosha kwamba, watu wamekiuka taratibu hizo.

Sambamba na hilo tunachokifanya ni kuongeza jitihada za kutangaza mlima huu kwamba, upo Tanzania na kuboresha miundombinu yetu ili wageni waweze kuingia au kupanda mlima huo kutokea kwenye *destination* au viwanja vyetu vya nchini.

Na. 342

Mapato Yatokanayo na Mlima Kilimanjaro

MHE. DKT. AMOS G. MAKALLA aliuliza:-

Wafugaji wa Kata za Doma, Melela, Dakawa, Kibati, Mtibwa, Pemba na Sungiji wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa dawa, majosho na malambo ya kunyweshea mifugo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wafugaji hao mahitaji hayo?

(b) Je, Serikali ina mpango wowote wa kuboresha Minada ya Mkongeni na Hoja?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Amos Makalla, Mbunge wa Mvomero, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo kwa Mikoa yote nchini kuanzia mwaka 2006/2007 ili kuwezesha upatikanaji wa dawa za kuogesha mifugo kwa gharama nafuu. Kwa mwaka 2006/2007, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ilipata jumla ya lita 700, mwaka 2007/2008 Halmashauri hiyo ilipata jumla ya lita 413, mwaka 2008/2009 lita 3,216 ambazo zinatumiwa hadi sasa na kufikia tarehe 30 Juni, 2011 Halmashauri ilikuwa na akiba ya dawa za kuogesha jumla ya lita 1,900. Kwa miaka yote hiyo, Serikali imeweza kuchangia shilingi 70,958,000 kama ruzuku kwa Wilaya ya Mvomero. Serikali itaendelea kutekeleza mpango huo kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa majosho kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilayani (*DADPs*). Kwa mwaka 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero imetengewa jumla ya Shilingi 487,695,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali kupitia *DADPs*, ikiwa ni pamoja na uhifadhi wa mazingira, ujenzi wa vituo vya mafunzo vya kilimo na mifugo kwa ajili ya wafugaji na wakulima, ujenzi na mnada na uchimbaji wa malambo ya maji kwa mifugo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, imetenga jumla ya shilingi milioni 48 kwa ajili ya kuboresha Mnada wa Kibaoni. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, itaboboresha kwa ukarabati Mnada wa Hoza kulingana na upatikanaji wa fedha. Ninaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, iweke mipango ya kuboresha Minada iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge kwa kupitia mipango yake ya *DADPs*.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Katika majibu yake amesema kwamba, Wilaya ya Mvomero imetengewa fedha katika mwaka 2010/2011. Mwaka huu wa Fedha ulishakwisha kwa hiyo amekosea tu kwamba imetengewa kwa mwaka huu, maana anasema imetengewa shilingi milioni 487 mwaka 2010/2011:-

(a) Je, fedha hizi ziko katika mwaka huu au mwaka uliopita?

(b) Minada niliyoitaja ya Hoja, Mkongeni na Kibaoni ni mikubwa sana; je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuongeza fedha na kuwa *serious* kabisa katika jambo hili badala ya kuiachia Wilaya Mvomero?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amos Makalla. kama ifuatavyo:-

Moja, fedha nilizozitaja zilikuwa kwenye Mipango ya Wilaya ya Mvomero kwa kipindi kilichopita, lakini pia wana fedha ambazo wao watazipangia kwamba, waziweke kwenye minada ipi kwa kipindi kinachokuja.

Pili, ni kweli kwamba, Wilaya ya Mvomero ina minada mingi na mizuri hasa ukiwepo Minada ya Kibaoni, Mkongeni, Mkombani pamoja na Hoza. Niseme tu kwamba, Minada hiyo itashughulikiwa kwa sababu tunaona umuhimu wake na kwa kumsisitiza tu Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, Minada hiyo itaboreshwa zaidi kwa sababu ipo kwenye mikakati na eneo hilo lipo kwenye *catchment area* hasa maeneo ambayo mifugo itatoka itakayochinjwa kwenye Machinjio ya Ruvu itakapokuwa imekamilika. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Minada hiyo kwa mujibu wa Halmashauri itakavyojipangia yenyewe, itakuwa kwenye mikakati hasa kwa ajili ya kutumika kama feeders kwa Machinjio ya Ruvu.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wafugaji wa Wilaya ya Longido wameboresha mifugo na mifugo hiyo inaweza kukidhi minada ya nje; na kwa kuwa Kenya wameshagundua kwamba Mifugo ya Longido imeboreshwa kwa hiyo wanakuja kununua kupeleka nje; je, ni lini Serikali itatumia Mifugo ya Longido kwa kwa ajili ya kuuza nje ili Tanzania waonekane nao wana mifugo iliyoboreshwa ambayo inakidhi masoko ya nje?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninampongeza kwamba, Longido ni kati ya wafugaji waliobadilisha na kuboresha mifugo yao na hivyo Mifugo ya Longido ina kila aina ya sifa inayotakiwa ili iweze kuuzwa nje.

Ninapenda kusema kwamba, tayari mipango imekuwepo na sehemu ya mipango hiyo ni kufunguliwa kwa soko la mpakani la Longido. Kwa hiyo, soko hilo la mpakani ni moja kati ya mikakati hiyo, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Kiwizara tayari tunajipanga na katika Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Mifugo, minada na mifugo iliyopo mpakani, itapewa mkazo zaidi katika kuboresha masoko hayo hasa ya nje ili wafugaji waweze pia kunufaika na pesa inayoweza kupatikana kwa ajili ya zao la mifugo yao.

Na. 343

Rushwa Kwenye Mgao wa Mbolea ya Ruzuku

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS aliuliza:-

Mfumo wa mgao wa mbolea ya ruzuku umegubikwa na rushwa na upendeleo kiasi cha kufikia kupoteza lengo la msingi la kusaidia wakulima maskini:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu Viongozi wa Vijiji wanaotuhumiwa kwa ufisadi kwenye mbolea ya ruzuku?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuondokana na Vocha za Mbolea na badala yake mbolea iuzwe kwa bei rahisi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kumekupo na ubadhirifu wa Vocha za Ruzuku ya Pembejeo katika baadhi ya maeneo hapa nchini uliofanywa na Watendaji wa Serikali, Mawakala wa Pembejeo na Watendaji wa Vijiji.

Katika mwaka 2009/2010, jumla ya kesi 22 zilifikishwa Mahakamani na katika mwaka huu wa 2010/2011, kesi 44 tayari zimefunguliwa katika Mahakama mbalimbali katika Mikoa ya Mwanza, Mara, Mbeya, Rukwa, Morogoro, Manyara, Kilimanjaro na Iringa. Kesi nyingi kati ya hizo, bado zipo katika hatua ya upelelezi.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupunguza bei ili mbolea iuzwe kwa bei rahisi kwa wakulima, ulijaribiwa katika mwaka 2003/2004 hadi mwaka 2010/2011. Bado upo upungufu ambao ni pamoja na walengwa wengi, ambao ni wakulima wadogo, kutonufaika na badala yake wafanyabiashara na wakulima wakubwa na mawakala kunufaika zaidi. Pamoja na mfumo wa vocha kugubikwa na ubadhirifu wa Watendaji niliowataja, katika maeneo ambayo Kamati za

Pembejeo za Mikoa na Wilaya zilifuata Waraka uliotolewa kuhusiana na usimamizi wa ruzuku ya pembejeo, zoezi hilo limekuwa na mafanikio. Ninapenda kuzitaja Wilaya za Sikonge na Songea kuwa ni mifano mizuri ya kuigwa katika usimamizi wa pembejeo.

Kwa kuwa, utaratibu huo umeonesha mafanikio katika baadhi ya maeneo, Serikali inaendelea kutafuta mbinu za kuboresha mfumo wa utoaji wa pembejeo yenye ruzuku, ikiwa ni pamoja na kuziba mianya inayotumiwa na Watendaji wasio waaminifu.

Aidha, kwa kushirikiana na Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, yaani CAG, Serikali inaandaa Ukaguzi Maalum (*Special Audit*), kuhusu utekelezaji wa mfumo wa pembejeo yenye ruzuku. Wizara yangu ipo tayari kupokea maoni na ushauri wowote wa kuboresha mfumo wa sasa wa utoaji wa pembejeo.

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba ni kweli kuna ufisadi katika utoaji wa mbolea kwa utaratibu uliopo ambao ni wa vocha na katika jibu lake la msingi emekiri kwamba kadiri miaka inavyoendelea kesi katika masuala haya zinaongezeka; na kwa kuwa vocha ya mbolea ambayo mkulima anaipata ni ndani ya ekari moja na hivyo haitoshelezi kwa mkulima mwenye ekari zaidi ya moja:-

(i) Je, Mheshimiwa Waziri anatwambia nini ama kuna mkakati gani wa kuwasaidia wakulima maskini ambao wana ekari zaidi ya moja na mbolea wanayopata haiwatoshelezi?

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri takriban wiki mbili zilizopita katika majibu yake alijibu kwamba katika Kanda za Kusini kuna mchakato wa kuanzisha Kiwanda cha Mbolea; na kwa kuwa tuna kiwanda kimoja cha mbolea cha Minjingu ambacho hakitoshi kuzalisha mbolea kwa wakulima wetu ambao wanahangaika; na kutokana na maelezo yake kuna mchakato wa kuanzisha kiwanda hicho; na kwa kuwa sera tuliyo nayo ni Sera ya Kilimo Kwanza...

SPIKA: Naomba uulize swali, kumekuwa na kwa kuwa nyingi mno.

MHE. RAYA IBRAHIM: KHAMIS: Kwa kuwa kuna Sera ya Kilimo Kwanza; na kwa kuwa Waziri amesema kwamba katika kuiimarisha Sera hiyo lazima tuwe na kiwanda cha mbolea kusaidia wakulima wetu; je, mchakato huo utachukua muda gani na ni lini utaanza? Uwe wa haraka zaidi kusaidia wakulima.

SPIKA: Hapa swali ni kuwa kiwanda kipo na mbolea inatosha kwa wakulima maskini; basi! Ninaomba Mheshimiwa Naibu Waziri ujibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninaomba nijibu maswali yote mawili ya Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mimi sijasema kwamba kuna ufisadi; nimesema kuna ubadhiri na wizi unaofanywa na baadhi ya watendaji wasio waaminifu. Nimekiri kwamba, upo na ndiyo maana baadhi yao wamefikishwa mahakamani na kesi ziko huko na hatuwezi kuziingilia mpaka zitakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea ambayo inatolewa kuwa kidogo; ninaomba nitoe ufafanuzi kwamba, Serikali haitoi mbolea kwa kila mkulima. Kwanza, itakuwa ni vigumu sana kwa kila Mkulima wa Tanzania sasa ategemee Serikali imletee mbolea. Utaratibu huu wa ruzuku, lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba, wakulima kadhaa ambao watakuwa mfano wanazoea kutumia mbolea, wakashazoea na tukishawajengea uwezo, baadaye sasa wataanza kununua mbolea wenyewe kutoka kwenye vyombo vinavyohusika. Ndiyo maana tunaanza Benki ya Kilimo na Taasisi nyingine. Lengo ni kuhakikisha kwamba, wakulima wanakuwa na uzoefu na uelewa mpana wa matumizi ya mbolea na baadaye tuwajengee uwezo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaona kwamba hata katika msimu huu, wale wakulima 740 tulioanza nao wataacha, tutawandoa sasa halafu linaingia kundi lingine tena. Hivyo, siyo lengo letu kumpatia kila mkulima mbolea hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwanda ni kwamba, nilijibu ninadhani Mheshimiwa Mbunge ameshindwa tu kulikumbuka vizuri au kuchanganua maswali yake; mchakato unaendelea na nilieleza kwamba, kiwanda hicho kitajengwa Mtwara na mchakato upo unaendelea na kitatumia gesi asili ambayo tunayo hivi sasa.

Na. 344

Utekelezaji wa Miradi ya Mifereji ya Umwagiliaji

MHE. STEPHEN J. MASELE aliuliza:-

Serikali inatekeleza Miradi mikubwa mitatu ya Ujenzi wa Mifereji ya Umwagiliaji katika Kata za Kitangile, Mwamalili/Seseko na Kizumbi eneo la Mwamashele kwa kutumia maji ya mito na mifereji ya muda:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Mwamalili/Seseko ambao umekaribia kukamilika?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya Mradi wa Kizumbi eneo la Mwamashele ambao usanifu wa upembuzi umekamilika?

(c) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuchimba mabwawa ya kuvuna maji ya mito hiyo ili yaweze kutumika wakati wote wa mwaka na kuongeza uzalishaji wa mpunga?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha Mradi wa Mwamalili, Serikali ilianza kutenga fedha kwa awamu tangu mwaka 2009 kwa ajili ya kuendeleza Mradi huu wa umwagiliaji. Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 300 zimekwishatolewa kwa ajili ya kujenga banio na mfereji mkuu wenye urefu wa kilomita 2.6. Mradi huu unanufaisha vijiji vya Mwamalili (hekta 260) chenye kaya 501 na Seseko (hekta 150) chenye kaya 280.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi kwa upande wao wanaendelea kuchangia nguvu zao kwa kuchimba mfereji wenye urefu wa mita 900, ambapo ujenzi wa kivuko cha korongo (*cross drainage structure*) ukifanyika, utawezesha Kijiji cha Seseko kufikiwa na maji ya umwagiliaji. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha Mradi huo wa Mwamalili kutoka katika vyanzo vingine ili kuukamilisha.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2010/2011, Serikali ilitenga na kutoa fedha kiasi cha shilingi milioni 300 kutoka Mfuko wa *DIDF* kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Mwamashele, wenye hekta 450, unaotarajiwa kunufaisha kaya 1,074. Hatua ya zabuni imekamilishwa na Bodi ya Zabuni ya Manispaa ya Shinyanga na Mkandarasi amepatikana kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Mradi huo. Aidha, Mradi huo sasa umetengewa fedha za nyongeza kiasi cha shilingi milioni 250 kutoka Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*District Irrigation Development Fund*) katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu umuhimu wa kuchimba mabwawa ya kuvuna maji katika mito ya msimu ili yatumike wakati wote wa mwaka na kuongeza uzalishaji wa mazao. Nia ya Serikali ni kuvuna maji ya mvua kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa hususan katika maeneo kama Mkoa wa Shinyanga. Hatua ya kwanza ambayo

imekuwa ikitumika kutekeleza miradi ya teknolojia ya kuvuna maji ni kujenga mabanio, mifereji na majaruba ili kuyanasa maji ya mito wakati wa masika, hata kama mvua inanyesha mbali kutoka kwenye skimu husika ili kumhakikishia mkulima kupata maji shambani wakati wa msimu wa masika angalau mara moja kwa mwaka. Gharama za utekezaji wa mradi katika hatua hii ni nafuu na unaweza kuwanufaisha wakulima wengi. Hatua ya pili ni kujenga mabwawa katika sehemu ambapo sura ya ardhi inaruhusu ujenzi wa mabwawa.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Serikali imetekeleza Mradi wa Seseko/Mwamallili kwa asilimia hamsini na katika bajeti ya mwaka huu haijatenga fedha hata kidogo za kuukamilisha Mradi huo; je, Waziri anawaeleza Wananchi wa Shinyanga kwamba atatoa wapi fedha zingine kwa ajili ya kukamilisha Mradi huu?

(ii) Kwa kawaida sisi Wasukuma ni aibu kuomba chakula na mara nyingi nimekuwa nikisema hapa kwamba tunaomba Serikali itujenge mabwawa kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua; je, Serikali itatekeleza lini dhamira ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameleza ya kuvuna maji ya mvua katika Mkoa wa Shinyanga na Mikoa mingine ya jirani ambayo inakabiliwa na njaa kila mwaka?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stephen Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mradi wa Seseko unaendelea lakini haujakamilika na nimekwishazungumza na Mheshimiwa Mbunge vizuri, tumekwishaelewana kabisa kwamba, nia ya Serikali ni kukamilisha Miradi yote ambayo ni endelevu. Kwa hatua iliyofikia Mradi huu wa Seseko, tunayo kila sababu ya kuutafuta fedha kutoka vyanzo vingine na nilitoa mifano michache tu kwamba, tunao Mfuko wa Pamoja kati ya Tanzania na Japan, ambao unatusaidia kuendeleza Miradi ya Umwagiliaji. Mifuko hiyo siyo lazima tuilete hapa Bungeni, ndiyo maana tumezungumza na Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutatafuta vyanzo vingine ili tuweze kuhakikisha Mradi huu unakamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ipo *DASP* katika Mkoa wa Shinyanga na Mikoa ya Ukanda wa Ziwa. Kwa hiyo, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mradi huu nao tutaukamilisha kwa sababu ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvunaji wa maji katika Mikoa hii, nilijibu pia swali hili na kusema kwamba, katika mpango wetu huu ambao tumeufikisha hapa Bungeni wa Miaka Mitano, umetaja mle ndani kwamba, tutajenga mabwawa 33. Yale ni mabwawa makubwa ambayo yanalenga kuvuna maji na hususan katika mikoa hii kame ya Shinyanga, Tabora, Singida na Dodoma. Kwa hiyo, Shinyanga nayo ni sehemu mojawapo ambayo tunaipa kipaumbele, tuna hakika kabisa kwamba, wakilibua Miradi ikapitia kwenye *DADPs* ikaletwa, tutatweza kujenga Miradi ambayo hatujajenga. Hii ni pamoja na hata mifereji mingine ambayo haikutajwa kama nilivyosema kama kule Mkomazi kwa Mheshimiwa Profesa Maji Marefu, ile mifereji tutajenga sisi wenyewe Serikali na kazi ya mfereji ni yetu sisi na Maji Marefu na Wananchi wa kule na siyo wale Wabunge wengine wanaokwenda kusema watawajengea.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninataka kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Manispaa ya Shinyanga imekuwa ikikumbwa na ukame mkubwa hasa kipindi cha mwaka wa 2011; na kwa kuwa mito na mifereji hiyo imekuwa ikisubiria mvua ndiyo ijae; je, Serikali haioni sasa baada ya Miradi hiyo kukamilika itumie maji yanayotoka Ziwa Victoria ambayo sasa hivi tayari yako Mkoa wa Shinyanga?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Ninaomba ujibu kwa kifupi sana, wakati mwingine majibu yenu yanakwenda mpaka dakika kumi haiwezekani.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, labda niseme ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tumeuchukua, lengo ni kutumia kila rasilimali tuliyonayo, lakini hizi rasilimali unajua tunapozitumia lazima pia tuangalie ni wakati gani tunatumia, ni kiasi gani na wakati mwingine ni lazima tushirikiane hasa maji ni rasilimali shirikishi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wake ni mzuri, tutajaribu kuuzingatia.

SPIKA: Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, unapopita mbele ya Kiti unainama, hupiti kama uko sokoni tu.

Na. 345

Matatizo ya Umeme Ukonga

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA aliuliza:-

Ingawa umeme ni kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii, lakini umekuwa ni kero kubwa katika Jimbo la Ukonga na Kata zake:-

(a) Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye maeneo hayo ya Ukonga na Kata zake?

(b) Kwa kuzingatia kuwa gharama za kuweka umeme ni kubwa; je, Serikali inasemaje kuhusu suala la kuwakopesha Wananchi hasa wenye kipato kidogo ili waweze kupata huduma hiyo na baadaye warejeshe mikopo hiyo kwa kulipa kidogo kidogo wakati wa kulipa bili za umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba, changamoto za kufikisha huduma ya umeme kwa Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam ni tofauti na maeneo mengine nchini, pamoja na kwamba nazo zina ugumu na ukubwa unaotokana na mazingira maalum ya Dar es Salaam na mahitaji yake. Kwa kutambua hayo, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*), imepanga katika bajeti ya mwaka huu wa 2011/2012, kukarabati njia za umeme, kuongezea nguvu vituo vidogo vya kupoza umeme vilivyozidiwa na kujenga njia mpya za umeme kwenye maeneo mapya ya Jimbo la Ukonga na Kata zake.

Ukarabati unafanyika katika njia kubwa tano za umeme msongo wa kV 11 na njia za umeme msongo wa kV 0.4 zinazopeleka umeme maeneo ya Kipawa, Kipunguni, Ukonga, Gongo la Mboto, Ulongoni na maeneo yanayopakana na maeneo hayo ya Ukonga, ambayo ni Banana, Kitunda, *Air Wing*, Majumba Sita, Mongo la Ndege na Machimbo Kipunguni. Maeneo ambayo vituo vidogo vidogo tisa vya kusambaza umeme vitaongezwa ili kuongeza nguvu ya umeme ni Gongo la Mboto, Kipunguni, Karakata, Vingunguti, Kiwalani na Ukonga Mombasa. Ujenzi wa njia mpya za umeme utahusisha jumla ya kilomita 8.5 kwa msongo wa kV 11 na kilomita tisa za msongo wa kV 0.4 kwa gharama ya shilingi milioni 210.

Maeneo mengine mapya ambayo yatasambaziwa umeme katika vituo vidogo 14 ni Gongo la Mboto, Kitunda, Ulongoni, Mwanagati, Kitunda Machimbo na Kibeberu pamoja na maeneo yanayoyazunguka. Kazi nyingine katika maeneo hayo ni ujenzi wa kilomita 13.5 za njia ya

umeme wa msongo wa kV 11 na kilomita 50 za njia ya umeme wa msongo wa kV 0.4. Miradi hii inakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.123

(b) Suala la *TANESCO* kupata mfumo utakaowapatia unafuu wa gharama wateja wanaokusudia kuunganisha umeme, limejibiwa hapa Bungeni mara kadhaa na utaratibu huo umeelezwa vizuri. Utaratibu huu ujulikanao kama *ACB Umeme Loan*, ulizinduliwa terehe 2 Juni, 2011. Chini ya utaratibu huo ni kwamba, mteja atakadiriwa gharama zake za kuunganisha umeme na *TANESCO* na kisha zitawasilishwa *Akiba Commercial Bank* na Benki huilipa moja kwa moja *TANESCO*. Mikoa itanayonufaika na huduma hii ni ile ambayo ina *branches* za *Akiba Commercial Bank*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukweli wa kikwazo cha gharama za juu za kuunganisha umeme, Serikali imeiagiza *TANESCO* kuangalia njia za kupunguza gharama za kuunganisha umeme, lakini pia kupanua wigo wa huduma zilizopo sasa hivi za kulipia kwa awamu, ikiwa ni pamoja na kushirikisha mashirika na taasisi za fedha nyingi zaidi ili Wananchi wengi wanufaika na utaratibu huo.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata jibu la jumla kutoka kwa Waziri. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Kata ya Msongola na Vijiji vyake vyote havijawahi kupata umeme; je, Serikali inawaambia nini Wananchi wa Jimbo la Ukonga katika suala zima la kuendelea kuishi katika giza?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimepokea taarifa kwamba, Kata ya Msongola haina umeme, lakini changamoto zilizopo kwenye Kata ya Ukonga ni kwamba; Ukonga ni Kata ambayo inapanuka haraka na wakazi wanaongezeka haraka sana na ndiyo maana kama ulivyoona hapa kuna vituo tisa vya kupooza umeme na nyaya na kilomita hamsini kwa kuwa Kata yenyewe ina wakazi wengi sana. Huku ni kama upande huu wa Mbagala na Kigamboni na huku chini maeneo ya Kawe kwa Mheshimiwa Halima Mdee. Kwa hiyo, kuna maeneo ya Dar es Salaam na ndiyo maana nikasema yana mazingira maalum, tumelipokea suala hilo na tutalifanyia kazi kwa Kata ya Msongola.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuniona.

Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali lake la msingi ameligusia suala la Kigamboni; Kigamboni ni Jimbo ambalo linakua kwa haraka sana; kuna Kata za Vijibweni, Kibada, Kisarawe II, Kimbiji, Somangira, Tuangoma na Pemba Mnazi, ambazo hazina umeme; na Kata ya Kigamboni na sehemu nyingine za Mbagala kwa sasa hivi zimezidiwa; je, Wizara ina mikakati gani ya kupeleka umeme katika maeneo ambayo nimeyataja?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati ninajibu swali la Ukonga kama alivyotaja mwenyewe ni kweli niliongeza na eneo la Kigamboni, kwa sababu Kigamboni ni katika maeneo ambayo kwa Dar es Salaam, yanapanuka haraka sana. Sasa umetaja Kimbiji na Pemba Mnazi, kule kidogo ni mbali lakini kwa haya maeneo uliyoyataja ya Kigamboni, Kibada na Vijibweni ni maeneo ambayo yanaweza kupata umeme na umeme wake unatokea huku Temeke na Mbagala. Mbagala yenyewe imezidiwa, kwa hiyo, kitakachofanyika ni kwamba, pale Mbagala pana ujenzi wa *sub station* kubwa ambayo yenyewe itapokea umeme moja kwa moja kutoka Ubungo. Ie ikishakamilika ina maana kwa maeneo ya Mbagala pale na kuja huku Kigamboni na kwa kweli labda nijiseme mwenyewe tu kwamba, mpaka Mkuranga, maeneo hayo yote yatakuwa yanapata umeme wa kutosha ikilinganishwa na ilivyo sasa.

Leseni Mpya za Madereva

MHE. MOSES J. MACHALI aliuliza:-

Je, ni lini leseni mpya za madereva zitaanza kutolewa kwa sababu Wananchi wanapofika Polisi na *TRA* huelezwa kuwa zinaandaliwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zoezi la utoaji wa leseni mpya za udereva lilianza rasmi kwa awamu ya kwanza hapa nchini tarehe 1 Oktoba, 2010 katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya zoezi hili, inahusisha mikoa kumi na nne ya Kigoma, Morogoro, Iringa, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Pwani, Singida, Manyara, Mara, Shinyanga, Kagera, Tabora na Rukwa. Ninapenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Mikoa hii imeanza kutoa leseni katika awamu ya pili, isipokuwa Mkoa wa Rukwa na Manyara. Kwa Mkoa wa Rukwa, kuna tatizo la jengo na kwa Mkoa wa Manyara kuna tatizo la Wakala. Tuko mbioni kumaliza matatizo haya mawili na shughuli ya kutoa leseni ianze mara moja.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. La kwanza, kiwango cha shilingi 40,000/= ambacho hutozwa wananchi mbalimbali ambao wana *interests* za kuwa Madereva kinaonekana kuwa kikubwa. Vilevile kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba wamekuwa wanatozwa zaidi ya kiwango hicho. Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuweza kuangalia jinsi gani ambavyo wanaweza wakadhibiti viwango ambavyo vinakuwa vinatozwa zaidi ya shilingi 40,000/= hasa kwenye ofisi za Ma-*Vehicle* wetu Mikoani?

Pili, hivi sasa inaonekana baadhi ya leseni kama vile Daraja "C" hapa nchini wanapewa watu ambao wamesoma kwenye Vyuo vya *NIT* lakini Serikali hiihi inatambua kwamba kuna baadhi ya Vyuo ambavyo vimesajiliwa kama vile Vyuo vya *VETA* na vyuo vya watu binafsi ambavyo pia hufundisha kozi za udereva. Je, Serikali haioni kuwa inajikanganya kwa kuwazuia vijana wetu na watu mbalimbali ambao wamesoma katika Vyuo vya *VETA* ambao wanakataliwa kupewa leseni za Daraja la "C" eti tu kwa sababu hawajasoma *NIT* na *NIT* imeonekana kwamba wanaorodhesha majina leo hii, wanatoa kozi kwa siku chache kama siku 10 tena huwezesha watu katika Mikoa mbalimbali kwamba ikitimia kiwango ambacho wanaweza wakapewa posho basi wataenda kwenda kufundisha. Tatizo ni nini, naomba majibu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kiwango cha shilingi 40,000/= ni kiwango ambacho kimewekwa na Serikali na tunaamini kabisa kwamba ni kiwango ambacho wananchi wengi wanaweza wakakimudu na mwenye magari, kama ni mabasi au malori na kadhalika. Pia tumesema kwamba pawe pana utaratibu ambapo wenye magari wenyewe wanaweza wakashirikiana na Madereva, sidhani kama hicho ni kiwango kikubwa. Isipokuwa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili suala la kwamba kumekuwa na pesa za ziada mbali na hizo shilingi 40,000/=, nimelisikia kwake kwa mara ya kwanza, niseme kwamba ni kinyume na taratibu na sheria. Kweli kama lipo, tutalifuatilia na tutachukua hatua ambazo zinastahili kuchukuliwa.

Swali la pili, kuhusu *NIT* na *VETA*, tumesikia malalamiko ya namna hiyo ama tuseme hoja za namna hiyo kutoka kwa wananchi mbalimbali mbali na Wabunge. Nitake kumhakikishia kwamba ni mambo ambayo tumeyachukua na tunayafanyia kazi na tutaona ni utaratibu gani kwa sababu Serikali tuliyokuwa nayo kama ninavyosema siku zote haiko hapa kuwabughudhi wananchi ama kuwaudhi wananchi. Tutafanya kitu ambacho kitasaidia kuhakikisha kwamba kazi za wananchi zinakwenda sawasawa.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza, kwa kuwa mpaka sasa hivi Vitambulisho vya Uraia bado havijapatikana Tanzania na kwa kuwa wako watu wanapenda kutumia Shahada zile za Kupigia Kura na hizi Leseni kama ndio utambulisho wao kwa masuala mbalimbali ya kifisi. Je, Serikali inatoa tamko gani la uhalali wa kutumia nyaraka hizo kama vitambulisho halali?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Mnyaa kwamba si suala la tamko kwa sasa hivi isipokuwa ukweli ni kwamba kama Taifa tuna tatizo kutokuwa na Vitambulisho vya Taifa na vile Vitambulisho katika shughuli nyingi ambazo zinazofanywa katika Taifa letu ni kumtambua nani raia wa nchi hii na nani sio raia wa nchi hii. Kitu ambacho naweza nikatamka hapa ni kwamba tuendelee na hili zoezi la kuwa na Vitambulisho vya Utaifa na mara tutakapokuwa tumemaliza kwa kuwa azma na nia ipo, kwa kuwa vitambulisho vya kwanza vitaanza kutoka mwisho wa mwaka huu na tutaendelea mpaka hapo tutakapokuwa tumekamilisha zoezi katika Taifa zima nadhani jibu lako litakuwa limejibika.

Sasa kwa kuwa Vitambulisho vile havipo, huwezi ukazuia wananchi kuchukulia vile Vitambulisho vya Kupigia Kura na kwa kweli vimekuwa vinatumika, ni vya kupigia kura lakini ndivyo ambavyo vimekuwa vinatumika katika Taifa letu lakini hivyo si Vitambulisho ambavyo unaweza kusema ni vitambulisho vya uraia. Nijibu tu kwa kusema kwamba vitakapokuwa Vitambulisho hivyo vitakapokuwa vimetoka tatizo hili litakuwa limekoma na tunategemea kwamba litakoma.

Na 347

Lugha ya Kufundishia Shule za Msingi

MHE. RIZIKI OMAR JUMA (K.n.y. MHE. AMINA M. MWIDAU) aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali imeruhusu Elimu ya Msingi katika Shule za Serikali kufundishwa kwa lugha ya Kiswahili na kwa Shule Binafsi kufundishwa kwa lugha ya Kiingereza?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mwidau, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, lugha ya kufundishia katika Elimu ya Msingi ni Kiswahili na Kiingereza hubaki kufundishwa kama somo la lazima. Matumizi ya lugha ya Kiingereza yanazingatia mahitaji ya baadhi ya wadau wa elimu wakiwemo wanaopendelea lugha hiyo, yaani raia wa nchi za kigeni, Mabalazi wetu, Wanadiplomasia na Maofisa Waandamizi wanaotumikia Balozi zao hapa nchini ambao hutumia Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, inaruhusu pia sekta binafsi kumiliki na kuendesha shule. Kiswahili husaidia wanafunzi katika kuendeleza mila, utamaduni, kujenga umoja na uzalendo, wakati Kiingereza kinasaidia kuiunganisha Tanzania Kimataifa katika masuala ya teknolojia, biashara na utawala.

Mheshimiwa Spika, kuna shule za msingi tisa (9) za Serikali zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia. Vilevile kuna shule za msingi ishirini na mbili (22) za binafsi zinazotoa elimu ya msingi kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia malengo ya elimu na mahitaji mbalimbali ya wadau ndio maana kuna matumizi ya lugha hizo mbili kwa msisitizo tofauti ili kuweza kuwafikia watoto wote na kutekeleza kikamilifu Sera ya Elimu kwa wote.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Sera ya Elimu, lugha ya kufundishia ni ya Kiswahili lakini kwa mawazo yangu kwa sababu kuna matumizi ya lugha tofauti katika shughuli zetu, zile za binafsi na zile za Kiingereza, hatuoni

kwamba wanafunzi wengine watakuwa tunawanyima ile fursa au watakuwa hatuendi sambamba na ile Sera ya Kufundishia katika Taifa letu wakati mmesema lugha ya Kiswahili ndio lugha ya Taifa? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye Sera ya mwaka 1965 kwamba tuko huru na lugha ya Kiingereza ni lugha ya Kimataifa na lugha ya Kiswahili pia. Kama nilivyosema kwamba lugha ya Kiingereza inatoa ufahamu hasa katika masuala ya kiutawala, teknolojia na masuala mengine ya kibiashara katika ulimwengu wa utandawazi lakini vilevile lugha ya Kiswahili ni lugha yetu ya Taifa kwa kulinda mila zetu, utamaduni na hata kutambulisha sisi kama ni Watanzania, lazima tutambulike huku kwenye Mataifa kwamba tunatumia lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, lugha zote hizi mbili ni muhimu kufundishia katika Shule za Msingi na hata sekondari.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge muda umeisha na umeisha sana na maswali pia yamekwisha.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wachache katika ukumbi wetu ambao tunawatambulisha. Kwanza tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Naibu Waziri wa Ujenzi naye sio mwingine isipokuwa mke wake mpendwa Linah Mwakyembe. Anakuja kusikiliza mume wake atakapokuwa anasulubiwa. *(Makofi)*

Tuna viongozi wengine wa Wizara ya Ujenzi yupo Katibu Mkuu, Balozzi Herbert H. Mrango, ahsante. Tuna Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Eng. John Ndunguru. Wapo na Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo mbalimbali kwa sababu leo ni Wizara yao. Wapo Wenyeviti wa Wakala na Taasisi za Wizara ya Ujenzi ambao ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, Dkt. James Wanyancha. Huyu alikuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mbunge mwenzenu mpaka juzi tu. Kwa niaba yake nasema ahsante sana. Wanakupigia makofi wakijua barabara ndio wewe upo pale. *(Makofi)*

Tuna Mwenyekiti wa Wakala za Majengo, ni Dkt. Edward Ngwale, ahsante sana. Tuna Mwenyekiti wa Wakala wa Ufundi na Umeme, Prof. Idrisa Mshoro. Tuna Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Prof. Ninatubu Lema. Tuna Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi, ni Eng. Consolata Ngimbwa, afadhali angalau wanaonekana wengine wapo. Tuna Kaimu Mwenyekiti, Bodi ya Wakala wa Barabara, Ndugu Richard Rugimbana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu tuna Watendaji Wakuu wa Wakala na Taasisi za Wizara ya Ujenzi na hao wasimame sijui wako wapi, wengine wote walikuwepo hapa, ahsante sana. Tuna Mameneja wa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* wa Mikoa yote Tanzania Bara, wasimame wote walipo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnawaona hao kila mtu anamjua wa kwake hapo, ahsante sana Mameneja. *(Makofi)*

Tuna Wawakilishi wa *Association of Consulting Engineers Tanzania (ACET)*. Wawakilishi wake wasimame sijui wako wapi? Ahsante yuko mmoja. *(Makofi)*

Wageni wengine yuko Ndugu Nape M. Nnauye, Katibu wa Itikadi na Uenezi ya CCM Taifa. Ahsante. Waheshimiwa Wabunge inatosha ahsante. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo hawa ni kikundi cha akinamama kutoka Usharika wa Arusha Road Dodoma. Wako wapi akinamama hawa. Kikundi cha Usharika, nafikiri wamekosa nafasi watakuwa pale kwenye *basement*. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi tisa (9) kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wako wapi, ahsante, karibuni. *(Makofi)*

Tuna Madaktari na Manesi wanaotoa huduma ya kuwapima afya Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni. Naomba wasimame Manesi wetu, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mnakwenda kupima afya zenu, sio kupiga chenga. Mpaka wamekuja kujionyesha wenyewe kwamba wengine hamjui kama wapo, kwa hiyo mkapima afya zenu. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 45 na Walimu watano (5) kutoka Shule ya Msingi ya *Rainbow* Dodoma. Wako wapi Walimu na Wanafunzi wa *Rainbow*. Aaah, ndio ninyi wazuri kabisa. Karibuni, karibuni sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna shughuli za kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake ya Kudumu kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati katika ukumbi Na. 219, ghorofa ya pili, jengo la Utawala. Kwa hiyo, Wajumbe wote saa 7.00 mchana, chumba namba 219. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana watakuwa na kikao chumba Na. 227.

Katibu wa Kamati ya Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM, Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wanawake wote wa CCM kwamba leo watakutana katika Ukumbi wa Pius Msekwa saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge.

Naona na mwingine tena, Katibu wa Kamati ya Wabunge Wanawake wa CCM, Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o naye anatangaza tangazo hilo kwamba watakutana saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Ofisini kwangu mimi natangaza kwamba saa 7.00 mchana, leo Kamati ya Uongozi maana yake Wenyevidi na kama Mwenyekiti hayupo Makamu Mwenyekiti, tutakuwa na kikao kifupi saa 7.00 mchana kujaribu kufikiria utaratibu utakaotumika wakati huu wa Mwezi wa Ramadhani. Kwa hiyo saa 7.00 mchana tutakuwa na kikao ili tuweze kupanga utaratibu wa kuweza kuona wenzetu wanaofanya kazi ya mfuno wa Ramadhani wanafanyaje katika kipindi kama hicho hasa ukizingatia muda. Kwa hiyo, nawaomba Wenyevidi wote tutahudhuria saa 7.00 mchana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kukumbushana Kanuni zetu leo hamkufanya vizuri kwa sababu zifuatazo. Staha ndani ya Bunge, Mbunge aliyepo Bungeni wakati wote wa mjadala anatakiwa kuingia au kutoka kwenye ukumbi wa Bunge kwa staha na atainamisha kichwa kuelekea kwa Spika au kufanya mkunjo wa magoti kwa heshima kila mara Mbunge huyo atakapokuwa akienda au kutoka mahali pake, hiyo moja.

Lakini ya pili ndiyo kubwa zaidi, kutulia na kukaa kwa heshima mahali pake na hatatangatanga kwenye ukumbi wa Mikutano bila sababu. Sasa hili nalisema mara nyingi watu wamekuwa wanatangatanga na kwamba kutakuwa na kukaa kwa utulivu. Waheshimiwa Wabunge, hapa ukimsimamisha mtu ukimuuliza kwamba tunaendelea kuongea nini hapa, hawezi kusema kwa sababu alikuwa na biashara yake, anaongea na kuzungukazunguka ndani ya ukumbi, sasa watakaokuwa wanazunguka ninawataja majina na watakaokuwa wanaongea tunawaita kwa majina. Sasa hapo basi mtaoneshwa kwa wananchi waliowapigieni kura kazi yenu kutangatanga kwenye ukumbi. Kwa hiyo, msome hizo Kanuni muweze kuzielewa. Tunaendelea na shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Wizara ya Ujenzi

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha pili. Hii inadhahirisha jinsi ambavyo wananchi wa Tanzania walivyo na imani kwake na kwa Serikali anayoiongoza. Aidha, napenda kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuishukuru Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini, kwa kuendelea kutupa ushirikiano wa kutosha katika kuiongoza Sekta hii. Ushauri na maelekezo yao mazuri yaliwezeshwa Wizara kutekeleza mipango ya utendaji, kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma zitolewazo na sekta. Ushauri wa Kamati na Wabunge wote utaendelea kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, katika kuwapongeza na kuwashukuru Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mashariki na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa jumla katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012. Naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba za Mawaziri waliotangulia. Ni matumaini yangu kuwa, maoni yao yatasaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi iliundwa na Serikali ya Awamu ya Nne baada ya kutenganishwa kwa iliyokuwa Wizara ya Miundombinu. Wizara ya Ujenzi ilipewa jukumu la kusimamia Sekta za Ujenzi ambayo ni kichocheo kikubwa katika ukuaji na maendeleo ya sekta za kiuchumi na kijamii nchini. Wizara inatekeleza majukumu na mipango yake kwa kuzingatia Iiani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na 2010, ahadi za Mheshimiwa Rais na Serikali, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 (*National Development Vision 2025*) na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Aidha, Wizara ya Ujenzi inazingatia Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Miundombinu ya Uchukuzi (*Transport Sector Investment Program – TSIP*) ambayo ni programu ya miaka kumi (2007-2017) inayolenga kuimarisha na kuboresha miundombinu ya uchukuzi, Sera na Sheria ya Uhifadhi wa Mazingira na malengo ya Kimataifa kama vile Malengo ya Maendeleo ya Milenia (*Millenium Development Goals- MDGs*).

Mheshimiwa Spika, dira ya Wizara ni kuwa na Barabara, Vivuko, Nyumba za Serikali na Huduma za Ujenzi zenye ubora wa kiwango cha juu, zenye gharama nafuu, zinazozingatia usalama na utunzaji wa mazingira. Aidha, dhamira ya Wizara ni kuwa na Barabara, Vivuko, Nyumba za Serikali na Huduma za Ujenzi; ambazo ni salama; zinazotegemewa; zilizo na uwiano na ambazo zinakidhi mahitaji katika kiwango bora na kwa bei nafuu zinazoendana na mikakati ya Serikali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii na wakati huo huo zikiwa endelevu kiuchumi na kimazingira.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi imekabidhiwa majukumu ya kusimamia ujenzi na matengenezo ya Barabara, Madaraja na Vivuko pamoja na ukarabati wa Majengo ya Serikali na Masuala ya Ufundi. Aidha, Wizara inahusika na shughuli za Uhandisi na Usanifu wa Ujenzi, masuala ya Usalama na Mazingira pamoja na uboreshaji wa Utendaji na Uendelezaji wa Watumishi wa Wizara. Pia, Wizara husimamia majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake, Wizara imejiwekea malengo ya:-

Kuhakikisha kuwa Miji yote Mikuu ya Mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo mwaka 2017/2018 na kuendelea kusimamia na kudhibiti wataalamu wa sekta mfano; Makandarasi, Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiraji Majenzi kwa kutumia bodi husika. Aidha, Wizara itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya ujenzi. Wizara pia itaendelea kushirikiana na taasisi husika katika kushughulikia masuala mtambuka kama vile kampeni za kupunguza maambukizi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI, uhifadhi

wa mazingira, masuala ya jinsia pamoja na uendelezaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali. Ili malengo haya yatimie Wizara itaweka mazingira mazuri ya Makazi kwa Watumishi wa Umma kwa kuiwezesha Miradi ya Ujenzi wa nyumba za kuishi pamoja na Majengo ya Serikali. Wizara pia itaendelea kusimamia Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 hususan kifungu cha 29 (1) kinachohusu matumizi ya Hifadhi ya Barabara (*Road Reserve*) pamoja na Sheria nyingine zinazohusu utunzaji na utumiaji wa barabara.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Wizara katika kufikia malengo. Ili kuweza kutekeleza malengo yake, Wizara imeweka mikakati ya kuendelea kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha, hususan fedha za Mfuko wa Barabara zinazopelekwa Mikoani na Wilayani ikiwa ni pamoja na kuwabana wadau wote wanaohusika na shughuli za ujenzi ili kazi zilingane na thamani ya fedha (*value for money*). Aidha, Wizara itaendelea kuzifanyia marekebisho Sheria za kisekta ili ziweze kuendana na mazingira ya mifumo ya kiutendaji na kufikia viwango vinavyokubalika Kimataifa na Kikanda kama vile *EAC* na *SADC* katika kutekeleza Sera za Ujenzi na Sera ya Usalama Barabarani. Wizara pia itasimamia utoaji elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya barabara kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 pamoja na Sheria zingine ili miundombinu iweze kutunzwa na kudumu kwa muda uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni pamoja na kuendelea kutekeleza Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Uchukuzi (*Transport Sector Investment Programme – TSIP*) kwa kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Sahihi (*Appropriate Technology*) katika sekta ya ujenzi na kujenga mazingira mazuri yatakayoweza ushiriki wa sekta binafsi chini ya mfumo wa *Public Private Partnership*. Aidha, Wizara itahakikisha Makandarasi, Wahandisi Washauri na Wasanifu Majenzi wa kizalendo wanahusishwa kikamilifu katika ujenzi wa miradi mikubwa hasa ya barabara inayogharamiwa na Serikali badala ya kutegemea Kampuni za nje ili kuwajengea wananchi uzoefu stahili katika sekta ya ujenzi na kupunguza kasi na wingi wa fedha zinazotokana na vyanzo vyetu kuhamishiwa nje ya nchi kwa kulipia kazi za Kampuni za nje.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2010/2011. Ukusanyaji wa mapato na matumizi ya kawaida. Katika mwaka 2010/11, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi 42,100,000.00 kupitia Idara za Utawala na Huduma za Kiufundi pamoja na Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi. Hadi Mei, 2011, jumla ya shilingi 51,852,540.80 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 123. Sababu za kukusanya fedha zaidi ni kuwa makusanyo yaliyopatikana kutokana na Marejesho ya Serikali (*Recovery of Public Money*) na makusanyo mchanganyiko (*miscellaneous receipt*) ni makubwa ikilinganishwa na makadirio.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilitengewa shilingi 298,495,949,166.40 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi Mei 2011, Shilingi 261,492,533,257.50 zilitolewa na Hazina sawa na asilimia 87.6.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2010/2011. Katika mwaka wa 2010/2011, Wizara ilitengewa shilingi 710,945,105,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 275,902,770,000 ni za ndani na shilingi 435,042,335,000 ni za nje. Aidha, katika mwezi Machi 2011, bajeti ya Wizara iliongezwa kwa shilingi 255,000,000,000 kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi wa barabara. Fedha zilizotolewa hadi Mei, 2011 ni shilingi 364,590,800,000 (shilingi 246,897,190,000 za ndani na shilingi 117,693,610,000 ni fedha za nje).

Mheshimiwa Spika, miradi ya barabara. Katika mwaka 2010/2011, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ilipanga kujenga kilometa 392.1 za barabara kuu kwa kiwango cha lami, kukarabati kilometa 216.8 kwa kiwango cha lami na kilometa 154.8 kwa kiwango cha changarawe. Hadi kufikia Mei 2011, ujenzi wa miradi ya barabara kuu kwa kiwango cha lami ulifikia kilometa 203.6 sawa na asilimia 52 ambapo jumla ya kilometa 154.8 za ukarabati kwa kiwango cha lami ulikamilika sawa na asilimia 71.4. Aidha, kilometa 77.5 za barabara kuu sawa na asilimia 55 zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Kuhusu matengenezo ya barabara kuu, lengo lilikuwa ni kuzifanyia matengenezo kilometa 10,262 na madaraja 1,140. Hadi kufikia Mei, 2011 utekelezaji ulikuwa umefikia kilometa 6,730 sawa na asilimia 65 na madaraja 631 yalikuwa yamefanyiwa matengenezo sawa na asilimia 55.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Mikoa, Wizara ilipanga kujenga kilometa 1,350.9 kwa kiwango cha changarawe, kilometa 98.55 kwa kiwango cha lami na kukamilisha ujenzi wa madaraja 17. Kati ya hizo, kilometa 327.8 za changarawe, kilometa 30 za lami na daraja 1 zilipangiwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Hadi kufikia Mei 2011, jumla ya kilometa 777.7 zilikuwa zimekamilika kwa kiwango cha changarawe (sawa na asilimia 55.6), ambapo kilometa 31.64 zilijengwa kwa kiwango cha lami (sawa na asilimia 41.3) na madaraja manne sawa na asilimia 22 yalikamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matengenezo ya barabara za Mikoa Wizara ilipanga kuzifanyia matengenezo kilometa 20,055 na madaraja 1,129. Hadi kufikia Mei 2011 jumla ya kilometa 11,635 zilikuwa zimekamilika sawa na asilimia 58 na madaraja 757 sawa na asilimia 67 yalikuwa yamefanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kudhibiti uzito wa magari iliendelea katika mwaka wa fedha 2010/11 kwa kutumia mizani 25 ya kudumu na 17 inayohamishika katika barabara kuu za lami. Hadi Mei 2011 magari yapatayo 2,206,378 yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo 506,219 yalikuwa yamezidisha uzito. Hii ni sawa na asilimia 23 ya magari yaliyopimwa. Jumla ya fedha iliyokusanywa kutokana na tozo ya uharibifu wa barabara na malipo ya kupitisha mizigo mipana na isiyo ya kawaida ilikuwa ni shilingi milioni 3,008.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia lengo la kuhakikisha kuwa Mikoa yote nchini inaunganishwa kwa barabara za lami, miradi yenye jumla ya kilometa 11,154.35 imekamilika au inaendelea kutekelezwa katika nchi nzima katika awamu hii. Miradi hiyo iko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa barabara ya Kagoma – Biharamulo - Lusahunga (km 154), kazi zilianza tarehe 16 Septemba, 2009 na zimefikia asilimia 41. Kazi zimepangwa kukamilika tarehe 15 Julai, 2012. Gharama ni shilingi bilioni 191.46 na Mkandarasi ni CHICO na Msimamizi ni *Intercontinental*.

Mradi wa barabara ya Isaka-Lusahunga (km 242) umegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

(i) Isaka-Ushirombo (km 132):

Kazi zilianza tarehe 18 Februari 2010 na zimefikia asilimia 20. Kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 17 Mei 2013. Gharama ni shilingi bilioni 145.34 na Mkandarasi ni CHICO na Msimamizi ni Nicholas O'Dwyer.

(ii) Ushirombo-Lusahunga (km 110):

Kazi zilianza tarehe 18 Februari 2010 na zimefikia asilimia 20 na zinatarajiwa kukamilika tarehe 17 Agosti 2012. Gharama ni shilingi bilioni 114.56 na Mkandarasi ni Strabag na Msimamizi ni Nicholas O'Dwyer.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Kahama Mjini (km 5), ujenzi wa km 1.5 za awamu ya pili umekamilika mwezi Machi 2011 kwa gharama ya shilingi milioni 760. Hatua inayofuata ni kutafuta fedha za kumalizia ujenzi wa sehemu iliyobaki. Kuhusu barabara ya Kyaka-Bugene (km 59.1), mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinategemewa kukamilika tarehe 29 Oktoba 2012. Gharama ni shilingi bilioni 64.96 na Mkandarasi ni CHICO. Aidha, barabara ya Bariadi-Lamadi (km 71.8), kazi zilianza tarehe 8 Julai 2010 na zimefikia asilimia 6.4. Kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 7 Januari 2013. Gharama ni shilingi bilioni 67.41 na Mkandarasi ni *China Communication*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sumbawanga-Matai-Kasanga Port (km 112), kazi zilianza tarehe 13 Januari, 2010 na zinafanyika kwa njia ya Kusanifu na Kujenga (*Design & Build*). Kazi za usanifu wa kina zimefikia asilimia 55. Kazi za ujenzi zimepangwa kukamilika tarehe 12 Januari, 2013

kwa gharama ya shilingi bilioni 133.29. Mkandarasi ni *China Railways*. Kwa barabara ya Tunduma-Sumbawanga (km 231), mradi huu unagharamiwa na fedha za *MCC* na umegawanyika katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

(i) Tunduma-Ikana (km 63.7):

Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 22 Septemba 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 21 Septemba 2012. Gharama ni shilingi bilioni 82.52 na Mkandarasi ni *Consolidated Group* na Msimamizi ni kampuni ya *Egis BCEOM*.

(ii) Ikana-Laela (km 64.2):

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 17 Septemba 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 16 Septemba 2012. Gharama ni shilingi bilioni 76.1 na Mkandarasi ni *China New Era* na Msimamizi ni Kampuni ya *Egis BCEOM*.

(iii) Laela-Sumbawanga (km 95.1):

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 1 Aprili 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 1 Novemba 2012. Gharama ni shilingi bilioni 130.1 na Mkandarasi ni *Aasleff* na Msimamizi ni kampuni ya *Egis BCEOM*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sumbawanga-Kanyani-Nyakanazi (km 829) imegawanywa katika sehemu nne kama ifuatavyo:-

(i) Sumbawanga-Kanazi (km 75):

Kazi zilianza tarehe 16 Desemba 2009 na ujenzi unaendelea. Kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 16 Desemba 2012. Gharama ni shilingi bilioni 78.84 na Mkandarasi ni *Jiangxi*.

(ii) Kanazi-Kizi-Kibaoni (km 76.6):

Kazi zilianza tarehe 16 Desemba 2009 na ujenzi unaendelea. Kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 16 Desemba 2012. Gharama ni shilingi bilioni 82.84 na Mkandarasi ni *CHICO*.

(iii) Kizi-Sitalike-Mpanda (km 95):

Usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

(iv) Mpanda-Uvinza-Kanyani-Nyakanazi (km 582.4):

Usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Marangu-Rombo Mkuu na Mwika-Kilacha (km 34), kazi zilianza tarehe 17 Juni, 2008 na zimefikia asilimia 80 na zimepangwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 25.1 na Mkandarasi ni *General Nile* na Msimamizi ni *UNETEC*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kwa Sadala-Masama (km 12.5), kazi zilianza tarehe 10 Machi 2010 na ujenzi unaendelea. Kazi zinatarajiwa kukamilika katika mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 5.34 na Mkandarasi ni *ATLANTIC* na Msimamizi ni *CROWN TECH*.

Aidha, barabara ya Kibosho Shine – Kwa *Rafael-International School* (km 43), kazi zilianza tarehe 2 Machi 2010 na ujenzi unaendelea. Kazi zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 8.93 na Mkandarasi ni *DOTT SERVICES* na Msimamizi ni *CROWN TECH*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Rau Madukani-Mawela-Uru Njari (km 12.5), kazi zilianza tarehe 2 Machi 2010. Ujenzi unaendelea na kazi zinatarajiwa kukamilika mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 4.88 na Mkandarasi ni *DOTT SERVICES* na Msimamizi ni *Inter-Consult*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilua Nduoni-Marangu Mtoni (km 31.5), kazi zilianza tarehe 2 Machi 2010. Ujenzi unaendelea na kazi zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 9.10 na Mkandarasi ni *DOTT SERVICES* na Msimamizi ni kampuni ya *Inter-Consult*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Arusha-Namanga (km 105), kazi zilianza tarehe 14 Julai, 2008 na zimefikia asilimia 80. Kazi zinatarajiwa kukamilika Desemba 2011. Gharama ni shilingi bilioni 81.77 na Mkandarasi ni China Geo na Msimamizi ni John Burrow.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Arusha-Minjingu (km 104) mkataba wa ukarabati ulisainiwa tarehe 12 Mei 2011 na ukarabati unagharamiwa na fedha za mkopo toka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Minjingu-Babati-Singida (km 223.5) utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

(i) Singida-Kateshi (km 65.1):

Kazi zilianza tarehe 11 Machi, 2009 na zimefikia asilimia 61 na zinatarajiwa kukamilika Septemba 2011. Gharama ni shilingi bilioni 51.63 na Mkandarasi ni *SINOHYDRO* na Msimamizi ni *AFRICON*.

(ii) Kateshi-Dareda (km 73.8):

Kazi zilianza tarehe 11 Machi, 2009 na zimefikia asilimia 46. Kazi zitakamilika mwishoni mwa 2011. Gharama ni shilingi bilioni 64.14. Mkandarasi ni *SINOHYDRO* na Msimamizi ni *COWI*.

(iii) Dareda-Babati-Minjingu (km 84.6):

Kazi zilianza tarehe 11 Machi, 2009 na zimefikia asilimia 75 na zinatarajiwa kukamilika tarehe 10 Machi, 2012. Gharama ni shilingi bilioni 84.92 na Mkandarasi ni *CHICO* na Msimamizi ni *Crown Tech*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tanga-Horohoro (km 65) ujenzi unaendelea kwa fedha za *MCC*. Mkandarasi ni *SINOHYDRO* na Msimamizi ni *Intercontinental*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Korogwe-Handeni (km 65) kazi zilianza tarehe 15 Februari, 2010 na zimefikia asilimia 19 na zinatarajiwa kukamilika tarehe 14 Mei, 2012. Gharama ni shilingi bilioni 63.2 na Mkandarasi ni *SINOHYDRO* na Msimamizi ni *SMEC*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Handeni-Mkata (km 54) kazi zilianza tarehe 28 Desemba, 2009 na zimefikia asilimia 32 na zinatarajiwa kukamilika tarehe 17 Novemba 2011. Gharama ni shilingi bilioni 57.34 na Mkandarasi ni *SINOHYDRO* na Msimamizi ni *SMEC*.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa Mziha-Turiani-Magole (km 84.6) umegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

(i) Magole – Turiani (km 48):

Kazi zilianza tarehe 3 Machi, 2010 na zimefikia asilimia 23.29 na zinatarajiwa kukamilika tarehe 2 June 2012. Gharama ni shilingi bilioni 48.2 na Mkandarasi ni *China Civil Engineering*.

(ii) Turiani – Mziha (km 36.6):

Usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dumila – Kilosa (km 63) imegawanywa kama ifuatavyo:

(i) Dumila-Ludewa (km45):

Kazi zilianza tarehe 1 Februari 2009 na zimefikia asilimia 30. Kazi hii inatarajiwa kukamilika tarehe 10 Februari 2012. Gharama ni shilingi bilioni 41.93 na Mkandarasi ni *China Civ. Eng* na Msimamizi ni *SMEC*.

(ii) Ludewa-Kilosa (km 18):

Usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Msimba-Ikokoto-Mafinga (km 219) imegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

(i) Msimba-Ruaha-Mbuyuni/Ikokoto-Mafinga (km 149.6):

Kazi za ukarabati zimefikia asilimia 80 kwa fedha za DANIDA na zinatarajiwa kukamilika tarehe 18 Septemba 2011. Gharama ni shilingi bilioni 127.7 na Mkandarasi ni Aarslef na Msimamizi ni *COWI*.

(ii) Iringa-Mafinga (km 69.4):

Mchakato wa kumpata Mkandarasi unaendelea na utagharamiwa na fedha za *DANIDA*.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mbeya-Chunya-Makongorosi (km 115) umegawanywa katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

(i) Mbeya-Lwanjilo (km 36):

Mkataba mpya ulisainiwa mwezi Desemba 2010 baada ya Mkandarasi wa awali (Kundan Singh) kushindwa kazi na kufukuzwa. Mkandarasi mpya anaendelea na maandalizi ya ujenzi.

(ii) Lwanjilo-Chunya (km 36):

Kazi zilianza tarehe 5 Agosti, 2009 na zimefikia asilimia 66. Kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 4 Novemba 2011. Gharama ni shilingi bilioni 40.28 na Mkandarasi ni *China Communication* na Msimamizi ni *Nicholas O'Dwyer*.

(iii) Chunya-Makongorosi (km 43):

Usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara ya Ndundu-Somanga (km 60) kazi zilianza tarehe 15 Julai, 2008 na zimefikia asilimia 64 na zinatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2011. Gharama ni shilingi bilioni 58.82 na Mkandarasi ni Kharafi na Msimamizi ni *ESG*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara ya Masasi-Mangaka (km 55.1) kazi zilianza tarehe 9 Desemba 2009 na zimefikia asilimia 70. Kazi zinatarajiwa kukamilika katika mwaka 2011. Gharama ni shilingi bilioni 21.62 na Mkandarasi ni TOKURA na Msimamizi ni *Ingerosec Corporation* zote za nchini Japan.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Makofia-Msata (km 64), kazi zilianza tarehe 11 Agosti 2010 na zimefikia asilimia sita (6) na zinatarajiwa kukamilika tarehe 10 Agosti 2012 kwa gharama ya shilingi bilioni 89.61 na Mkandarasi ni *ESTIM* na Msimamizi ni Gauff.

Mheshimiwa Spika, kwa barabara ya Chalinze-Segera-Tanga (km 245), ukarabati wake unaendelea katika sehemu ya Kitumbi-Tanga (km 120) na unagharamiwa na fedha za DANIDA. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 24 Desemba 2010 na Mkandarasi yuko kwenye maandalizi ya kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara ya Korogwe – Mkumbara - Same (km 172), mchakato wa kumpata mkandarasi wa ukarabati uko kwenye hatua za mwisho na utagharamiwa na fedha za mkopo toka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kilwa/Dar es Salaam (km 12), mkataba ulisainiwa tarehe 19 Oktoba 2010. Mkandarasi ameanza kazi ya ujenzi wa km 1.5 zilizobaki wakati km 10.5 toka Bendera Tatu hadi Rangji Tatu ziko kwenye hatua ya kukamilishwa. Wizara imekataa kupokea sehemu hii ya barabara kutokana na upungufu uliojitokeza kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Mandela (km 16.8) kazi zilianza tarehe 1 Oktoba 2007 na zimekamilika tarehe 30 Juni 2011. Mradi huu uko kwenye kipindi cha matazamiao ya mwaka mmoja. Gharama ni shilingi bilioni 41.22 na Mkandarasi ni *Maltauro/Spenco* na Msimamizi ni *BCEOM*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Kawawa *Junction*-Mwenge-Tegeta (km 17) kazi za ujenzi kwa sehemu ya Mwenge – Tegeta zinaendelea kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Japan. Aidha, sehemu ya Mwenge – Kawawa *Junction* (km 4.3) itafadhiliwa pia na Serikali ya Japan.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Babati-Dodoma-Iringa (km 521) imegawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya Dodoma-Iringa (km 260):

Ujenzi unagharamiwa na fedha za mkopo toka *ADB* na *JICA* na kazi zimegawanywa katika sehemu tatu. Mikataba ya ujenzi ilisainiwa tarehe 13 Januari 2011 na kazi zinatarajiwa kukamilika mwezi Januari 2014.

(ii) Sehemu ya Dodoma-Babati (km 261):

Mradi huu ulikwishaanza katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

- Dodoma-Mayamaya (km 43.6):

Mkataba wa ujenzi umesainiwa mwezi Mei 2010 na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya ujenzi. Gharama ni shilingi bilioni 40.61 na Mkandarasi ni *SINOHYDRO*.

- Bonga-Babati (km 19.2):

Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 31 Mei 2010 na ujenzi umeanza. Gharama ni shilingi bilioni 19.69 na Mkandarasi ni *CHICO*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nzega-Tabora (km 115) imegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

- (i) Nzega-Puge (km 56.1)

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010. Kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Oktoba 2012. Gharama ni shilingi bilioni 66.36 na Mkandarasi ni *China Communication*.

- (ii) Puge-Tabora (km 58.8):

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Oktoba 2012. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 62.74 na Mkandarasi ni *SINOHYDRO*.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Manyoni-Itigi-Tabora (km 264) umegawanywa katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

- (i) Tabora-Nyahua (km 85):

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Julai 2013. Gharama ni shilingi bilioni 93.41 na Mkandarasi ni *Chongqing Foreign Trade*.

- (ii) Manyoni-Itigi-Chaya (km 89.4):

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Julai 2013. Gharama ni shilingi bilioni 109.64 na Mkandarasi ni *SINOHYDRO*.

- (iii) Chaya – Nyahua (km 90):

Sehemu hii usanifu wake umekamilika.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Tabora-Urambo (km 94) umegawanywa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

- (i) Tabora-Ndono (km 42):

Mkataba ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Julai 2012. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 51.35 na Mkandarasi ni *CHICO*.

- (ii) Ndono-Urambo (km 52):

Mkataba ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Julai 2012. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 59.77 na Mkandarasi ni *China Civil Engineering*.

Mheshimiwa Spika, kazi za barabara ya Uvinza-Kidahwe (km 76.6) zilianza tarehe 24 Septemba 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 23 Juni 2013. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 78.24 na Mkandarasi ni *CHICO*.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa ujenzi wa Daraja la Malagarasi na barabara zake (km 48) ulisainiwa tarehe 22 Oktoba 2010 na Mkandarasi yupo kwenye maandalizi ya kuanza kazi. Kazi zitafanyika kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga (*design and build*). Usanifu umekamilika kwa asilimia 50. Kazi inategemewa kukamilika tarehe 21 Oktoba 2013. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 78.91 na Mkandarasi ni *Hanil Engineering* na Msimamizi ni *Cheil Engineering*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara ya Tunduru-Namtumbo (km 194) - ujenzi unagharamiwa na fedha za mkopo toka *ADB* na *JICA* na kazi zimegawanywa katika sehemu tatu. Mikataba ya ujenzi ilisainiwa tarehe 24 Desemba 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika mwezi Aprili 2013. Aidha ujenzi wa sehemu ya Namtumbo-Songea (km 70) unaendelea kwa fedha za *MCC*.

Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 62.88 na Mkandarasi ni Sogea Satom na Msimamizi ni Nicholas O'Dwyer.

Mheshimiwa Spika, ujenzi pia unaendelea kwa sehemu ya Peramiho-Mbinga (km 78) kwa fedha za MCC. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 79.81 na Mkandarasi ni SINOHYDRO na Msimamizi ni kampuni ya Nicholas O'Dwyer.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara ya Musoma-Mwanza/Mara Border (km 85.5) ambayo mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 inatarajiwa kukamilika tarehe 30 Desemba 2012. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 85.368 na Mkandarasi ni CHICO.

Mheshimiwa Spika, miradi ya usanifu inayoendelea ni Bunda-Kisorya-Nansio (km 93), Ipole-Koga-Mpanda (km 255), Makurunge-Saadani-Pangani-Tanga (km 178), Matai-Kasesya (km 65), Same-Himo (km 96), Makambako – Songea (km 295), Mtwara – Masasi (km 200), Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 140), Tabora-Mambali-Bukene-Itobo-Kahama (km 149), Lupilo-Malinyi-Kilosa kwa Mpepo-Londo-Kitanda (km 396), Ifakara-Mahenge (km 67), Kibondo-Mabamba (km 35), Kolandoto-Lalago-Mwanhuzi-Matala-Oldean Junction (km 328), Omugakorongo-Kigarama-Murongo (km 105), Mpemba-Isongole (Tanzania/Malawi) (km 49), Soni-Bumbuli-Dindira-Korogwe (km 74), Makofia-Mlandizi-Vikumburu (km 148), Kibaoni – Majimoto-Inyonga (km 162), Mpanda – Ugala-Kaliua-Ulyankulu-Kahama (km 428), Makongolosi-Rungwa-Mkiwa (km 412), Mtwara-Newala-Masasi (km 209), Handeni-Kiberashi-Kondoa-Singida (km 460), Kibaha-Mapinga (km 23), Geita-Bukoli-Kahama (km 107) na Mbande-Kongwa Junction-Mpwapwa (km 50).

Mheshimiwa Spika, katika awamu hii, barabara za Manyoni – Isuna (km 54), Rombo Mkuu – Tarakea (km 32), Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 32), Geita – Sengerema – Usagara (km 90), Chalenze – Kitumbi (km 125) na Mwandiga – Manyovu (km 60) ujenzi wake umekamilika.

Mheshimiwa Spika, miradi ya usanifu iliyokamilika katika awamu hii ni Rujewa-Madibira-Mafinga (km 152), Mayamaya-Bonga (km 198.2), Nata-Fort Ikoma (km 141), Chaya-Nyahua (km 90), Mangaka-Mtambaswala (km 65), Mto wa Mbu-Loliondo-Mugumu-Nata-Makutano (km 452), Mbinga – Mbamba Bay (km 66), Kamwanga-Sanya Juu (km 75), Uyovu-Bwanga-Biharamulo (km 112), Kisesa – Usagara (km 17), Sanya Juu-Bomang'ombe (km 25) na Katumba-Mbambo-Tukuyu (km 80).

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa ya ujenzi wa madaraja. Usanifu wa Daraja la Mto Kilombero umekamilika na ujenzi utanza mwaka 2011/2012. Aidha, kazi ya ujenzi wa Daraja la Mto Mwatisi inaendelea na kiasi cha shilingi milioni 870.0 kimekwisha tolewa. Gharama kulingana na mkataba wa kazi ni shilingi bilioni 1.39. Ujenzi wa Daraja la Malagarasi umeanza kwa ufadhili wa Serikali ya Korea na kwa Daraja la Kigamboni Serikali na NSSF wanaendelea na maandalizi ili kuanza ujenzi wa Daraja kwa njia ya *Public Private Partnership* katika mwaka wa fedha 2011/12.

Mheshimiwa Spika, usanifu umekamilika kwa daraja la Nangoo na Mkandarasi yuko kwenye maandalizi ya kuanza kazi ya ujenzi. Aidha, usanifu umekamilika kwa daraja la Sibiti na mchakato wa kumpata Mkandarasi wa ujenzi unaendelea. Kuhusu Daraja la Mbutu usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi. Kazi za ujenzi wa daraja la Ruhekei zinaendelea na zimefikia asilimia 50. Katika Daraja la Ruhuhu, mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu unaendelea kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Kujenga Barabara za Juu (*Fly Overs*) Kwenye Makutano ya Barabara Maeneo ya TAZARA na Ubungo.

Mheshimiwa Spika, Usanifu wa '*Flyover*' ya TAZARA umeanza Juni 2011 kwa ufadhili wa JICA. Kwa upande wa '*Flyover*' ya Ubungo Serikali imepeleka maombi kwa Serikali ya Japan kupitia JICA ili kusaidia ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kupanua mtandao wa barabara za Jiji la Dar es Salaam kwa Kujenga na Kukarabati Barabara zifuatazo:-

Barabara za *Ubungo Bus Terminal* – *Mabibo-Kigogo Roundabout* (km 6.4) kazi ya ujenzi inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 75. *Kigogo Roundabout-Bonde la Msimbazi* – *Twiga/Msimbazi Junction* (km 2.7) kazi ya ujenzi inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 42. *Tabata Dampo* – *Kigogo-Ubungo Maziwa External* (km 2.25), usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya *Old Bagamoyo-Garden Road* (km 9.1) mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usanifu unaendelea wakati barabara ya *Jet Corner-Vituka-Davis Corner* (km 10.3) kazi ya ujenzi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, usanifu tayari umekamilika, hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi kwa barabara za Mbezi (*Morogoro road*) –Maramba Mawili – Kinyerezi - Banana (km 14), Tegeta - Kibaoni-Wazo – Goba - Mbezi Mwisho (km 20) na Tangi Bovu-Goba (km 9).

Mheshimiwa Spika, kazi ya usanifu inaendelea na itakamilika katika mwaka 2010/11 kwa barabara za Kimara Baruti-Msewe-Changanyikeni (km 2.6) na Kimara-Kilungule-*External Mandela Road* (km 9).

Mheshimiwa Spika, kuanza mradi wa mabasi yaendayo kasi (*DART*) (km 20.9). Mradi wa mabasi yaendayo kasi (*DART*) una sehemu zifuatazo: -

- (i) Ujenzi wa barabara ya Kimara- Magomeni (km 10.4) na Magomeni – Kivukoni, Kawawa na Msimbazi (km 10.5):

Mchakato wa kumpata Mkandarasi unaendelea na mradi unafadhiliwa na Benki ya Dunia.
- (ii) Ujenzi wa Kituo cha Ubungo:

Mkandarasi amepatikana ila hajakabidhiwa eneo la mradi kwani huduma za biashara hazijahamishwa.
- (iii) Ujenzi wa '*Depot*' ya Jangwani:

Mkandarasi amepatikana na anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi.
- (iv) Ujenzi wa Kituo cha Kivukoni:

Mkandarasi amekabidhiwa eneo tarehe 4 Agosti 2010 na kazi imefikia asilimia 24.
- (v) Ujenzi wa Kituo cha Kariakoo:

Mkandarasi amepatikana lakini hajakabidhiwa eneo la mradi kwa sababu mgogoro wa eneo hili bado uko Mahakamani.
- (vi) Kujenga Vituo 6 (Shekilango, Urafiki, Magomeni, *Fire*, Kinondoni 'A' na Mwinjuma):

Mkandarasi amepatikana na amekabidhiwa maeneo ya mradi isipokuwa *Fire* kwa sababu eneo hilo bado lina mgogoro.
- (vii) Kuhamisha Miundombinu ya Umeme:

Kazi ya kuhamisha nguzo za umeme inaendelea na imefikia asilimia 35.

Mheshimiwa Spika, Vivuko na Magari. Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (*TEMESA*) katika mwaka 2010/11 ilitengewa shilingi 1,304,250,000 kwa ajili ya kuendelea na ununuzi wa vivuko vipya vya Rusumo, Msangamkuu na Ilagala. Ujenzi wa vivuko vya Rusumo na Msangamkuu unaendelea nchini Uholanzi na unatarajiwa kukamilika Agosti, 2011. Ununuzi wa kivuko cha Ilagala ulitangazwa upya baada ya kumkosa Mzabuni na kwa sasa zabuni imeshafunguliwa na hatua za ununuzi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maegesho ya vivuko, katika mwaka 2010/2011, mradi huu ulitengewa shilingi 751,943,600/= kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Ruhuhu, Rugezi-Kisorya, Musoma-Kinesi, Utete, Msangamkuu, Rusumo na Itungi Port. Katika mwaka 2010/2011, maegesho yaliyokamilika ni ya vivuko vya Musoma-Kinesi na Utete.

Mheshimiwa Spika, suala la ukarabati wa vivuko, katika mwaka 2010/2011, mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 471,964,600 kwa ajili ya ukarabati vivuko vya MV Alina (Dar es Salaam) na Pangani I (Tanga) ili vivuko hivyo viendeleo kutoa huduma ya uhakika na salama kwa watumiaji na mizigo yao. Mkandarasi wa kufanya kazi ya ukarabati wa Mv Alina amepatikana na maandalizi ya kutangaza zabuni ya ukarabati wa Mv Pangani I yamekamiliika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matengenezo ya magari ya Serikali, katika mwaka 2010/2011, Wakala ulitengeneza magari 3,360 ikilinganishwa na lengo la magari 6,905 sawa na asilimia 49, miradi ya umeme 32 kati ya miradi 51 iliyopangwa ambayo ni sawa na asilimia 63 na miradi 69 ya ushauri wa kihandisi ikilinganishwa na lengo la miradi 216 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kupitia Wakala wa Majengo ya Serikali (*TBA*) ilitengewa jumla ya shilingi 5,696,834,150/= kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Waheshimiwa Majaji nchini, kukamilisha ujenzi wa mifumo ya ulinzi, uboreshaji wa mazingira pamoja na uzio (*fence*) katika nyumba za viongozi na kukamilisha ujenzi wa nyumba za viongozi katika Wilaya mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, hadi Mei, 2011, Wakala ulikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa kazi ya ukarabati wa nyumba 82 za Viongozi jijini Dar es Salaam na ujenzi wa uzio kuzunguka nyumba za viongozi Msasani Penisullar. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na ukarabati wa majengo yaliyopo katika miji ya Dodoma (1), Mwanza (1), Lushoto (1), Tanga (1), Mafia (1), Musoma (2), Arusha (2), Lindi (3) na Bagamoyo (1). Wizara ya Ujenzi kwa kupitia Wakala wa Majengo imeendelea kujenga nyumba kwa ajili ya Viongozi mbalimbali katika mikoa ya Dar es Salaam (2), Iringa (1), Mbeya (1), Ruvuma (1), Tanga (1), Arusha (1), Dodoma 1, Tabora 1, Urambo (Tabora)1 na Mwanza 2, Bahi (Dodoma) 2, Ukerewe (Mwanza) 2 na Mvomero (Morogoro) 1.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, *TBA* ilikamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa Miradi mitano ambayo ni jengo la ghorofa 10 Mtaa wa Wachaga/Wasukuma (Arusha), jengo la ghorofa 6 Mtaa wa Moshi (Dodoma), Makao Makuu ya Wakala na jengo la ghorofa nane (8), (Dar es Salaam). Aidha, Wakala unaendelea na ujenzi wa miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na jengo la *Ex-NMC Mbezi Beach* (DSM), jengo la ofisi ya *TBA* (Manyara), Ujenzi wa Nyumba tatu za viongozi (Shinyanga) na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bariadi. Miradi mingine ni Ujenzi wa nyumba ya *RAS* na DC Ilala (DSM), Nyumba za Viongozi (Songea), Nyumba ya Viongozi Msasani (DSM) na Ujenzi wa Nyumba za Majaji katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Mwanza, Tabora na Tanga na Ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Spika, usalama barabarani na mazingira. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 jumla ya shilingi milioni 783.09 za ndani na shilingi milioni 575.00 za nje zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za usalama barabarani. Hadi Mei 2011, kiasi cha shilingi milioni 416 za ndani zilitolewa. Masuala yaliyotekelezwa ni pamoja na kutoa elimu kuhusu usalama barabarani, kuandaa mafunzo ya *Road Safety Audit* na kampeni za usalama barabarani (*Road Safety campaigns*). Masuala mengine ni ukaguzi na udhibiti wa uharibifu wa miundombinu ya barabara (*Axle Load Control*), kutoa elimu na miongozo mbalimbali ya kuboresha usalama barabarani ikiwa ni pamoja na *Highway code*, *Road Safety Audit manual*, *Road Signs Manual* na muongozo wa madereva wanafunzi. Aidha, Wizara ilifanya maandalizi ya kuanza utaratibu wa utoaji wa vibali

kwa njia ya teknolojia ya kisasa katika kudhibiti uzito (*Abnormal loads – e permit*). Kuanza maandalizi ya kutunga Sheria mpya ya Usalama barabarani badala ya Sheria Na. 30 ya mwaka 1973. Kuanza maandalizi ya ujenzi wa vituo vya ukaguzi na kupumzikia madereva na abiria katika maeneo ya mtandao wa barabara kuu nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazingira, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilisimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ikiwa ni pamoja na kupitia taarifa za Tathimini ya Athari kwa Mazingira (*TAM*) za miradi mbalimbali ya sekta iliyotekelezwa. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa Wahandisi na Mafundi Sanifu.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara. Katika mwaka 2010/2011, Wizara ilipanga kutekeleza kazi mbalimbali zikiwa ni pamoja na; kuendesha mafunzo ya ukandarasi kwa kampuni za wanawake 15, kuandaa miongozo ya ushiriki wa wanawake katika kazi za ujenzi wa barabara, kuhamasisha na kufuatilia maendeleo ya ushiriki wa Wanawake katika kazi za barabara. Hadi Juni, 2011, Wizara iliendesha semina ya mafunzo kwa Wanawake Makandarasi na wanaopenda kuanzisha kampuni za Kandarasi ya Nguvu Kazi (45) jinsi ya kutumia teknolojia ya Nguvu Kazi katika kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara. Mafunzo hayo yalifanyika Mkoani Morogoro na washiriki walitoka katika Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, ushiriki katika Jumuiya mbalimbali. Katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kuiwakilisha nchi katika masuala yanayohusu sekta ya ujenzi katika Jumuiya mbalimbali za kikanda. Jumuiya hizo ni pamoja na *EAC* na *SADC*. Wizara imeshiriki katika vikao mbalimbali vya nchi Wanachama wa *COMESA – EAC – SADC* kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo uanzishaji wa Eneo Huru la Biashara (*Free Trade Area – FTA*) katika nchi za *SADC, EAC* na *COMESA*. Ili kuimarisha biashara kwenye Soko Huru, pamoja na mambo mengine mkazo unawekwa kwenye kuimarisha miundombinu ya usafiri ikiwemo barabara.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake katika uendelezaji wa miundombinu ya barabara ili kuiunganisha nchi yetu na nchi wanachama wa *EAC*. Miongoni mwa miradi inayotekelezwa ni barabara ya Arusha – Namanga, Bagamoyo – Saadani - Tanga – Horohoro, Arusha – Himo – Holili/Taveta na Vituo vya pamoja vya mipakani (*One Stop Border Posts*).

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya watumishi. Katika mwaka 2010/2011, Wizara imeendelea kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma kwa kuwapeleka watumishi 35 katika mafunzo ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, watumishi 20 walipelekwa mafunzo ya muda mrefu na 10 mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Watumishi watano walipelekwa mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi. Aidha, watumishi watatu (3) walibadilishwa na kupandishwa vyeo, watumishi 50 walithibitishwa kazini, watumishi 34 walipandishwa vyeo na watumishi watatu (3) walijajiwa katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kupambana na UKIMWI. Katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na *TACAIDS* iliendelea kuhamasisha watumishi wake kupima afya zao ili kujiepusha na maambukizi ya UKIMWI pamoja na kutoa huduma ya lishe bora.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya rushwa. Katika kupambana na kupunguza vitendo vya rushwa, Wizara katika mwaka 2010/2011, iliendelea kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa kutoa elimu kwa watumishi wote kwa kupitia semina mbalimbali kuhusu athari za rushwa, makosa ya rushwa yanayoweza kutendeka na kuwahimiza kuepukana na vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara (*RFB*). Katika mwaka 2010/2011, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilipanga kukusanya shilingi bilioni 286.9 kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Hadi Mei, 2011 shilingi bilioni 269.38 zilikusanywa sawa na asilimia 93.89. Wizara kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara inaendelea kuandaa mapendekezo ya kupanua wigo wa vyanzo vya fedha za matengenezo ya barabara. Aidha, Bodi imeshirikiana na *EWURA* katika kuweka mikakati ya kudhibiti uchakachaji wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*ERB*). Katika mwaka 2010/2011, Bodi ya Usajili wa Wahandisi imeendelea kutekeleza jukumu lake kubwa la kuhakikisha kuwa, shughuli zote za Kihandisi zinafanywa na Wahandisi waliosajiliwa au na makampuni yaliyosajiliwa kwa kuzingatia viwango na maadili ya kihandisi. Hadi Juni 2011, Bodi iliweza kusajili Wahandisi 818 na Kampuni za ushauri 17 ikilinganishwa na malengo ya kusajili Wahandisi 725 na Kampuni za Ushauri 20. Jumla ya Wahandisi waliosajiliwa tangu Bodi ilipoanzishwa ni 10,281 na Kampuni za Ushauri 191. Aidha, Bodi imeendelea kusimamia utekelezaji wa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wote sambamba na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu. Aidha, Bodi pia ilikagua miradi ya ujenzi wa barabara na migodi yote mikubwa ili kuhakikisha kuwa wahandisi wote wa kigeni katika miradi hiyo wamesajiliwa na Bodi, na imeendelea kusimamia na kukagua shughuli za kihandisi pamoja na maendeleo ya wahandisi katika halmashauri katika mikoa yote Tanzania bara.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiraji Majenzi (*AQSRB*). Katika mwaka 2010/2011, Wabunifu Majengo 20 na Wakadiraji Majenzi 13 walisajiliwa. Aidha, makampuni 13 ya Wabunifu Majengo na makampuni nane (8) ya Wakadiraji Majenzi yalisajiliwa. Bodi pia ilivasajili wataalam wa fani hizi wenye sifa za kati nane (8), kwa kupitia mpango unaogharamiwa na Serikali wa mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wa taaluma katika fani hizi mbili. Bodi ilifanya ukaguzi wa majenzi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara, kwa lengo la kuhakikisha kwamba, shughuli zote zinazotekelezwa zinasimamiwa na kampuni za Wabunifu Majengo na Wakadiraji Majenzi waliosajiliwa. Katika zoezi hilo, jumla ya miradi ya majenzi 1,259 ilikaguliwa ikilinganishwa na miradi 999 katika mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Makandarasi (*CRB*). Katika mwaka 2010/2011, Bodi imeendelea kushirikiana na Serikali katika kuendeleza sekta ya ukandarasi wa kizalendo, ili iweze kuchangia katika kuongeza ajira na ujenzi bora wa miundombinu. Bodi ilisajili Makandarasi 860 ikilinganishwa na malengo ya Makandarasi 803. Aidha, Bodi ilikagua miradi ya ujenzi 2,111 ikilinganishwa na malengo ya miradi 1,980. Kati ya hiyo miradi 805 ilikuwa na upungufu na Makandarasi wahusika walichukuliwa hatua za kisheria. Katika kipindi hicho, Bodi iliendesha kozi za mafunzo ya Makandarasi, katika Mikoa ya Shinyanga, Rukwa, Dar es Salaam na Mtwara. Aidha, Bodi ilifanya maonyesho ya teknolojia, vifaa na huduma za ujenzi jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Ujenzi. Katika mwaka 2010/2011, Baraza la Taifa la Ujenzi limeendelea kushughulikia maendeleo ya Sekta ya Ujenzi nchini kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa msukumo wa utekelezaji wa Sera ya Ujenzi, ushauri wa kiufundi, utafiti, ukaguzi wa kiufundi, mafunzo pamoja na kushughulikia uanzaji kazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi. Aidha, Baraza limeendelea kuratibu utekelezaji wa majaribio ya mfumo wa kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya umma ujulikanao kwa jina la *Construction Sector Transparency Initiative (CoST)*.

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Ujenzi (*Corporation Sole Works*) kilianzishwa kwa Sheria Na. 23 ya Mwaka 1974 ili kufanya kazi za ujenzi pamoja na kubuni miradi ya kibiashara yenye mahusiano na kazi za ujenzi. Kikosi kimeteteleza miradi mingi kwa ufanisi hasa katika Ujenzi na Ukarabati wa Majengo. Katika mwaka 2010/11, Kikosi cha Ujenzi kimeteteleza miradi nane (8) inayohusu ukarabati wa Jengo la Boma la Kale Bagamoyo (phase II), ujenzi wa nyumba za Viongozi Dar es Salaam na Mwanza, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Nyamagana - Mwanza, ujenzi wa gati (*Ferry Ramps*) katika Kivuko cha Musoma- Kinesi na Ujenzi wa Ofisi za Kituo cha Hifadhi ya Bahari (MACEMP) - Tanga.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi (*Tanzania Transportation Technology Transfer Centre- TANTP*). Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Kituo kilisambaza kwa wadau makala na taarifa zinazoelezea teknolojia mbalimbali katika sekta ya Ujenzi na Uchukuzi. Aidha, kituo kilishirikiana na taasisi nyingine kuandaa na kuendesha Mafunzo ya Ukaguzi wa Usalama wa Barabara (*Road Safety Audit Course*) kwa wahandisi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ujenzi Morogoro kwa sasa kinatoa mafunzo kwa Mafundi Sanifu na Stadi wanaoshiriki kazi za ujenzi kwenye sekta zote za umma na binafsi. Mwaka

2010/2011, jumla ya wanafunzi 474 wa fani mbalimbali za ujenzi walipata mafunzo kama ifuatavyo: *Basic Technical Course* – 173, *Basic Driving Course* – 154 na *Technician Maintenance Management Courses* – 147.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Matumizi Stahili ya Nguvu Kazi (*ATTI-MBEYA*). Chuo cha *ATTI* kina jukumu la kuratibu kazi zote za miradi, kutoa ushauri, maelekezo na miongozo kwa wadau na watendaji wa kazi za barabara kuhusu matumizi bora ya teknolojia stahili ya nguvu kazi pamoja na mafunzo.

Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Chuo kiliendesha mafunzo kwa Mafundi Sanifu wa Halmashauri na Makandarasi, Viongozi wa Vikundi wa Vijiji, Mafunzo ya Uwekaji wa Tabaka la Lami kwenye barabara za vijijini na Mafunzo ya Teknolojia ya Nguvu kazi kwa Makandarasi Wanawake. Aidha, Chuo kilihitimisha mafunzo ya watumishi na kuendelea na matengenezo ya kawaida ya barabara za mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Chuo pia kilitekeleza miradi ya majaribio kwa Makandarasi Wanafunzi katika Halmashauri za Kongwa, Igunga, Nzega, Urambo, Sikonge, Chunya, Manyoni na Manispaa ya Tabora. Aidha, Chuo kilishiriki katika ujenzi wa barabara za mitaa (*community roads*) zenye jumla ya kilometa nne (4) katika Kitongoji cha Ipagika na Nsongwa vilivyoko kijiji cha Ilenge Wilayani Rungwe kwa kushirikiana na wananchi waliohamasika na kujitolea nguvu zao. Chuo kinaendelea na ukarabati wa barabara ya kilometa tano (5) kwa kushirikiana na wananchi wa kijiji cha Isebelo, Wilayani Rungwe.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida 2011/2012. Wizara ya Ujenzi inakadiria kukusanya jumla ya shilingi 36,583,000 katika mwaka 2011/2012 kutoka Idara za Utawala (shilingi 183,000), Huduma za Kiufundi (shilingi 30,000,000) na Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi (shilingi 6,400,000).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 245,440,294,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 221,588,980,000 ni fedha za Mfuko wa Barabara, shilingi 15,879,643,781 ni fedha za mishahara kwa Wizara na Taasisi na shilingi 7,974,670,219 ni fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012. Katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka 2011/2012, Wizara imezingatia vipaumbele vya Miradi inayoendelea kutekelezwa, Miradi inayofadhiliwa na wahisani na yenye kuhitaji mchango wa Serikali, Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na Utekelezaji wa Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2011/2012, maelezo ya kila mradi ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya *Wazo Hill* – Bagamoyo – Msata (Km 107) shilingi milioni 6,806.90. Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa km 43 kutoka Wazo Hill – Bagamoyo kwa kiwango cha lami ambapo ujenzi ulikamilika mwaka 2006. Awamu ya pili inahusisha ujenzi wa sehemu ya Bagamoyo – Msata (km 64) kwa kiwango cha lami. Mkataba wa Ujenzi unatekelezwa na kampuni ya *ESTIM Construction* na ulisainiwa tarehe 11 Agosti 2010 kwa gharama ya shilingi milioni 89,610. Kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami inaendelea na inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 24.

Mheshimiwa Spika katika mwaka 2011/2012, jumla ya Shilingi milioni 6,648.60 za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Msata (km 64) kwa kiwango cha lami. Kiasi cha shilingi milioni 158.53 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa barabara ya Bagamoyo – Sadani – Tanga (km 178).

Mheshimiwa Spika, barabara ya Usagara – Geita – Kyamyorwa (km 422) sehemu ya Uyovu – Biharamulo (km 112) - shilingi milioni 2,308.22. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kyamyorwa – Buzirayombo – Geita hadi Usagara yenye urefu wa kilometa 310.

Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa Barabara ya Kyamyorwa - Geita (km 220) ambayo ilikamilika Februari 2008. Awamu ya pili ilihusisha ujenzi wa barabara ya Geita - Usagara (km 90) ambapo ujenzi wake ulianza Februari 2008 na umekamilika mwezi Januari 2010. Awamu ya tatu itahusisha ujenzi wa barabara ya Uyovu - Biharamulo kupitia Bwanga (km 112). Jumla ya Shilingi milioni 2,308.22 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Uyovu - Biharamulo (km 112) katika mwaka wa fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua - Tabora (km 443) – shilingi milioni 80,980.97. Lengo la mradi huu ni kufanya usanifu na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kati ya Kigoma na Tabora (km 443) ikiwa ni pamoja na ujenzi wa daraja la Mto Malagarasi na barabara za maingilio ya daraja (km 48). Kazi ya ujenzi wa daraja ilianza tarehe 2 Desemba, 2010 na zinatarajiwa kukamilika Desemba 2013. Ujenzi wa barabara ya Kidahwe - Uvinza (km 76.6) ulianza tarehe 17 Desemba, 2010 na unatarajiwa kukamilika Oktoba 2013. Ujenzi wa barabara za Tabora-Ndono (km 42) na Ndono-Urambo (km 52) ulianza tarehe 3 Januari, 2011 na unatarajiwa kukamilika Februari 2013. Aidha, maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Tabora – Sikonge (km 70) yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya shilingi milioni 791.50 fedha za ndani zimepangwa kulipia sehemu ya deni la Mkandarasi wa barabara ya Kigoma – Kidahwe (km 35.7) ambayo ujenzi wake umekamilika kwa kiwango cha lami. Kiasi cha shilingi milioni 3,287.59 fedha za ndani na shilingi milioni 20,158.59 fedha za nje zimetengwa ili kuendelea na ujenzi wa lami barabara ya Kidahwe-Uvinza (km 76.6). Kiasi cha shilingi milioni 1,321.81 fedha za ndani na shilingi milioni 11,859.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa daraja la Malagarasi. Kiasi cha shilingi milioni 5,582.20 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tabora - Ndono (km 42) na shilingi milioni 6,156.35 kwa Ndono -Urambo (km 52). Kwa upande wa barabara ya Tabora – Sikonge (km 70) kiasi cha shilingi milioni 590.31 kimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Marangu – Tarakea – Kamwanga/Bomang’ombe – Sanya Juu (km 173) – shilingi milioni 28,187.69. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Marangu –Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 96) kwa kiwango cha lami ili kuchochea maendeleo ya sekta ya utalii kuzunguka mlima Kilimanjaro na hivyo kukuza uchumi wa nchi. Ujenzi wa sehemu ya Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 32) ulikamilika Septemba 2009 na ujenzi wa sehemu ya Tarakea – Rombo Mkuu (km 32) ulikamilika Januari 2011. Kazi za ujenzi wa sehemu ya Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika (km 32) zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika Oktoba 2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya Shilingi milioni 1,424.70 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipia sehemu ya madeni ya mkandarasi wa Tarakea – Rombo na shilingi milioni 1,519.68 kwa ajili ya kukamilisha kilometa 21.5 za lami zilizosalia kwa barabara ya Marangu – Rombo Mkuu na Mwika Kilacha (km 34). Aidha, kiasi cha shilingi 1,843.31 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Sanya Juu – Kamwanga (km 75).

Mheshimiwa Spika, Nangurukuru - Mbwemkulu (Km 95) – shilingi milioni 2,216.20. Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Mingoyo ambayo ni kiungo muhimu kati ya Dar es Salaam na mikoa ya kusini ambao ujenzi wake ulikamilika mwezi Januari 2008. Katika mwaka wa fedha 2011/12, jumla ya shilingi milioni 2,216.20 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya deni la Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Dodoma – Manyoni (Km 127) – shilingi milioni 31.66. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma - Manyoni (km 127) kwa utaratibu maalum wa kusanifu na kujenga (*Design & Build*). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na ulikamilika mwezi Novemba 2009. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya shilingi milioni 31.66 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya deni la Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Mbwemkulu – Mingoyo (Km 95) – shilingi milioni 1,583.00. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mbwemkuru - Mingoyo yenye urefu wa kilomita 95 kwa utaratibu wa *Design & Build*. Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Dar es salaam – Lindi – Mingoyo ambayo ni kiungo muhimu kati ya Dar es Salaam na Mikoa ya kusini na ujenzi

wake ulikamilika Desemba 2007. Katika bajeti ya mwaka 2011/2012, barabara hii imetengewa shilingi milioni 1,583.00 fedha za ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya deni la mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Manyoni – Singida (Manyoni – Isuna (Km 54) – shilingi milioni 474.900. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Manyoni - Isuna (km 54) kwa utaratibu wa *Design & Build*. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Ujenzi ulikamilika tarehe 7 Januari, 2011. Katika bajeti ya mwaka 2011/2012, barabara hii imetengewa shilingi milioni 474.90 fedha za ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya deni la mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Nelson Mandela (*Port Access*) (Km 16.8) – shilingi milioni 32,923.60. Malengo ya mradi huu ni kukarabati barabara hii ambayo ujenzi wake ulikamilika mwaka 1980. Kazi nyingine zitakazofanyika sambamba na uimarishaji wa barabara hii ni kuboresha mfumo wa mifereji pamoja na taa za barabarani na zile za kuongozea magari (*street lighting and traffic lights*). Aidha, mizani ya kupimia uzito wa magari itawekwa nje ya lango la kutokea bandarini ili kudhibiti uzito wa magari ya mizigo yanayotoka bandarini. Mradi huu unagharamiwa kwa msaada kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya pamoja na mchango wa Serikali ya Tanzania. Kazi ya ukarabati wa barabara hii ilianza Oktoba, 2007 na kukamilika tarehe 30 Juni, 2011. Mradi huo uko kwenye kipindi cha matazamia cha mwaka mmoja. Jumla ya Shilingi milioni 32,923.60 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi za ukarabati katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dumila – Kilosa (Km 78) – shilingi milioni 7,915. 00. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Dumila – Kilosa (km 78). Kazi ya ujenzi wa barabara ya Dumila - Rudewa (km 45) ilianza Februari 2010 na inatarajiwa kukamilika Machi 2013. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 7,915.00 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sumbawanga – Matai - Kasanga Port (Km 112) – shilingi milioni 9,498.00 lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Sumbawanga – Matai-Kasanga Port (km. 112) kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na unatekelezwa kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 8 Oktoba, 2009 na kazi ilianza Januari 2010. Mkandarasi anaendelea na uandaaji wa michoro pamoja na kupeleka mitambo eneo la kazi (*Mobilization*). Katika bajeti ya mwaka 2011/2012, kiasi cha Shilingi milioni 9,498.00 fedha za ndani kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Madaraja ya Nanganga, Sibiti, Kilombero, Maligisu, Kavuu, Mbutu, Ruhekei na Ununuzi wa *Mabey Emergency Bridge* – shilingi milioni 3,932.70. Lengo la mradi huu ni kujenga Daraja la Nanganga kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru, Daraja la Sibiti kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti, Daraja la Kilombero kwenye barabara ya Mikumi - Ifakara – Mahenge, daraja la Maligisu (Mwanza) kwenye barabara ya Bukwimba – Kadashi - Maligisu, daraja la Kavuu barabara ya Majimoto-Inyonga, daraja la Mbutu barabara ya Igunga-Manonga, daraja la Ruhekei katika barabara ya Mbinga-Mbamba Bay na ununuzi wa *Mabey Compact Emergency Bridges*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, kiasi cha shilingi milioni 330.21 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Nanganga, Daraja la Sibiti shilingi milioni 1,107.79, Daraja la Maligisu shilingi milioni 732.20, Daraja la Kilombero shilingi milioni 1,054.13, Daraja la Kavuu shilingi milioni 252.99, Daraja la Mbutu shilingi milioni 252.99, Daraja la Ruhekei shilingi milioni 71.68. Aidha, shilingi milioni 80.11 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa *Mabey Compact Emergency Bridges* na shilingi milioni 50.60 kwa ajili ya usanifu wa daraja la Ruhuhu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya New Bagamoyo (Kawawa *JCT* - Tegeta Km 17) – shilingi milioni 88,619.20. Lengo la mradi huu ni kupanua barabara hii kutoka njia mbili za sasa hadi njia nne kuanzia makutano ya Moroco hadi na Ali Hassan Mwinyi hadi Tegeta ili kupunguza msongamano wa magari katika barabara hii. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Japani kupitia Shirika la Maendeleo la *JICA*. Jumla ya shilingi milioni 216.20 fedha za ndani na shilingi milioni 88,403.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi, kulipa fidia na kuhamisha

huduma za jamii kwenye eneo la ujenzi (mabomba ya maji, nguzo na nyaya za umeme/simu n.k) katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kyaka –Bugene – Kasulo (Km 179.1) – shilingi milioni 5,140.94. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (Kyaka-Bugene) yenye urefu wa kilometa 59.1 kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali kwa asilimia mia. Kazi za ujenzi zilianza tarehe 15 Desemba, 2010 na zinatarajiwa kukamilika machi 2013. Jumla ya shilingi milioni 5,140.94 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Isaka – Lusahunga (Km 242) - shilingi milioni 28,746.20. Lengo la mradi huu ni kufanya ukarabati wa barabara hii yenye urefu wa kilometa 242 kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili (2) ili kuharakisha utekelezaji: Isaka – Ushirombo (km 132) na Ushirombo – Lusahunga (km 110): Mikataba ya ujenzi wa sehemu hizi ilisainiwa tarehe 8/08/2009 na kazi ya ukarabati ilianza rasmi Novemba 2009 na inatarajiwa kukamilika Mei 2013. Katika mwaka 2011/2012, barabara hii imetengewa fedha za ndani shilingi milioni 15,192.98 kwa sehemu ya Isaka – Ushirombo na shilingi milioni 13,553.22 kwa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga kwa ajili ya kuendelea na ukarabati.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (Km 254) – shilingi milioni 14,415.64. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Manyoni - Itigi – Tabora kwa kuanzia na sehemu ya Manyoni – Chaya yenye urefu wa kilometa 89.35 na sehemu ya Tabora –Nyahua yenye urefu wa kilometa 85 kwa kutumia fedha za ndani. Mikataba ya ujenzi ilisainiwa tarehe 30 Julai 2010 na kazi za ujenzi zinatarajiwa kukamilika tarehe 29 Julai 2013 kwa sehemu zote mbili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya Shilingi milioni 7,000.64 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Tabora – Nyahua na shilingi milioni 7,415.00 kwa sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Korogwe – Handeni (Km 65) – shilingi milioni 6,465.20. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Korogwe – Handeni (km 65). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi ya ujenzi ilianza tarehe 19 Julai 2009 na inatarajiwa kukamilika katika tarehe 14 Mei 2012. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 6,465.20 kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi katika bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara za Mikoa shilingi 27,442.33 milioni. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kufanya ukarabati wa jumla ya kilometa 492.0 kwa kiwango cha changarawe na kujenga kilometa 15.6 kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo. Kazi za ukarabati kwa kiwango cha changarawe zitafanyika katika Mikoa yote. Aidha, ujenzi wa madaraja 14 utatumia fedha za Bajeti ya Maendeleo katika Mikoa ya Katavi (1), Morogoro (1), Mbeya (3), Manyara (1), Mtwara (1), Ruvuma (3), Simiyu (3), Lindi (1).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, miradi ya maendeleo ya barabara za Mikoa imetengewa jumla ya shilingi milioni 27,442.33 kutoka fedha za Bajeti ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 12,062.33 ni za Ndani na shilingi milioni 15,380.00 ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Handeni – Mkata (Km 54) – shilingi milioni 6,032.00. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Handeni – Mkata yenye urefu wa kilometa 54. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi za ujenzi zilianza tarehe 28 Desemba, 2010 na zinatarajiwa kukamilika Desemba, 2012. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 6,032.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara katika bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwandiga – Manyovu (Km 60) – shilingi milioni 949.80. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya kutoka Mwandiga hadi Manyovu inayounganisha Mkoa wa Kigoma na nchi jirani ya Burundi kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Ujenzi wa barabara hii umekamilika Oktoba, 2010. Barabara hii imetengewa

shilingi milioni 949.80 kwa ajili ya kulipia sehemu ya deni la mkandarasi katika bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kuondoa msongamano barabara za Dar es Salaam – shilingi milioni 5,020.55. Lengo la mradi huu ni kujenga, kufanya upanuzi, na kukarabati barabara za Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari. Ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano wa magari ulianza katika mwaka wa fedha 2009/10. Barabara hizo ni Ubungo Bus Terminal – Kigogo-Kawawa Roundabout (km 6.4), Kawawa Roundabout-Msimbazi Valley – Jangwani/Twiga JCT (km 2.7), *Jet Corner* – Vituka-Devis (km 10.3) na ujenzi wa mfereji wa Bungoni unaoanzia barabara ya Nyerere hadi Uhuru (Bungoni).

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2011/2012, kiasi cha shilingi milioni 633.20 kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizobakia kwa barabara ya *Ubungo Bus Terminal* – *Kigogo-Kawawa Roundabout*, shilingi milioni 633.20 kwa barabara ya *Kawawa Roundabout-Msimbazi Valley* – Jangwani/Twiga *JCT* na shilingi milioni 1,266.40 kwa barabara ya *Jet Corner* – *Vituka-Devis Corner*.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi milioni 337.32 kimetengwa kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha changarawe kwa barabara ya Ubungo Maziwa – *External* na Tabata Dampo – Kigogo, shilingi milioni 843.31 kwa barabara ya Kimara – Kilungule – *External*, shilingi milioni 337.32 kwa barabara ya Mbezi Malambamawili – Kinyerezi – Banana, shilingi milioni 337.32 kwa barabara ya Tegeta Kibaoni – *Wazo Hill* – Goba – Mbezi/Morogoro road, shilingi milioni 295.16 kwa barabara ya Tanki Bovu – Goba na shilingi milioni 337.32 kwa barabara ya Kimara – Baruti – Msewe – Changanyikeni.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ndundu – Somanga (Km 60) - Shilingi Milioni 6,157.80. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara sehemu ya Ndundu hadi Somanga yenye urefu wa kilometa 60 kwa kiwango cha lami. Mradi unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kukamilika Novemba 2011. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 6,157.80 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kidatu – Ifakara (Km 30) - shilingi milioni 210.83. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Kidatu hadi Ifakara kwa kiwango cha lami nyepesi yaani *Otta Seal* chini wa msaada wa Serikali ya Uswizi na mchango wa Serikali ya Tanzania. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 210.83 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilometa 1 ya lami katika bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tabora - Ipole - Koga – Mpanda (Km 359) - shilingi milioni 633.20. Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Mkataba wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulisainiwa tarehe 8 Juni, 2009 na kazi zinatarajiwa kukamilika Agosti, 2011. Jumla ya Shilingi milioni 633.20 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili kukamilisha kazi ya usanifu katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Makutano - Natta – Mugumu - Loliondo – Mto wa Mbu (Km 328) – shilingi milioni 1,634.81. Lengo la mradi huu ni kufanya usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Mikataba kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina kwa sehemu ya Natta-Mugumu - Loliondo (km 115) na Mto wa Mbu – Loliondo (km 213) ilisainiwa tarehe 26 Agosti, 2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya Shilingi milioni 791.50 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu na shilingi milioni 843.31 kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi wa lami kwa sehemu ya Makutano – Nata (km 50).

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ibanda – Itungi Port (Km 4) – shilingi milioni 609.00. Lengo la mradi huu ni kufanya ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu umetengewa Shilingi milioni 609.00 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ukarabati katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tanga - Horohoro (Km 65) – shilingi milioni 98.15. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Tanga - Horohoro (km 65) kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Mfuko wa MCC na mchango wa Serikali ya Tanzania. Kazi ya ujenzi ilianza tarehe 22 Januari 2010 na kazi inatarajiwa kukamilika Aprili, 2012. Katika mwaka wa fedha 2011/12, kiasi cha shilingi milioni 98.15 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nzega – Tabora (Km 115) – shilingi milioni 10,174.78. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Nzega – Tabora (km 115) kwa kiwango cha lami. Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo. Nzega-Puge (km 58.8) na Puge-Tabora (km 56.10). Kazi zilianza Februari 2011 na zinatarajiwa kukamilika Machi 2013. Kiasi cha shilingi milioni 5,065.60 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Nzega – Puge na shilingi milioni 5,109.18 kwa sehemu ya Puge – Tabora katika mwaka wa fedha 2011/12.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sumbawanga Mpanda Nyakanazi (KM 829)- Shilingi milioni 16,980.43. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Kanyani (km 497) kwa kiwango cha lami. Kazi ya ujenzi kwa sehemu ya Sumbawanga-Kanazi (km 75) na Kanazi-Kizi-Kibaoni (km 75.6) zilianza Desemba 2009 na zinatarajiwa kukamilika Desemba 2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya Shilingi milioni 7,415.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi kwa sehemu ya Sumbawanga-Kanazi na shilingi milioni 7,415.00 kwa sehemu ya Kanazi-Kizi-Kibaoni. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 1,264.96 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya barabara ya Kizi-Sitalike-Mpanda na shilingi milioni 885.47 kwa sehemu ya Mpanda-Mishamo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyanguge-Musoma (KM.85.5) na Mchepuo wa Usagara – Kisesa km 17 shilingi 6,669.33; lengo la mradi huu ni kuikarabati barabara ya Nyanguge-Musoma (km 183) na kujenga kwa kiwango cha lami kilometa 17 za mchepuo wa Usagara - Kisesa. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Mwanza/Mara Border – Musoma (km 85.5) ulisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 na kazi za ukarabati zinatarajiwa kukamilika Desemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, mradi huu umetengewa shilingi milioni 6,669.33 kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ukarabati. Kiasi cha shilingi milioni 337.33 kimetengwa kwa sehemu ya barabara ya Kisesa – Usagara *Bypass* kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Magole-Mhiza (Magole-Turiani (KM.48.8) - Shilingi 4,339.96). Lengo la mradi huu ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Kazi zilianza tarehe 3 Machi, 2010 na zinatarajiwa kukamilika Juni, 2012. Kiasi cha shilingi milioni 4,339.96 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwigumbi-Maswa-Bariadi-Lamadi (KM 171) (Bariadi – Lamadi - KM71.8) – shilingi milioni 5,635.20. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Shinyanga-Mwigumbi-Maswa-Bariadi-Lamadi yenye jumla ya kilometa 171 kwa kiwango cha lami. Kazi zilianza tarehe 8 Julai, 2010 kwa sehemu ya Bariadi – Lamadi na zinatarajiwa kukamilika Januari, 2013. Kiasi cha shilingi milioni 5,635.20 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ipole-Rungwa (KM 95-shilingi milioni 269.11). Lengo la mradi huu ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Mwaka 2011/2012 mradi huu umetengewa Shilingi milioni 269.11 kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakunifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kidahwe- Kasulu-Kibondo-Nyakanazi (KM 300) - Shilingi milioni 2,108.27. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Mwaka wa fedha 2011/2012, kiasi cha shilingi milioni 2,108.27 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara za Mafia (*Mafia Access Road*) (KM 14) - Shilingi milioni 1,899.60. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa na Shirika la Misaada la Marekani (*MCC*) ambao wametoa fedha za ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mafia kwa makubaliano ya Serikali kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Kiasi cha shilingi milioni 1,899.60 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, *Dodoma University Road* (KM 12) -Shilingi 421.65. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kiasi cha shilingi milioni 421.65 kimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya kuanza kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Daraja la Kigamboni - Shilingi Milioni 316.60. Hili ni moja ya daraja linalojengwa kwa njia ya *PPP*, fedha zingine zinatolewa na *NSSF*. Lengo la mradi huu ni kujenga Daraja litakalounganisha Jiji la Dar es Salaam na mji wa Kigamboni. Kiasi cha shilingi milioni 316.60 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi katika mwaka wa fedha 2011/12. Mradi utajengwa kwa ushirikiano na *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tunduma - Sumbawanga (KM 231) - Shilingi 949.80. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Tunduma – Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 231 kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Mfuko wa *MCC* na mchango wa Serikali ya Tanzania. Utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni:-Tunduma – Ikana (km 64); Ikana – Laela (km 64) na Laela – Sumbawanga (km 96.5). Kazi za ujenzi wa sehemu ya Laela – Sumbawanga zinatarajiwa kukamilika Novemba 2012, sehemu ya Tunduma – Ikana na Ikana-Laela zinatarajiwa kukamilika Septemba 2012. Kazi zinaendelea kwa sehemu zote tatu.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012, kiasi cha shilingi milioni 316.60 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi kwa sehemu ya Tunduma – Ikana, shilingi milioni 316.60 kwa sehemu ya Ikana-Laela na shilingi 316.60 kwa sehemu ya Laela – Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kagoma-Lusahunga (KM 154)- Shilingi Milioni 14,853.14. Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Mutukula – Bukoba – Biharamulo – Lusahunga yenye urefu wa kilometa 294 iliyofanyiwa usanifu mwaka 1996 chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Ujenzi wa sehemu ya barabara ya Mutukula – Muhutwe – Kagoma ulikamilika chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na Mfuko wa *OPEC*. Awali Benki ya Maendeleo ya Afrika ilitoa mkopo wa ujenzi wa sehemu ya Kagoma – Lusahunga (km 154) kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mkandarasi *China State Construction Engineering Corporation Ltd (CSCEC)* wa China kushindwa kutekeleza mkataba wa awali na kuondolewa, mkataba mpya wa kumaliza ujenzi wa barabara ya Kagoma – Lusahunga yenye urefu wa kilometa 154 kwa kiwango cha lami ulisainiwa tarehe 18 Juni 2009 na unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi za ujenzi zilianza Septemba 2009 na zimepangwa kukamilika Julai 2012. Barabara hii imetengwa shilingi milioni 14,853.14 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Arusha –Namanga (KM 105) - Shilingi milioni 52,074.42. Mradi wa Arusha – Namanga (km 105) – Athi River, ni sehemu ya miradi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki unaojumuisha nchi za Tanzania na Kenya ambao unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na Benki ya Maendeleo ya Japan (*JBIC*) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania na Kenya. Lengo la mradi ni kukarabati barabara hii kwa kiwango cha lami. Jumla ya Shilingi milioni 3,799.20 fedha za ndani na shilingi milioni 48,275.22 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ukarabati katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Singida –Babati –Minjingu-Arusha (KM321) ambazo Wakandarasi wapo pale, Shilingi milioni 108,026.44. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Singida - Babati -Minjingu yenye urefu wa kilomita 223 na kukarabati kwa kiwango cha lami sehemu ya Minjingu-Arusha yenye urefu wa kilometa 98.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Singida - Babati - Minjingu umegawanywa katika sehemu tatu za Singida – Katesh (km 65.1) , Katesh – Dareda (km 73.8) na Dareda – Babati – Minjingu (km 84.6). Kazi za ujenzi zilianza Machi 2009 na zinategemewa kukamilika mwezi Machi 2012. Miradi hii inagharamiwa na *ADB, JICA* na Serikali ya Tanzania. Mkataba wa ukarabati wa sehemu ya Minjingu-Arusha umesainiwa tarehe 12 Mei 2011 na kazi inatarajiwa kukamilika Mei 2014. Sehemu hii inakarabatiwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2011/2012 kiasi cha shilingi milioni 5,635.48 fedha za ndani na shilingi milioni 19,220.00 fedha za nje zimetengwa kwa sehemu ya Singida – Katesh, shilingi milioni 7,123.50 fedha za ndani na shilingi milioni 19,600.00 fedha za nje kwa ajili ya sehemu ya Katesh – Dareda na shilingi milioni 5,572.16 fedha za ndani na shilingi milioni 22,400.00 fedha za nje kwa ajili ya sehemu ya Dareda – Babati – Minjingu kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa sehemu zote tatu. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 158.30 fedha za ndani na shilingi milioni 28,317.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara ya Minjingu hadi Arusha.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dar es Salaam - Mbagala (Kilwa Road KM 12.9) - shilingi milioni 538.22. Lengo la mradi huu ni ukarabati na kupanua barabara ya lami kutoka njia mbili hadi nne kati ya Gerezani na Mbagala chini ya msaada kutoka Serikali ya Japan na Serikali ya Tanzania. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu nne ambapo awamu ya kwanza inahusisha sehemu ya Bendera Tatu-Mtoni kwa Azizi Ally (km 5), awamu ya pili inahusisha sehemu ya Mtoni kwa Azizi Ally-Mbagala Zakhem (km 5.1), awamu ya tatu inahusisha sehemu ya Mbagala Zakhem-Mbagala Rangi Tatu (km 1.5) na awamu ya nne inahusisha upanuzi wa sehemu ya Bendera Tatu-Gerezani (km 1.5). Awamu ya kwanza na ya pili imejengwa kwa msaada wa fedha kutoka Serikali ya Japan. Mkataba wa awamu ya tatu km 1.5 ulisainiwa tarehe 19 Oktoba, 2010 na kazi zinatarajiwa kukamilika Desemba, 2011. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, mradi huu umetengewa shilingi milioni 474.90 kwa ajili kukamilisha ujenzi wa kilometa 1.5 kwa sehemu ya Mbagala Zhakhem-Mbagala Rangi Tatu. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 63.32 kimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Bendera Tatu - Gerezani.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Msimba-Ruaha-Ikokoto –Mafinga Km(219) - shilingi milioni 71,693.123. Lengo la mradi huu ni kufanya ukarabati wa barabara ya lami ya Dar es Salaam – Tunduma (*TANZAM*). Mradi huu unahusisha ukarabati wa sehemu ya Iyovi - Kitonga Gorge (km 86.3), Ikokoto - Iringa (km 60.9), barabara ya mchepuo kuingia Iringa mjini (km 2.1) na Iringa-Mafinga (km 68.9). Mradi huu unagharamiwa kwa mkopo kutoka Serikali ya Denmark pamoja na mchango wa Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 jumla ya shilingi milioni 633.20 fedha za ndani na Shilingi milioni 70,405.283 za kigeni zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha km 36.6 zilizobaki za Iyovi hadi Iringa na kuendelea na ukarabati wa kilometa 68.9 za Iringa - Mafinga. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 654.64 kimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152).

Mheshimiwa Spika, barabara ya Korogwe - Mkumbara –Same (km 172) - Shilingi 36,316.60; ambayo ni sehemu ya barabara ya Segera – Moshi – Arusha, ilijengwa kwa kiwango cha lami katika miaka ya sabini imechakaa na kuhitaji kufanyiwa ukarabati. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia na jumla ya shilingi milioni 316.60 fedha za ndani na shilingi milioni 36,000.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ukarabati katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbeya-Makongolosi (KM 115) - shilingi milioni 5,065.60. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Mbeya hadi Makongolosi (km 115) kupitia Chunya kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Mbeya – Lwanjilo (km 36); Lwanjilo-Chunya (km 36) na Chunya-Makongolosi (km 43). Ujenzi wa sehemu ya Mbeya – Lwanjilo (km 36) ulianza mwezi Septemba 2007 na ulitegemewa kukamilika Machi 2010. Hata hivyo, mkataba wa ujenzi ulisitishwa Aprili 2009, baada ya Mkandarasi kushindwa kutimiza matakwa ya mkataba. Mkataba na Mkandarasi mwingine ulisainiwa Desemba 2010. Kazi

kwa sehemu ya Lwanjilo - Chunya (km 36) zilianza tarehe 5 Agosti 2009 na zinatarajiwa kukamilika Agosti 2013. Barabara hii imetengewa kiasi cha shilingi milioni 2,532.80 kwa kila sehemu kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Chalinze-Segera-Tanga (KM 245) - Shilingi milioni 65,635.18. Lengo la mradi huu ni kuifanyia ukarabati na upanuzi barabara ya Chalinze - Segera hadi Tanga. Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni: Chalinze-Kitumbi (km 125) na Kitumbi-Segera-Tanga (km 120). Ujenzi wa sehemu ya Chalinze-Kitumbi ulianza Aprili 2008 na ulikamilika Oktoba 2010. Mkataba wa sehemu ya Kitumbi-Segera-Tanga ulisainiwa tarehe 24 Desemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2011/12, jumla ya Shilingi milioni 1,635.18 fedha za ndani na shilingi milioni 64,000.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Kitumbi-Segera-Tanga.

Mheshimiwa Spika, Daraja la Ruvu. Lengo la mradi huu ni kujenga daraja jipya katika Mto Ruvu katika barabara ya Dar es Salaam – Tunduma (*TANZAM*). Mradi huu ulikamilika mwaka 2009. Jumla ya Shilingi milioni 253.28 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya deni la mkandarasi katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma-Iringa - (km 260)-Shilingi milioni 42,453.03. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma – Mtera – Iringa (km 260). Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na Shirika la Misaada la Japan (*JICA*). Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Iringa-Migori (km 95.1), Migori-Fufu Escapment (km 93.8) na Fufu *Escapment*-Dodoma (km 70.9). Mikataba ya ujenzi wa barabara hii ilisainiwa tarehe 13 Januari 2011.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2011/2012, kiasi cha shilingi milioni 1,222.39 fedha za ndani na shilingi milioni 13,850.00 fedha za nje zimetengwa kwa sehemu ya Iringa - Migori, shilingi milioni 1,083.41 fedha za ndani na shilingi milioni 12,274.00 fedha za nje kwa ajili ya sehemu ya Migori – Fufu *Escapment* na shilingi milioni 1,137.23 fedha za ndani na shilingi milioni 12,886.00 fedha za nje kwa ajili ya sehemu ya Fufu *Escapment* – Dodoma kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wakandarasi wote wapo kwenye *site*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma ya Babati - (km 261) - Shilingi milioni 10,226.41. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati yenye urefu wa kilomita 261. Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Dodoma-Mayamaya (km 43), Mayamaya-Bonga (km199) na Bonga-Babati (km 19).

Mheshimiwa Spika, mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Dodoma-Mayamaya ulisainiwa Juni 2010 na unatarajiwa kukamilika katika muda wa miezi 27. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Bonga – Babati (km 19.2) ulisainiwa Mei 2010 na unatarajiwa kukamilika katika muda wa miezi 12. Ujenzi wa sehemu hizi mbili unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Aidha, sehemu ya Mayamaya-Bonga inatarajiwa kujengwa kwa fedha za mkopo wa *ADB* na *JICA* ambao wameonesha nia ya kusaidia.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012, kiasi cha shilingi milioni 4,432.40 zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Dodoma – Mayamaya na shilingi milioni 2,434.01 kwa sehemu ya Bonga – Babati kwa ajili ya kuendelea na ujenzi. Aidha, shilingi milioni 3,360.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mayamaya - Bonga.

Mheshimiwa Spika, katika barabara ya Masasi-Songea-Mbamba Bay - (KM 649) - Shilingi milioni 41,844.67. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Masasi-Songea – Mbamba Bay yenye jumla ya kilometa 649. Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu zifuatazo:- Masasi – Mangaka (km 54), Mangaka – Tunduru (km 146), Namtumbo - Kilimasera (km 60.7); Kilimasera-Matemanga (km 68.2), Matemanga –Tunduru (km 58.7), Songea - Namtumbo (km 67), Peramiho – Mbinga (km 78) na Mbinga - Mbamba Bay (km 66) na sehemu nyingi makandarasi wapo kwenye *site*.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi huu kwa barabara ya Masasi-Mangaka umekamilika isipokuwa mifereji ya maji ya mvua. Sehemu hii inagharamiwa na Serikali za Japan na Tanzania. Kwa barabara ya Mangaka-Tunduru, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeanza Januari 2011 na inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi nane (8). Aidha, kwa barabara ya Tunduru-Matemanga-Songea, Mikataba ya Namtumbo-Kilimasera (km 60.7); Kilimasera-Matemanga (km 68.2) na Matemanga –Tunduru (km 58.7) ulisainiwa tarehe 24 Desemba 2010 na utekelezaji wake ni miezi 29 chini ya ufadhili wa *ADB* na *JICA*. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Songea – Namtumbo (km 67), ulisainiwa tarehe 25 Mei 2010 na muda wa utekelezaji ni miezi 27 chini ya ufadhili wa *MCC*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Peramiho-Mbinga-Mbambabay, ujenzi wa sehemu ya Peramiho Jct – Mbinga - (km 78), unagharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa *MCC* na mchango wa Serikali ya Tanzania. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Peramiho Jct – Mbinga ulisainiwa tarehe 2 Julai, 2010 na muda wa utekelezaji ni miezi 27.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012, zimetengwa jumla ya Shilingi milioni 316.60 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua sehemu ya Masasi-Mangaka, Shilingi milioni 1,112.53 fedha za ndani na shilingi milioni 12,607.00 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tunduru-Matemanga, shilingi milioni 989.06 fedha za ndani na shilingi milioni 11,208.00 fedha za nje kwa ajili kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Matemanga-Kilimasera, shilingi milioni 908.01 fedha za ndani na shilingi 10,286.00 fedha za nje kwa ajili ya sehemu ya Kilimasera – Namtumbo, shilingi milioni 79.15 fedha za ndani kwa ajili ya Songea - Namtumbo, na shilingi milioni 79.15 fedha za ndani kwa ajili ya Peramiho – Mbinga.

Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 42.17 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kumalizia usanifu kwa sehemu ya Mangaka - Tunduru, shilingi milioni 126.50 kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mbinga – Mbamba Bay, shilingi milioni 126.5 kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha changarawe kwa sehemu ya Mangaka – Mtambaswala. Kiasi cha shilingi milioni 9.50 fedha za ndani na shilingi milioni 2,220.00 fedha za nje kwa sehemu ya Makambako – Songea na shilingi milioni 9.50 fedha za ndani na shilingi milioni 1,725.00 fedha za nje kwa sehemu ya Mtwara – Mingoyo – Masasi kwa ajili ya usanifu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara - Shilingi milioni 20.00. Lengo la mradi huu ni kujenga Makao Makuu ya Wakala wa Barabara. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za ndani. Usanifu wa jengo hili umekamilika. Kiasi cha shilingi milioni 20.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya matayarisho ya kuanza kazi ya ujenzi katika mwaka wa fedha 2011/12.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Maegesho ya Vivuko (Shilingi 1,722,304,000). Mradi huu una lengo la kujenga maegesho (*landing ramps*) ili vivuko viweze kuegeshwa na kuwezesha abiria na magari kupanda na kushuka kwenye kivuko kwa urahisi nyakati zote za mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 mradi huu umetengewa shilingi 1,722,304,000 kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya vivuko mbalimbali nchini vikiwamo Chato, Rusumo, Msangamkuu, Utete, Rugezi-Kisorya, Kilambo, Ukara, Ruhuhu na Kilombero.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa Vivuko Vipya (Shilingi 1,271,149,000). Katika mwaka wa fedha 2011/12 mradi huu umetengewa shilingi 1,271,149,000 kwa ajili ya kuendelea na ununuzi wa kivuko kipya cha Ilagala (Kigoma) na kuanza hatua za ununuzi wa kivuko kipya cha Maisome-Kaunda (Geita).

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Vivuko (Shilingi 799,415,000). Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, mradi huu umetengewa jumla ya shilingi 799,415,000. Fedha hizi zitatumika kukifanyia ukarabati kivuko cha MV Alina (Dar es Salaam), kivuko cha Pangani I (Tanga), kivuko cha MV Geita (Mwanza) na kivuko cha Chato (Biharamulo) ili vivuko hivi viendelee kutoa huduma ya uhakika na salama kwa watumiaji na mizigo yao.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali (Shilingi 5,262,525,200). Lengo la mradi huu ni kujenga nyumba kwa ajili ya makazi ya Viongozi na watumishi wa Serikali wenye stahili hiyo. Kipaumbele kwa sasa ni katika ujenzi wa nyumba za Majaji pamoja na viongozi wengine wa Serikali wenye stahili ya kupewa nyumba na Serikali. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi itaanza maandalizi ya ujenzi wa nyumba 10,000 kwa ajili ya watumishi wa Serikali katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nyumba za viongozi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya shilingi 1,899,600,000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na umaliziaji wa nyumba za Waheshimiwa Majaji. Nyumba hizi ziko katika maeneo mbalimbali Jijini Dar es Salaam (2), Tabora (1), Mwanza (1), Iringa (1), Arusha (1), Mbeya (1), Ruvuma (1), Tanga (1), Dodoma (1), Kilimanjaro (1), Kagera (1), Mtwara (1), Shinyanga (1) pamoja na ghorofa moja iliyopo Mtaa wa Ngano jijini Dar es Salaam yenye jumla ya makazi sita (6) ya Viongozi.

Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi 918,140,000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mifumo ya ulinzi, uboreshaji wa mazingira pamoja na uzio (*fence*) katika nyumba za viongozi zilizojengwa Mikocheni, Kijitonyama na Msasani Peninsular jijini Dar es salaam. Aidha, jumla ya shilingi 949,800,000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba za Viongozi wa Serikali (*OCD, DSO, DAS na DMO*) katika Wilaya sita (6) za Tanzania Bara, Bahi (2), Mvimeru (1), Ukerewe (2), Kasulu (1), Urambo (1) na Kondoa (1). Wizara kupitia Kikosi cha Ujenzi imeendelea na ukarabati/uhifadhi wa jengo la Boma la kale Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Karakana za Serikali. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya shilingi 474,900,000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Karakana za Serikali chini ya Wakala wa Ufundi na Umeme.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Ofisi na Karakana za Kikosi cha Ujenzi. Mradi huu una lengo la kukarabati Ofisi na Karakana za Useremala zilizoko Dar es Salaam (Makao Makuu), Dodoma, Arusha na Mwanza zinazomilikiwa na Kikosi cha Ujenzi (*Works Corporation Sole*). Katika mwaka wa fedha 2011/2012 mradi huu umetengewa jumla ya shilingi 63,320,000 fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, usalama barabarani - Tshs. 1,435.00 Milioni. Mradi huu una lengo la kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, kiasi cha shilingi milioni 1,435.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mizani za kisasa, kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa vituo vya kutahini madereva kabla ya kupatiwa leseni na kuandaa michoro ya vituo vya kupumzikia madereva na abiria baada ya kusafiri kwa umbali mrefu. Shughuli nyingine ni kuanzisha mfumo wa usimamizi wa kutathimini na kuzuia uharibifu wa barabara (*Establishment of Overloading Management System and Harmonizing of Road Damage Control and Evaluation*) pamoja na kutathimini ajali za barabarani na kuzuia ajali (*Accident Analysis and Control*).

Mheshimiwa Spika, Usalama, Mazingira na Marekebisho ya Mfumo (*Institutional Support to Safety, Environment and Reforms*) Shilingi 1,215.88 Milioni. Mradi huu una lengo la kugharamia shughuli za Usalama na Mazingira pamoja na Marekebisho ya Mfumo wa utekelezaji wa shughuli katika maeneo haya. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na *DANIDA*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 mradi huu umetengewa fedha za ndani shilingi milioni 535.88 na shilingi milioni 680.00 fedha za nje kwa ajili ya kulipia gharama za ushauri wa kitaalamu (*Technical Assistance*) katika kuandaa programu za maendeleo ya sekta, kujenga uwezo wa watumishi wa Idara (*Capacity Building*), kutoa elimu ya usalama barabarani (*Road Safety Education*) pamoja na kugharamia matangazo yanayohusu usalama barabarani kuelimisha umma kwa njia ya luninga, magazeti, vipeperushi n.k. (*Road Safety Campaign*).

Mheshimiwa Spika, Menejimenti na Utunzaji wa Mazingira (*Environmental Management Assessment - EMA*) – Shilingi 339.50 Milioni. Mradi huu una lengo la kutekeleza usimamizi wa Sheria ya Mazingira katika sekta. Mwaka wa fedha 2011/2012, kiasi cha shilingi milioni 105.00 fedha za ndani na shilingi milioni 232.50 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya shughuli za kusimamia utekelezaji wa

Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 kwa miradi ya ujenzi inayotekelezwa na kutoa mafunzo kuhusu tathmini na usimamizi wa mazingira katika sekta ya ujenzi. Shughuli nyingine ni maandalizi ya programu mbalimbali za uhabibi wa uchafuzi wa kimazingira katika sekta na kujenga uwezo wa kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza wakati wa kutekeleza miradi mbalimbali ya sekta.

Mheshimiwa Spika, fedha za Mfuko wa Barabara kwa Mwaka 2011/2012. Katika mwaka 2011/2012, kiasi cha shilingi 221,585,980,000 fedha za Mfuko wa Barabara zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali ya barabara, vivuko na usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya barabara. Kati ya fedha hizo, Wizara ya Ujenzi imetengewa shilingi 21,936,984,300, *TANROADS* shilingi 197,432,856,700 na shilingi 2,215,857,000 zitatumika kugharamia sehemu ya uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, fedha za Mfuko wa Barabara za Wizara ya Ujenzi zitatumika kutekeleza miradi ya Miradi ya Barabara Kuu ambayo imetengewa shilingi 9,011,713,150. Aidha, Miradi ya Barabara za Mikoa inayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imetengewa shilingi 10,036,170,317.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ni ununuzi wa vivuko vya Kilambo na Itungi Port ambavyo vimetengewa jumla ya shilingi 1,763,733,538. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,445,769,512 ni kwa ajili ya Kivuko cha Kilambo na shilingi 317,964,026 ni Kivuko cha Itungi Port. Shughuli za Usimamizi na Ufuatiliaji Miradi umetengewa shilingi 1,125,367,295

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Matengenezo ya Barabara kwa Mwaka 2011/2012. Fedha za matengenezo ya Barabara Kuu na Barabara za Mikoa kwa mwaka 2011/2012 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni jumla ya shilingi 197,434,856,700. Fedha hizi zitatumika kwa kazi za matengenezo ya barabara kuu kilomita 9,844, madaraja ya barabara Kuu 1,129, barabara za Mikoa kilomita 20,649 na madaraja yake 1,196. Aidha, mradi wa majaribio wa kufanya matengezo ya muda mrefu katika Mikoa ya Mwanza, Rukwa na Tanga (*PMMR*) zitahusisha kilomita 1,092 pamoja na shughuli za mizani na matengenezo ya dharura.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa narabara nchini. Nchi ya Tanzania ina ukubwa wa eneo linalofikia kilometa za mraba 949,000 na mtandao wa barabara wenye jumla ya kilometa 86,472. Mchanganuo wake ni kwamba, km 12,786 ni za Barabara Kuu, kilometa 21,105 ni za Barabara za Mikoa na Barabara za Wilaya ni kilometa 52,581. Aidha, kuna jumla ya Madaraja 4,880 katika Barabara Kuu na za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Mpango Maalum wa Kitaifa wa Kuinua Matumizi ya Teknolojia ya Nguvu Kazi (*Taking Labour Based Technology to Scale*). Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo cha Nguvu Kazi kimepanga kuendesha mafunzo kwa Makandarsi na Wahandisi yanayohusu utunzaji na ukarabati wa barabara za changarawe kwa kutumia teknolojia ya Nguvu Kazi katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Iringa na Ruvuma. Aidha, Chuo kitaendesha mafunzo mafupi kwa Makandarasi kuhusu namna ya kujenga barabara zenye magari machache kwa kiwango cha lami (*Low Volume Sealed Roads*). Chuo pia kitaendelea kuhamasisha wananchi kutumia Teknolojia ya Nguvu Kazi katika kazi za barabara ili kuongeza kipato chao kutokana na sekta ya ujenzi kwa kupitia vyombo vya upashanaji habari.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wanawake. Katika mwaka 2011/2012, Wizara inaendelea kuhamasisha wanawake kushiriki katika kazi za barabara kwa kuendesha mafunzo kwa Waratibu wa uhamasishaji wa wanawake 20 wa Mikoa na kuendesha mafunzo ya ukandarasi kwa wanawake 15 wa kutumia teknolojia ya Nguvu Kazi. Aidha, ufuatiliaji wa maendeleo ya wanawake waliopatiwa mafunzo ya ushiriki katika kazi za barabara na kukamilisha miongozo ya ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara zitazingatiwa katika mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya watumishi. Katika mwaka 2011/2012, watumishi 40 wanatarajiwa kupewa mafunzo, kati ya hao, 30 watahudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi na watumishi 10 watakwenda nje ya nchi kwa mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kupambana na UKIMWI. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi walioathirika kwa virusi vya UKIMWI kwa kuwapa lishe bora kulingana na mwongozo wa kuhudumia watumishi wa Umma walioathirika na UKIMWI pamoja na kutoa elimu ya kupambana na maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya rushwa. Katika kupambana na vita dhidi ya rushwa, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa kutoa elimu kwa watumishi wote kwa kupitia semina mbalimbali kuhusu athari za rushwa na makosa ya rushwa yanayoweza kutendeka. Aidha, Wizara itahakikisha inahusisha vyombo vya dola kama vile Polisi, PCCB na kadhalika. Katika kuwadhibiti watumishi wanaopokea rushwa kwenye mizani, mikataba mbalimbali ya ujenzi na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, Habari, Elimu na Mawasiliano. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuratibu na kuandaa vipindi maalum kwenye Televisheni, Radio, Magazeti na Vijarida ili kutoa elimu kwa umma kuhusu shughuli za ujenzi. Aidha, Wizara itatumia fursa hiyo kutangaza matukio mbalimbali ya sekta ya ujenzi, mafanikio yanayopatikana, pamoja na matarajio ya utekelezaji wa shughuli zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Wakala wa Barabara umekabidhiwa jukumu la kukarabati na kufanyia matengenezo Barabara Kuu na za Mikoa zenye jumla ya kilometa 33,891. Katika mwaka 2011/2012, Wakala utaendelea kusimamia kazi za kukarabati, kujenga na kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mikoa zenye urefu wa kilometa 33,891 kulingana na bajeti iliyopangwa. Matengenezo ya barabara kuu na Mikoa yanayotarajiwa kufanyika yatahusisha matengenezo ya kawaida (*routine maintenance*) kilometa 27,345, matengenezo ya muda maalum kilometa 2,259 na madaraja 2,325. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za utawala na usimamizi wa kazi, udhibiti wa uzito wa magari, kazi za dharura, mradi wa matengenezo ya muda mrefu na kazi zinazosimamiwa toka Makao Makuu za mipango, usalama barabarani na hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Wakala pia utaendelea kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa Barabara Kuu ambapo kilometa 818 ni ujenzi mpya kwa kiwango cha lami na kilometa 211 ni za ukarabati kwa kiwango cha lami. Kwa upande wa barabara za mikoa, wakala umepanga kukarabati kilometa 956.9 kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa 36.9 kwa kiwango cha lami na madaraja 22.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo ya Serikali (*TBA*). Katika mwaka 2011/2012, Wakala umepanga kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea pamoja na kuongeza jitihada katika kununua viwanja zaidi Mikoani ili kuiwezesha wakala kujenga nyumba nyingi zaidi za watumishi wa Serikali. Mikakati mingine ni kujikita zaidi katika kutoa huduma bora za ushauri wa kitaalam kwa miradi ya ujenzi wa nyumba za watumishi na ofisi za Serikali zitakazozingatia mahitaji na matakwa ya watu wenye ulemavu. Aidha, Wakala utaboresha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo mabalimbali, kubuni na kuibua vyanzo vipya mapato na kuendelea kufanya matengenezo ya Majengo ya Serikali na ununuzi wa samani kwa nyumba za viongozi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ufundi na Umeme (*TEMESA*). Katika mwaka 2011/2012, Wakala utaendelea na mchakato wa kununua vivuko vipya vya Ilagala (Tani 50) Mkoani Kigoma na Itungi Port (Tani 35) Mkoani Mbeya na kutengeneza magari 10,740 katika Karakana za zilizopo kila Mkoa.

Aidha, Wakala utaendelea kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozzi na mabarafu katika majengo ya Serikali na kuendelea na ukarabati wa karakana na kuzipatia vitendea kazi vya kisasa na kusimamia uendeshaji wa vivuko vya Serikali na ukodishwaji wa mitambo mbalimbali pamoja na magari maalum ya viongozi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara (*RFB*). Katika mwaka 2011/12, Bodi imepanga kuendelea na mapendekezo ya kuongeza vyanzo vipya vya mapato ya mfuko. Bodi

itaweka mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kudhibiti uchakachuaaji wa mafuta na kuweka mikakati ya kuongeza uwezo na ufanisi wa Taasisi zinazotumia fedha za mfuko wa barabara kutumia fedha za mfuko kikamilifu. Aidha, Bodi itaanzisha utaratibu wa kuwatumia wataalam washauri waliopo maeneo husika (*local consultants*) kwa ajili ya kukagua ubora wa kazi (*value for Money*) wakati miradi ya matengenezo ya barabara inaendelea.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*ERB*). Katika mwaka 2011/2012, Bodi imepanga kusajili Wahandisi 750, Mafundi Sanifu 200 kampuni za ushauri wa kihandisi 16 pamoja na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa Wahandisi wahitimu 800. Aidha, Bodi itafanya ukaguzi wa kina katika kampuni za kigeni na za ndani ili kubaini kama kazi za kihandisi zinafanywa na Wahandisi waliosajiliwa kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi na kuwashauri Wahandisi wataalam waanzishe kampuni za uhandisi Mikoani kwa kutembelea mikoa yote. Bodi pia itahamasisha utekelezaji wa sheria mpya ya usajili wa Wahandisi na itaendelea kuandaa mitihani ya kitaaluma, kozi fupifupi na mihadhara ya kitaaluma kwa wahandisi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2011/2012, Bodi kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Wizara, itakagua kubaini ubora wa ujenzi wa barabara zote ikiwa ni pamoja na barabara za *TANROADS* na zile za Halmashauri. Aidha, Bodi itaendelea kuwashawishi Wahandisi Wataalam waanzishe Kampuni za Ushauri wa Kihandisi Mikoani, ili kuipeleka huduma hiyo jirani na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (*AQRB*). Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya mwaka 2010. Wabunifu Majengo 26 na Wakadiriaji Majenzi 15, kampuni za Wabunifu Majengo 15 na Kampuni za Wakadiriaji Majenzi 22 zinatarajiwa kusajiliwa. Bodi pia itaendelea kusimamia mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu 40, ili kuhakikisha wahitimu wanapata mafunzo yanayokidhi haja ya sekta ya ujenzi kulingana na sheria. Ukaguzi wa majenzi utafanyika katika makao Makuu ya Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara. Aidha, ili kuzuia ujenzi usiofuata Sheria katika Miji inayokua kwa kasi, Bodi itafanya ukaguzi wa marudio katika Miji hiyo ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mwanza, Mbeya, Iringa, Morogoro, Bukoba na Moshi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Makandarasi (*CRB*). Katika mwaka 2011/2012, Bodi imepanga kusajili makandarasi 853 na kukagua miradi ya ujenzi 3000. Pia, Wizara itaendelea na mkakati wa kuwaendeleza Makandarasi wa ndani 15 mpaka 30 ili waweze kutoa ushindani kwa Makandarasi wa nje kwenye ushiriki wa miradi mikubwa. Mafunzo kwa vitendo yatatolewa na Mshauri Mtaalam kuhusu namna ya kujenga barabara za lami. Aidha, kuna mkakati wa kuwanufaisha Makandarasi wadogowadogo kwa njia ya kupata *sub-contracts*. Wizara pia ina Mkakati wa Kuimarisha Mfuko wa Kuwasaidia Makandarasi wadogo (*Contractors Assistance Fund - CAF*) hususan wa ndani, kwa lengo la kutoa dhamana ya mikopo ya kukuza mitaji yao.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Ujenzi (*NCC*). Katika mwaka 2011/2012, Baraza linalenga kuendelea kutoa msukumo katika uhuishaji wa Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003, kuandaa Kanuni za utekelezaji wa Sheria iliyoanzisha Baraza, kuratibu na kutoa mafunzo katika sekta, ushauri wa kiufundi na utatuzi wa migogoro pamoja na kufanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, pamoja na miradi inayoendelea, Kikosi cha Ujenzi kinategemea kutekeleza miradi mitano (5). Miradi hiyo inahusu ukarabati wa Jengo la Boma la Kale Bagamoyo (*Phase III*), Ujenzi wa Nyumba za Viongozi Dar es Salaam na Mwanza, ujenzi wa Majengo ya abiria katika Kivuko cha Musoma – Kinesi na ukarabati wa Majengo ya Ofisi na nyumba za watumishi – Siha Kilimanjaro. Aidha, Kikosi kitaendelea kuboresha utaratibu wa utendaji (*restructuring*) ili kiwe na watumishi wenye sifa na wanaohitajika, pamoja na kuboresha vitendea kazi katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ujenzi – Morogoro. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo kimepanga kuendeleza ujenzi wa jengo jipya la madarasa na karakana ya

ufundi, kukarabati majengo manne (4), kununua samani na zana za kufundishia. Aidha, Chuo kitafundisha jumla ya mafundi 480 kama ifuatavyo:- Mafundi Sanifu wa Barabara, Majengo na Ufundi 90, Madereva Bingwa wa Umma 30, Madereva waanzaji 180 na Mafundi Stadi wanaoanza toka fani za barabara, Majengo na Ufundi 180.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia katika Sekta ya Uchukuzi (*Tanzania Transportation Technology Transfer (Tant²) Centre*). Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kituo kimepanga kuendelea na jukumu lake la kusambaza teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi hapa nchini. Aidha, Kituo kimepanga kusambaza kwa wadau 200,000 jumla ya makala na taarifa 150 zinazohusu teknolojia mbalimbali katika sekta ya barabara na uchukuzi kwa ujumla na kuendelea kuhamasisha wadau kutumia huduma zake, kuyapokea na kuyafanyia kazi maombi yasiyopungua 100 ya makala na taarifa kuhusu teknolojia mbalimbali kutoka kwa wadau wa sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, Kituo kwa kushirikiana na wadau kimepanga kuandaa rasimu yenye mapendekezo yanayolenga kuboresha jinsi ya kuendesha shughuli za utafiti zinazolenga kutatua changamoto zinazokabili Sekta ya Uchukuzi hapa nchini Tanzania. Aidha, Kituo kitaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuimarisha Wanafunzi wa Shule za Sekondari wanaochukua masomo ya Sayansi (*TRAC Programme*) kwa shule sita (6) za Sekondari na Shule moja ya Msingi Jijini Dar es Salaam na kuhamasisha shule za sekondari nyingine ili ziweze kuanza kutekeleza mradi huu. Pia, Wizara kupitia Kituo hiki inategemewa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa Kuhusu Usambazaji wa Teknolojia katika Sekta za Ujenzi na Uchukuzi Barani Afrika anaotarajiwa kuhudhuriwa na washiriki wapatao 300 kutoka Barani Afrika na Mabara mengine duniani. Mkutano huu utafanyika Arusha, Tanzania, tarehe 21 – 25 Novemba, 2011

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru tena Kamati ya Bunge ya Miundombinu ikiongozwa na Mwenyekiti wake Peter Serukamba kwa michango, ushauri na ushirikiano waliotupa katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango, changamoto na ushirikiano mlionipa katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, shukurani zetu ziwafikie wadau mbalimbali hasa wa sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya sekta zetu. Shukurani zetu pia ziwaendee Washirika wetu wa Maendeleo waliochangia katika kutekeleza programu na mipango yetu ya sekta. Nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyochangia kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta yetu ni pamoja na China, Demark, *EAC*, India, Japan, Korea, Marekani, Norway, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Benki ya Dunia (*WB*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Umoja wa Nchi za Ulaya, Kuwait *Fund*, *OPEC Fund* na wengine wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninapofika mwisho wa hotuba hii sina budi kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara nikianza na Mheshimiwa Dokta Harrison G. Mwakyembe, Naibu Waziri; Balozi Herbert E. Mrango, Katibu Mkuu; Eng. Dokta John S. Ndunguru, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti wa Bodi za *TANROADS*, *TEMESA*, *TBA*, *RF*, *ERB*, *CRB*, *AQRB* na *NCC* na Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na watumishi wote wa Wizara na Taasisi wakiwemo *Regional Managers* wa *TEMESA*, *TBA* na *TANROAD* na watumishi wengine wote. Wote kwa pamoja wamenipa ushirikiano mkubwa ambao umenisaidia kutekeleza majukumu niliyopewa ya kusimamia uendelezaji wa sekta za ujenzi. Michango yao ya mawazo na utendaji wao mzuri vimewezesha kufanya kazi yetu kuwa rahisi na yenye mafanikio. Tunawashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wa Jimbo langu la Chato, kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na kuendelea kushirikiana nami katika kipindi chote cha utumishi wangu katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Nawashukuru sana wa Vyama vyote. Nitaendelea kuienzi fursa hii adhimu waliyonipa kuwa mwakilishi wao. (Makofi)

Aidha, napenda kushukuru familia yangu ikiongozwa na mama yangu mzazi Suzan, Mke wangu na viongozi wote wakiwemo wa dini zote kwa kuendelea kuniombea na kuliombea Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imetayarisha Mpango na Bajeti ya mwaka 2011/2012 kwa kuzingatia Mwongozo wa Kutayarisha Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha. Mwongozo huo unalenga katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005-2010 na wala siyo chama kingine, Dira ya Taifa ya Maendeleo (*Vision 2025*), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) pamoja na mikakati mbalimbali ya Kitaifa na kisekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida 2011/2012, katika mwaka 2011/2012, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 245,440,294,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizi za Matumizi ya Kawaida, Sh. 15,879,643,781/= ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Sh. 221,585,980,000/= ni fedha za Mfuko wa Barabara na Sh. 7,974,670,219/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na Taasisi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo Kwa Mwaka 2011/2012, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Ujenzi inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 1,250,976,939,000/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Sh. 621,106,746,000/= ni fedha za ndani na Sh. 629,870,193,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato katika Bajeti hii, ni 1,496,417,233,000. Fedha hizo zinajumuisha mishahara 15,879,643,781, Mfuko wa Barabara Sh. 221,585,980,000/=, Matumizi mengineyo Sh. 7,974,670,219/=, Fedha za Ndani kwa ajili ya miradi ya Maendeleo 621,106,746,000, fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo Sh. 629,870,193,000/=. Kwa hiyo, jumla kuu ya fedha ambazo naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe na lipitishie katika bajeti ya mwaka 2011/2012 ili miradi hii mingi ya barabara, nyumba, ya vivuko na kadhalika iweze kutekelezwa kikamilifu na ningewaomba sana Wabunge wote wa CCM, CHADEMA, CUF, UDP, NCCR-Mageuzi, TLP na wengine wote hata wale ambao hawana vyama, waweze kupitisha bajeti hii ili tukaweze kutenda kazi kwa ajili ya kuwahudumia wananchi na barabara ziweze kupitika kwa sababu barabara ni uchumi. Wasipunguze hata shilingi na kwa Mbunge atakayepunguza shilingi ajue tumepunguza kwa barabara zake na wananchi wajue hilo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kutoa hoja na kushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Haya ya mwisho hayajaandikwa kokote. *(Kicheko)*

MHE. ANNE K. MALECELA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOBINU): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimamia mbele yako leo. Nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi pamoja na wapiga kura wangu wa Jimbo la Same Mashariki kwa kuendelea kuniamini. Pia napenda kutumia nafasi kumshukuru mume mpendwa John Samuel Malecela na wanangu Naki Nyange Wilmo, Ikumbo Nyange, Nafue Nyange, Nyange Edward Nyange na mwanangu wa mwisho Rich Joshua Kilango. Pamoja na wajukuu zangu malaika, Jack na Noah kwa kunipa moyo na kunivumilia ninapokuwa mbali nao nikiwatakia wananchi wangu wa Jimbo la Same Mashariki na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. Pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo Kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue fursa hii, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za

Bunge, Toleo la 2007, utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Ujenzi kwa maandalizi mazuri, ushirikiano na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hiyo mbele ya Kamati yangu kuhusu Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya 2011/2012. Aidha, Wizara pia iliwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa Maagizo ya Kamati na Mipango ya Bajeti ya 2010/2011 na kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na maombi ya fedha kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu inasimamia Wizara tatu, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mimi na Wanakamati wenzangu, tunaitambua dhamana hii kubwa na napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na umma wa Watanzania kwamba, kwa niaba yenu, kazi ya kupitia bajeti hizi tulizifanya kwa umahiri na umakini mkubwa na kufanikisha baadhi ya mabadiliko yenye tija kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua mapendekezo ya Bajeti hii Kamati ilipitia utekelezaji wa maagizo ya Kamati mwaka 2010/2011, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka huo, mafanikio na changamoto za utekelezaji wa bajeti hiyo na mwelekeo wa mpango wa bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara ya Ujenzi Kwa Mwaka 2010/2011, Wizara hii imeanza mwaka 2010/2011, kwa hiyo bajeti hii ya mwaka 2011/2012 ni ya kwanza kwani awali Wizara hii ilikuwa sehemu ya Wizara ya Miundombinu. Hata hivyo, Wizara ya Ujenzi imejitahidi kutekeleza maagizo yote yaliyokuwa yanaangukia chini yake. Aidha, yapo maagizo ambayo yametekelezwa kwa ukamilifu na yapo maagizo, ambayo utekelezaji wake ni wa muda mrefu na bado Wizara inaendelea kuyafanyia kazi. Kamati imeridhika na hali ya utendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2010/2011, ukusanyaji mapato, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara iliweka malengo ya kukusanya mapato ya Sh. 42,100,000/=. Mpaka kufikia Aprili 2011, jumla ya shilingi 53,771,085 zilikuwa zimekusanywa na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 123%. Ongezeko hilo limetokana na marejesho ya fedha za Serikali, ada ya ukaguzi na usajili wa magari ya Serikali pamoja na uuzaji wa nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara ilitengewa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida Sh. 298,495,949,166/= ikiwa ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara na ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara na matumizi mengineyo, hadi kufikia Mei, 2011 Wizara ilikuwa imepokea Sh. 261,492,533,257/= ikiwa ni 87.6% ya makadirio yote.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 2010/2011, katika mwaka 2010/2011, Serikali ilitenga Sh. 710,945,105,000/= kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Mpaka kufikia Mei, 2011 Sh. 426,939,525,000/= zilikuwa zimetolewa ambayo ni 60.05% ya bajeti iliyopitishwa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2010/2011. Kwa ujumla Wizara imepata mafanikio katika utekelezaji wa mipango ya mwaka 2010/2011, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo ni hizi zifuatavyo:-

Kutopata fedha kwa wakati kulingana na mahitaji halisi ya miradi ya maendeleo hususan barabara. Matokeo yake ni kupunguzwa kwa kasi ya utekelezaji wa miradi pamoja na madai ya riba na fidia ya *idle time* ya vifaa na wafanyakazi wa makandarasi. Hali hii imeathiri utekelezaji wa miradi kwa kushindwa kulipa makandarasi kwa wakati na kusababisha jumla ya makandarasi 17

wanaotekeleza miradi 30 ya barabara kutoa notisi za kusimamisha na wengine kupunguza kasi ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya barabara (*Road Reserve*). Watu wengi wamekuwa wakijenga katika maeneo ya hifadhi ya barabara na kusababisha usumbufu wa fidia zinazoongeza gharama kubwa katika ujenzi wa barabara kwa ujumla.

Uwezo mdogo wa kimtaji walionao Wakandarasi Wazalendo. Wakandarasi hao hushindwa kushiriki kikamilifu katika fursa za kazi kutokana na masharti ya upatikanaji wa dhamana za zabuni, dhamana za ushiriki wa kazi na mitaji ya kuwezesha kazi kutoka mabenki kuwa ngumu na kutozingatia mahitaji halisi ya shughuli za Kihandisi. Aidha, kushindwa kupata mitaji kunawafanya Wakandarasi kushindwa kukua na kupata fursa ambazo zitawezesha kuwakwamua ili kushiriki katika ushindani wa zabuni za miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, Mikakati, ili kukabiliana nazo changamoto hizo Wizara ina mikakati ifuatayo:-

Wizara kupitia Bodi ya usajili wa Wakandarasi (*CRB*) imeanzisha Mfuko wa kuwasaidia Wakandarasi wadogo (*Contractors Assistance Fund-CAF*) hususan Wakandarasi wa ndani kwa lengo la kutoa dhamana ya mikopo ya kukuza mitaji yao. Aidha, Bodi kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa makandarasi wa ndani ili kujenga uwezo wao. Bodi kuendelea kuhimiza Wakandarasi wadogo kuungana ili waweze kuwa na uwezo wa kupata kazi kubwa.

Katika suluhisho la muda, Wizara iliomba Serikali kuongeza fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya Wakandarasi kwa miradi ya barabara inayosimamiwa na Wizara. Serikali ilikubali kuiongezea Wizara fedha kwa kuhamisha kutoka mafungu mengine kiasi cha shilingi bilioni 255 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa 2010/2011.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaandaa mpango wa kuelimisha umma kwa njia ya vyombo vya habari, vipeperushi, mikutano na semina ili waweze kufahamu vyema Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 kwa minajili ya kuzuia ujenzi katika maeneo ya akiba ya barabara.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Bajeti na mpango wa Bajeti kwa mwaka 2011/2012, makadirio ya ukusanyaji wa mapato. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kupitia Idara mbalimbali na Vitengo vyake inatarajia kukusanya jumla ya Sh. 36,583,000/=.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya kawaida na maendeleo, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imetengewa jumla ya sh. 245,440,294,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 1,250,976,939,000/= kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hivyo, makadirio kwa ajili ya matumizi kwa mwaka 2011/2012, jumla ni sh. 1,496,417,233,000/=.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa kamati, miradi ya ujenzi wa barabara wakati wa kutekeleza zoezi la kubomoa nyumba za wananchi ili kupisha upanuzi wa barabara, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza zoezi hilo kwa umakini ili kuepusha manung'uniko ya wananchi hasa pale wanapocheleweshwa kulipwa haki zao za fidia, punde zoezi hilo linapokamilika. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuanza mara moja ujenzi wa miradi maeneo ambayo watu wamehamishwa, kwani kuchelewa kuanza kwa miradi hiyo husababisha ongezeko la gharama za mradi tofauti na ilivyokadiriwa na wakati fulani wananchi kuanza kuvamia tena. Aidha, Sheria za Ardhi na Sheria za Barabara zipitiwe upya ili kuondoa utata na kutatua tatizo hili sugu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miradi ya barabara unahitaji fedha nyingi, kwa kuwa Serikali haina fedha za kutosha Kamati inashauri iangalie maeneo ambayo inaweza kubana matumizi, kwa mfano, kupunguza matumizi ya magari yasiyo ya lazima. Hili lifanyike kwa kuhakikisha kuwa Maafisa wa Serikali wanaostahili kutumia magari ya Serikali wakopeshwe magari na kupewa posho maalum kwa ajili ya kununulia mafuta ya kuendeshea magari hayo badala ya kutumia magari ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya utafiti na kubaini kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, kiasi cha sh. 74,637,915,279/= kimepangwa kutumika kwa ajili ya kununulia mafuta, *oil* na vilainishi pamoja na kufanyia matengenezo ya magari ya Serikali kwa mujibu wa kasma namba 220300 na kasma namba 230400 ya vitabu vya Bajeti ya Serikali vilivyowasilishwa mbele ya Kamati. Aidha, kutokana na aina ya magari yanayotumika na maafisa wengi wa Serikali ya Toyota *VX* kuwa ya gharama kubwa Serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kununua magari haya ikiwa ni wastani wa shilingi milioni mia mbili na sitini (260,000,000/=) kwa gari moja ambalo linatumiwa na ofisa mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kusimamisha ununuzi wa magari kwa sasa, hata hivyo, ni vyema kusimamishwa huku kukaenda sambamba na kubadili sera ili Serikali ibaki na mzigo wa kugharamia magari ya huduma badala ya kugharamia magari ya kutumiwa na maafisa kwenda na kurudi kazini. Katika nchi zilizoendelea watumishi wa Serikali wanatumia magari yao au usafiri wa umma kwenda na kurudi kazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa miradi ya barabara mwajiri anawakilishwa na Wakandarasi washauri katika kusimamia ubora wa kazi zinazofanywa na mkandarasi. Ili mkandarasi mshauri aweze kufanya kazi zake kwa ufanisi, anapaswa kupewa malipo yake kwa wakati. Kucheleweshwa malipo kwa Wakandarasi Washauri kunasababisha wapunguze ufanisi na wakati mwingine kuwa upande wa Mkandarasi kwa kuwa anaweza kushawishiwa kirahisi ili kutomsimamia vizuri, hali ambayo inasababisha Serikali kupokea miradi iliyojengwa kwa kiwango cha chini kutokana na kukosa usimamizi mzuri wa Wakandarasi Washauri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara zinazohitajika kujengwa ni nyingi na kwa kuwa Serikali haina fedha za kutosha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutumia mpango wa *BOT (Build - Operate and Transfer)*, *BOOT (Build - Own - Operate and Transfer)* na ule wa *PPP (Public Private Partnership)* kwa uwazi ikiwemo kutumia sera, sheria na kanuni zilizopo. Hii itahamasisha wawekezaji wengi zaidi kujitokeza kushiriki katika ujenzi wa Miundombinu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, barabara zetu nyingi zimejengewa matuta kwa ajili ya kuwalazimisha madereva kupunguza mwendo. Maeneo yenye matuta ni pamoja na maeneo yenye watu wengi, kwenye mbuga za wanyama na kwenye miteremko mikali. Kamati inaunga mkono ujenzi wa matuta haya kwani hata baadhi ya maeneo wanavijiji wanalazimisha yajengwe. Hata hivyo, hakuna kipimo wala aina maalum ya matuta kiasi kwamba mengine ni makubwa mno. Aidha, matuta yanayojengwa kwenye miteremko mikali yanahatarisha usalama wa magari yanayopanda milima hiyo hasa kwa malori makubwa ya mizigo kwani matuta yanakuwa kikwazo. Matuta aina ya rasta yanaharibu magari, hivyo, yaondolewe kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kujenga barabara nchini. Katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2011 takriban kilomita 12,000 zimekuwa kwenye hatua mbalimbali za ujenzi kwa kiwango cha lami. Ni imani ya Kamati kuwa barabara hizi zitakamilika mapema iwezekanavyo ili kuboresha mawasiliano ya barabara nchini. Aidha, Kamati inashauri ujenzi wa barabara zinazounganisha Mikoa upewe kipaumbele ili kuunganisha Mikoa yote na kuinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya kujenga barabara nyingi nchini, Kamati inashauri Serikali isiingie mikataba ya ujenzi na Wakandarasi kabla ya kupata fedha za kugharamia miradi husika kwani kufanya hivyo kunaiongezea Serikali gharama zisizo za lazima kwa kulipa faini na riba zinazotokana na ucheleweshaji wa malipo baada ya kazi kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miradi ya vivuko na ujenzi wa nyumba za Serikali. Serikali imetenga kiasi cha sh. 799,415,000/= kwa ajili ya ukarabati wa vivuko vitatu. Kamati inashauri kuwa ubovu wa vivuko utambuliwe na kufanyiwa ukarabati mapema ili kuepusha majanga yanayotokana na ubovu wa vivuko hivi. Aidha, kila inapowezekana Serikali iendeleo kununua vivuko vipya ili kurahisisha usafiri kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mizani ya barabarani, mizani ya kupima uzito wa magari barabarani ina umuhimu mkubwa sana. Hata hivyo, ili iweze kukidhi matarajio ya wananchi Kamati inashauri kuwa teknolojia za kisasa ambazo zinawezesha ufuatiliaji wa utendaji kazi wa vituo kutoka makao

makuu ya *TANROADS* kwa lengo la kudhibiti rushwa. Aidha, magari yanayozidisha uzito unaotakiwa walipishwe faini na kuamriwa kupunguza mizigo iliyozi kwani yakiendelea na safari yao yatakuwa yameruhusiwa kuendelea na uharibifu wa barabara huko yaendako.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam ni tatizo kubwa sana na sababu zake ni mtambuka. Moja kati ya sababu ni kutokuwa na maono ya mbali ya ukuaji wa miji yetu, ujenzi wa miundombinu kutozingatia ukuaji wa miji na ongezeko la watu kwa miaka mingi ijayo. Aidha, uwepo wa maofisi mengi ya Serikali katikati ya Jiji, huduma nyingi za jamii na biashara kuwepo katikati ya Jiji na hivyo kupelekea magari mengi kuwa na mwelekeo wa aina moja hasa nyakati za asubuhi na za jioni. Sababu nyingine ni uchache wa mabasi yanayotoa huduma ya usafiri na kuwa na huduma hafifu, hali hiyo inalazimisha wakazi wa Jiji kutoa kipaumbele kwenye usafiri wa magari binafsi badala ya kutumia mabasi hayo.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili lina athari nyingi sana kiuchumi na kijamii kwa wakazi wa Dar es Salaam na Taifa kwa ujumla. Wafanyakazi wanachoka kabla ya kuanza kazi kwa kuwa wanatumia muda mwingi barabarani, hali hii inapunguza tija. Kwa mfano, wastani wa mwendo katika barabara kuu za jiji umefikia kilomita tano mpaka kumi kwa saa. Msongamano huu unasababisha matumizi makubwa ya mafuta ya magari hali ambayo inaathiri uchumi wa wakazi wa Jiji ikiwemo uchafuzi wa mazingira, uchafuzi wa hali ya hewa unasababisha magonjwa yanayoligharimu Taifa fedha nyingi kuyatibu.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam ndiyo sura ya Taifa letu, wageni wengi wanatembelea Jiji hili pamoja na ukweli kwamba shughuli nyingi za Kiserikali ziko Dar es Salaam. Hivyo, taswira inayooneshwa kutokana na msongamano huu ni mbaya na hivyo kuwafanya walidharau Jiji letu na Taifa kwa ujumla. Aidha, zaidi ya 84% ya kodi za ndani zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania zinapatikana jijini Dar es Salaam. Tafsiri yake ni kwamba uchumi wa nchi hii kwa sehemu kubwa unategemea shughuli za kiuchumi zilizopo Jijini Dar es Salaam ambazo kwa bahati mbaya zinatatizwa na usafiri na hivyo kudhoofisha uchumi wa nchi pia.

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyotolewa na Wakala wa Mradi wa Mabasi yaendayo kasi ilieleza kuwa utafiti umebaini Tanzania inapoteza kiasi cha sh. 4,000,000,000/= kila siku kutokana na msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam. Ili kuondoa hasara hii Kamati inashauri Serikali itekeleze mipango yote iliyopendekezwa na wataalam na watafiti mbalimbali. Baadhi ya mipango hii ni kujenga na kuimarisha barabara za mchepuo (*feeder roads*), uboreshaji wa usafiri wa Shirika la *UDA*, kujenga barabara za juu (*fly overs*), usafiri wa boti kutoka Bagamoyo mpaka feri pamoja na usafiri wa reli Jijini Dar es Salaam na usafiri wa mabasi yaendayo kasi (*DART*).

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa barabara za Dar es Salaam Kamati inashauri kuwa ni vema barabara nyingi za mchepuo katikati ya Jiji zijengwe kwa lami ili kupunguza msongamano kwenye barabara kuu nne za Jiji la Dar es Salaam. Aidha, Kamati inapendekeza Serikali ianze kufikiria mradi mkubwa wa *Highway-Cum- Industrial Corridor* itakayokuwa kama Dar es salaam *By-pass* kutokea maeneo ya Bagamoyo kupitia Kibaha, Kisarawe, Msongola, Kongowe hadi Kigamboni. *Corridor* hii itaweza kuwa na barabara kubwa za njia sita na itawezesha kuwa na njia nyingi za kuingia katikati ya jiji. Aidha, pembezoni mwa barabara hii patatengwa viwanja vya kuendeleza viwanda na hivyo viwanda visiendeleo kujengwa katikati ya Jiji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hasara iliyoenezwa ya sh. 4,000,000,000/=, kila siku nchi yetu inapoteza kiasi cha sh. trilioni 1.44 kiasi ambacho ni karibu sawa na bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka mzima. Jambo hili si dogo na linapaswa kupewa uzito wa pekee na wa dharura.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefurahishwa na ahadi mpya ya Serikali na *NSSF* kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu mkandarasi atakuwa ameanza ujenzi wa daraja la Kigamboni. Kamati inaamini kuwa safari hii ahadi hii itakuwa ni ya kweli. Kamati ilipewa taarifa kuwa daraja hilo litajengwa na *NSSF*, mpaka mwezi Februari, 2011 shirika hilo lilikuwa limeshapata 60% ya fedha zitakazotumika katika ujenzi wa daraja hilo. Kamati inashauri kuwa iwapo shirika hilo halijapata fedha zilizobaki Serikali iongeze 40% iliyobaki ili ujenzi huo uanze mapema kuepuka kupanda kwa gharama ya ujenzi na kupunguza hasara ya sh. 4,000,000,000/= kwa siku kutokana na tatizo la usafiri Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, usafiri katika miji yetu unasimamiwa na wadau wengi ambao wakati mwingine hawashirikiani katika utekelezaji wa majukumu yao kutokana na migongano ya maslahi. Kwa mfano, katika Jiji la Dar es Salaam wadau wanaosimamia usafiri ni pamoja na *SUMATRA*, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Manispaa zote tatu za Dar es Salaam, Askari wa Usalama Barabani, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Hali hii inapunguza ufanisi kiutendaji na kuongeza tatizo la msongamano.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuwa na wadau wengi pia linajitokeza kwenye mradi wa mabasi yaendayo kasi katika Jiji la Dar es Salaam (*DAR7*). Mradi huu uko chini ya mamlaka zifuatazo:-

Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa za Dar es Salaam, Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam, Mamlaka ya Kudhibiti Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (*SUMATRA*) na Wakala wa Taifa wa Barabara (*TANROADS*). Katika hali hii ni vigumu kufikia maamuzi ya haraka kutokana na kila mamlaka kuwa na Mpango kazi wake na hivyo kuwa na urasimu mkubwa kwenye utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msongamano wa magari pia limeanza kujitokeza katika Majiji ya Mwanza na Arusha. Kamati inashauri hatua za kutatua tatizo hilo zichukuliwe mapema kabla ya kuwa kubwa kama ilivyo Dar es Salaam. Mji wa Dodoma pia unakuwa kwa kasi sana na hivyo kupelekea ongezeko kubwa la magari. Ni vema mamlaka husika zianze kuboresha miundombinu ili kuzuia tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, maoni maalum ya Kamati. Miradi ya ujenzi wa barabara inaligharimu Taifa letu fedha nyingi sana. Kamati inashauri ujenzi wa barabara, hasa zinazojengwa kwa fedha za ndani, zijengwe na Wakandarasi wa ndani au Wakandarasi wa nje kwa kuingia ubia na Wakandarasi wa ndani. Uamuzi huu utasaidia kubakiza fedha zetu nchini na kuwapa uwezo Wakandarasi wa ndani pamoja na kuhawilisha teknolojia (*technology transfer*) kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa barabara za Wilaya zenye umuhimu kiuchumi ziendeleo kupandishwa hadhi ili zijengwe na *TANROADS* na zile ambazo ni za Wilaya lakini zimejengwa na *TANROADS* barabara hizo ziendeleo kusimamiwa na kukarabatiwa na mamlaka hii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Serikali imepanga kujenga nyumba 47 za viongozi na ghorofa moja lenye jumla ya makazi sita. Nyumba hizi zitajengwa katika Mikoa 12 nchini. Hata hivyo, kati ya nyumba hizo nyumba 28 na ghorofa hiyo zitajengwa Jijini Dar es Salaam wakati Dodoma zitajengwa nyumba mbili tu. Kwa kuwa azma ya Serikali ni kuhamia Dodoma Kamati inashauri nyumba za viongozi zisizendeleo kujengwa Dar es Salaam ili kutimiza azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Ili kuondoa tatizo la msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam. Kamati inashauri masuala ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam yasimamiwe na mamlaka moja itakayokuwa na mamlaka kamili kama ilivyokuwa mwaka 1996-2000, Jiji hilo lilivyosimamiwa na Tume ya Jiji la Dar es Salaam. Nchini Kenya kutokana na umuhimu wa jiji la Nairobi katika uchumi wa nchi hiyo, Serikali imeunda Wizara maalum kwa ajili ya kusimamia jiji hilo. Ni vema Serikali iangalie umuhimu wa Jiji la Dar es Salaam kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa bajeti inayoombwa na kupitishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii itolewe yote ili iweze kukamilisha kulipia miradi iliyotekelezwa kwa mujibu wa Mikataba baina ya Wizara na Wakandarasi kwani kutofanya hivyo kunasababisha Serikali iingie gharama ya kulipa riba na fidia kutokana na ucheleweshaji huo. Kwa mfano, katika mwaka wa 2010/2011, Serikali ilitenga sh. 710,945,105,000/= kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Mpaka kufikia Mei, 2011 426,939,525,000/= zilikuwa zimetolewa ambayo ni 60.05% ya bajeti iliyopitishwa.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Ili kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka 2011/2012, Wizara ya Ujenzi inaomba iidhiniwe jumla ya shilingi 1,496,417,233,000/=. Kati ya hizo sh. 245,440,294,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,250,976,939,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na kupitia kifungu kwa kifungu na kuipitisha na sasa inaliomba Bunge lako Tukufu kuyajadili na kuyapitisha maombi hayo ya fedha kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Nawashukuru pia Mheshimiwa Dokta John P. Magufuli, Waziri wa Ujenzi; Mheshimiwa Dokta Harrison G. Mwakyembe, Naibu Waziri wa Ujenzi; Balozi Herbert E. Mrango, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano, ushauri na utaalum wao ambao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha Taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa wa kupitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha Taarifa hii, ambayo kwa niaba yao naiwasilisha leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee napenda kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati ya Miundombinu, ambao ni:

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mwenyekiti; Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Saidi Amour Arfi, Mjumbe; Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba, Mjumbe; Mheshimiwa Herbet James Mtangi, Mjumbe; Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mjumbe; Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mjumbe; Mheshimiwa Inocent Edward Kalogeresi, Mjumbe; Mheshimiwa Kasikila Rosweeter Faustin, Mjumbe; Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mjumbe; Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mjumbe; Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machelemi, Mjumbe; Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mjumbe; Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, Mjumbe; Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mjumbe; Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema, Mjumbe; Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mjumbe; Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mjumbe; Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mjumbe; Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu Mjumbe; Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mjumbe; Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mjumbe; Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mjumbe; Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Mjumbe; Mheshimiwa Rukia M. Ahmed, Mjumbe; Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Mjumbe na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela K Kahigi, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dokta Thomas Didimu Kashillillah, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi pamoja na Katibu wa Kamati hii Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi kwa kuihudumia Kamati ya Miundombinu kwa ufanisi mkubwa na kuandaa taarifa hii kwa wakati. Nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba sasa kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. SALVATORY N. MACHEMLI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi kama wajibu wangu na kwa maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, pia nikushukuru wewe kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii kwa mujibu wa kanuni ya 99(7), ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wapiga kura wangu wa Jimbo la Ukerewe kwa imani yao kwangu. Ni dhahiri bila wao nisingefika hapa kwa kuwa pamoja na vitisho na mabomu ya machozi yaliyotawala siku ya kuhesabu na hata kutangaza matokeo ya kura bado wao walibaki na msimamo wa kulinda kura zao.

Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, kwa kuniamini na kunitewa kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi katika Wizara hii na pia Wabunge wenzangu wote wa kambi kwa ushirikiano wao kwangu.

Mheshimiwa Spika, sina budi kuishukuru sana familia yangu kwa ushirikiano mkubwa ambao imekuwa ikinipatia wakati wote ambao nimekuwa katika harakati za kutimiza wajibu wangu wa kuwatumikia wananchi wangu. Naomba waendeleo kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili anipe hekima katika kutimiza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Wizara ya Ujenzi. Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi na upembuzi hadi tarehe 31 Machi 2011 ilitolewa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) kuhusu Ukaguzi wa ufanisi ambao ni ukaguzi wa uwekevu, tija na ufanisi katika matumizi ya mkaguliwa wakati wa kutekeleza majukumu yake. Lengo la ukaguzi wa ufanisi ni kuboresha programu na utendaji ili huduma nzuri itolewe kwa wananchi kulingana na thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya ukaguzi wa ufanisi ilionesha kuwa pamoja na umuhimu na matumizi ya fedha yaliyooneshwa, sekta ya ujenzi wa barabara imethibitishwa, kupitia tafiti nyingi, kuwa na matatizo ya utendaji. Matatizo haya ni ya aina tatu. Tatizo la kwanza ni kazi za ujenzi kutokamilika katika muda uliopangwa hivyo kuchelewesha huduma za barabara kuwafikia wananchi. Tatizo lingine ni kuongezeka kwa gharama za ujenzi (nyongeza ya gharama za ujenzi ambayo ingeweza kuepukika). Tatizo la tatu ni kiwango cha chini cha ubora wa kazi ya barabara, linalopelekea barabara kuchakaa kwa haraka na hivyo kuhitaji matengenezo mapema kuliko ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huo ulibaini kwamba kazi ya usanifu haifanyiki vizuri na kusababisha kurudiwa mara kwa mara na kusababisha kuongezeka kwa gharama. Washauri hawakusimamiwa vizuri na walikuwa wanabeba majukumu mbalimbali yanayokinzana. Hakuna uchambuzi huru wa kuthibitisha utoshlevu wa maombi ya wakandarasi kuongezewa muda. Hakuna utaratibu wa ufuatiliaji wa washauri ambao wanahusika katika kusanifu na kusimamia kazi ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi uliendelea kueleza kuwa mfumo wa udhibiti wa ubora wa kazi haufanyi kazi vizuri. Ni wazi kuwa ukaguzi na tathmini zilizofanywa na Wizara/TANROADS hazikuweza kuzingatia baadhi ya udhaifu uliojitokeza katika kazi za barabara.

Aidha, adhabu zilizoainishwa katika mikataba hazikutumika vizuri kwa ajili ya kushughulikia na kufidia ongezeko la gharama, ucheleweshaji wa mara kwa mara wa ukamilishaji wa barabara na matatizo ya ubora wa barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, utekelezaji wa kazi za ujenzi wa barabara haukusimamiwa kwa kuzingatia udhibiti wa muda, gharama na ubora. Hii ina maana kwamba kazi ya ujenzi wa barabara kumi zilizokaguliwa haikufanyika kwa namna bora kwa maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, CAG katika ripoti yake alipendekeza pamoja na mambo mengine kuwa kuna hatua madhubuti za kuchukuliwa na Wizara kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Ujenzi na *TANROADS* wanapaswa kuboresha mchakato wa shughuli ya mwanzo katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi, kama vile kutimiza masharti ya mikopo na taratibu za manunuzi.

(ii) Wizara ya Ujenzi na *TANROADS* wanapaswa kuweka utaratibu wa kupitia na kurekebisha usanifu na makadirio ya miradi mara baada ya kuandaliwa na washauri na kabla ya ujenzi kuanza.

(iii) Wizara ya Ujenzi na *TANROADS* wanapaswa kuboresha usimamizi wa miradi na mfumo wa udhibiti wa ubora ili kuepuka ucheleweshaji, kuongezeka kwa gharama, na kulazimika kufanya matengenezo ya barabara muda mfupi tu baada ya kuanza kutumika.

Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu kuhusiana na masuala yafuatayo:-

(i) Wizara imechukua hatua gani katika kutekeleza ushauri huu wa *CAG*?

(ii) Je Wizara na Serikali imechukua hatua gani kuhusiana na mapendekezo ya *CAG* katika kuweza kuboresha ujenzi wa barabara zetu?

(iii) Je Wizara imechukua hatua gani dhidi ya utendaji dhaifu kama ulivyoainishwa kwenye ripoti ya *CAG* na hasa ikizingatiwa kuwa utendaji huu unakuwa na gharama kubwa sana katika ujenzi wa barabara zetu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Ni uhakika kwamba uchumi wa nchi yoyote ile duniani unategemea sana umadhubuti wa miundombinu wa nchi husika. Tanzania kama nchi nyingine duniani uchumi wetu unaweza kukua tu kama tutakuwa na miundombinu ya uhakika inayoweza kutoa huduma ya haraka kwa wahitaji, inayofika katika maeneo yote nchini na kutuunganisha na majirani zetu. Tanzania tumezungukwa na nchi ambazo hazina bandari kama Zambia, Uganda, Malawi, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, nchi hizi zina mizigo mingi sana inayohitaji kusafirishwa kwenda na kutoka nje ya nchi hizo. Lakini kutokana na ukosefu na udhaifu wa miundombinu ndani ya nchi yetu, Tanzania inakosa mabillioni ya dola za Kimarekani, kutokana na kutoweza kusafirisha mizigo hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sababu nilizozitaja hapo juu, pia inatokana na tabia ya watoa maamuzi wa nchi hii kuchelewa sana kutoa uamuzi na kutotoa kipaumbele kwa mambo ya maendeleo ya nchi. Ni vema Serikali izingatie kwamba biashara ni kulenga wakati (*Business is about timing*).

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina jumla ya barabara zenye urefu wa kilomita 86,472 na hizi zinajumuisha barabara kuu, za Mikoa, za Wilaya na za michepuo. Kati ya hizo kilomita 29,847 ndio zinasimamiwa na *TANROADS* na zilizobakia zinasimamiwa na Mamlaka za Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji.

Mheshimiwa Spika, miaka 50 sasa imepita tangu kupatikana kwa uhuru wa nchi hii, lakini tuna mtandao wa kilomita 6,320 tu za barabara nchini zilizojengwa kwa kiwango cha lami, sawa na kilomita. 126.4 kwa mwaka, ambayo ni sawa na asilimia 7.6% tu ya mtandao mzima wa barabara nchini.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kiwango kidogo sana kikilinganishwa na wastani wa takriban asilimia 13.3 kwa nchi za *SADC* na asilimia kati ya 30 na 35 kwa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara. Hii inamaanisha kwamba bado ipo haja kwa Serikali ya Tanzania kuongeza juhudi na kutoa kipaumbele maalum kwa ujenzi wa barabara nchini.

Mheshimiwa Spika, hali ya majirani zetu ambao tuliwasaidia katika vita ya kupata uhuru wao pamoja na kuwa wamepata uhuru nyuma yetu lakini wameweza kujenga barabara nyingi za lami kuliko sisi ambao tuliwatangulia, kwa mfano, Msumbiji 16.9%, Malawi 26.1%, Zambia 22.0%. Ni

dhahiri kuwa tunapaswa kuongeza kasi na kiwango cha fedha katika kuhakikisha kuwa barabara zetu zinajengwa ili kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliandaa mpango wa kujenga barabara wa kipindi cha miaka kumi (2007/2008- 2016/2017 *Transport Sector Investment Program (TSIP)*). Kwa awamu ya kwanza mpango huu ulikadiriwa kutumia dola za Kimarekani bilioni 6.2 (takriban trilion tisa za Kitanzania) (2007/2008 mpaka 2011/2012) .Ni dhahiri kuwa mpango huu kwa awamu ya kwanza ndio unafikia ukomo wake kwenye bajeti hii tuliyonayo.

Kambi ya Upinzani, tunataka kupata majibu kama lengo lililokusudiwa limefikiwa ama kulikuwa na ukomo wa bajeti katika kutekeleza mpango huu ili hatimaye sasa tuweze kuingia kwenye awamu ya pili. Pia tunataka kupata majibu ni kilomita ngapi za lami zilijengwa katika awamu ya kwanza na hawa ikizingatiwa kuwa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano umetenga kiasi cha shilingi trilion 6,793 kwa ajili ya kujenga kilomita 5,204.7 za lami hapa nchini (huu ni Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano uk.55) ambazo ni ndogo kuliko zilizotumika kwenye awamu ya mpango huu ambao unafikia ukomo wake kwenye mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ni asilimia 24 tu ya Watanzania wote wanaoishi vijijini, wanaishi kilomita mbili tu za barabara ambazo zinaweza kupitika kwa kipindi chote cha mwaka na hili linafanya usafirishaji wa mazao na bidhaa kutoka na kwenda vijijini hadi kwenye maghala yao kuwa adimu na hili ni tatizo kwa upande wa mijini linasababisha msongamano mkubwa wa magari huu ni Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano ukurasa 55.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2005-2010 kitakwimu ni kuwa Serikali iliweza kukamilisha miradi 15 kwa kiwango cha lami na hivyo kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 1,398.6. Kasi hii haitii matumaini hata kidogo kwani kwa mujibu wa ilani ya CCM kwa kipindi cha mwaka 2010-2015 Serikali imepanga kumalizia ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 1,140 (barabara tisa) ambazo ni miradi ambayo ilikuwa haikukamilika kwenye kipindi cha 2005/2010 na kuanza ujenzi mpya wa kilomita 5,282 kwa kipindi cha 2010-2015 (takwimu hizi ni kwa mujibu wa Ilani ya CCM 2010-2015). Takwimu hizi ni sawa na kusema kuwa Serikali itaweza kujenga kilomita 6,422 za lami katika kipindi cha miaka mitano.

Wakati huo huo Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaonyesha kuwa ni barabara zenye urefu wa kilomita 5,552 tu ndio zitaweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2011/2012-2015/2016).

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi hazijahusisha mpango wa Serikali wa kujenga barabara kwa viwango vya changarawe na zile za vijijini kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Kambi ya Upinzani tunasubiri kuona muujiza huu wa Serikali kujenga barabara zenye urefu mkubwa kuliko zilizojengwa tangu wakati wa uhuru yaani kwa kipindi cha miaka 50 ndani ya miaka mitano. Hasa ikizingatiwa kuwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita (2005-2010) Serikali hiyo iliweza kujenga kilomita 1,398.6 tu kwa kiwango cha lami, kwa kipindi hicho hii ni kwa mujibu wa (Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2010-2015 - Mafanikio katika Sekta ya Miundombinu" ukurasa wa 6). (*Makofi*)

Tunasema hivyo kwa sababu tunaona kuwa wananchi wanapewa matumaini makubwa ya miradi mingi ya barabara wakati fedha kwa ajili ya barabara hizo hazionekani kutengwa kwa ajili ya ujenzi huo. (*Makofi*)

Pili, kuhusiana na jumla ya kilomita za barabara ambazo zitajengwa kwa miaka mitano ijayo, kambi ya Upinzani, tunataka kupata majibu ni takwimu zipi zilizo sahihi. Ni za Ilani ya Uchaguzi ya CCM au ni za Mpango wa Taifa wa Maendeleo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Miradi maalum ya ujenzi wa barabara (kasma 4168).kitabu cha Miradi ya Maendeleo (sehemu-A juzuhu iv) katika fungu 98, kasma 4168 utaona kuwa mradi unaitwa "Miradi ya ujenzi wa barabara maalum" (*special road construction projects*) na fungu hili limetengewa kiasi kikubwa kuliko miradi mingine yoyote ya ujenzi wa barabara katika mwaka huu wa fedha kwani zipo jumla ya sh. 348,075,000,000/= na hizi zote ni fedha za ndani. Kwa hakika hizi ni fedha nyingi sana na hasa ikizingatiwa kuwa kitabu hicho kimeonesha miradi yote ya ujenzi wa

barabara ambayo itatekelezwa katika mwaka huu wa fedha, ila hii miradi maalum haijaoneshwa ni miradi ya barabara gani na zitajengwa wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kasma hii kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na 2010/2011 haikuwa imetengewa kiasi chochote cha fedha na ndio maana imetustua kuona mwaka huu fedha nyingi kiasi hicho zinatengwa kwa miradi isiyojulikana kuwa itajengwa wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia maelezo yaliyotolewa kwenye Kamati ya Bunge ya Miundombinu juu ya mpango na bajeti ya mwaka 2011/2012, kasma 4168 haipo kwenye randama na hakuna maelezo yoyote ambayo yametolewa kuhusiana na fedha hizo ambazo zimetengwa. (Makofi)

Kambi ya Upinzani, tunataka kupata maelezo ya kina ni miradi gani hii ambayo haiwezi kuandikwa na inatengewa fedha nyingi kiasi hicho? Kwani hii italiwezesha Bunge kuweza kupitisha bajeti inayoifahamu na kuisimamia Serikali kwa kuweza kufuatilia utekelezaji wa miradi husika.

Pili, fedha hizi zipangwe kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za kimkakati ambazo Kambi ya Upinzani imependekeza ili ziweze kuunganisha mikoa husika na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, *TANROADS* na madeni ya wakandarasi. Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la madeni ambayo Wakala wa Barabara (*TANROADS*) anadaiwa na hii ni kwa mujibu wa ripoti ya watathmini wa Jumuiya ya Ulaya ya mwaka 2011 mwezi Juni (*Mid term Evaluation of the Road Transport Sector Policy Support Programme for Tanzania*). Ripoti hii ilisema kuwa madeni yaliongezeka kutoka dola 30,000,000 hadi dola 300,000,000 kwa kipindi cha miezi tisa tu na kuwa hili ni jambo ambalo halikubaliki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2009/2010 ya *TANROADS*, madeni yaliyokuwepo kwa ajili ya wakandarasi na washauri waelekezi yalikuwa Shilingi milioni 43,183 au (US\$ 31.8m Juni, 2010) .

Mheshimiwa Spika, ripoti ya robo ya tatu ya mwaka ya tarehe 31 Disemba 2010, ilieleza kuwa wakandarasi walikuwa wanadai Serikali jumla ya shilingi milioni 321,581 (US\$224.9m) na malimbikizo ya madeni kwa ajili ya fidia ilikuwa jumla ya Shilingi milioni 49,605.

Mheshimiwa Spika, inashangaza sana kwamba Serikali ilipoulizwa na timu ya watathmini hawa wa Jumuiya ya Ulaya wakiongozwa na Mark Q WATSON na Christopher J FOLWELL iliweka kiwango cha juu zaidi cha madeni mpaka kufikia Shilingi bilioni 454.2 Desemba 2010 na kuwa mpaka tarehe 31 Machi 2011, Serikali ilikuwa imelipa kiasi cha Shilingi bilioni 242.8 kutoka kwenye fedha za Mfuko wa Barabara kutokana na Shilingi bilioni 266 zilizokuwa zimepitishwa kwenye bajeti ya 2010/2011 .

Mheshimiwa Spika, la kushangaza zaidi ni kuwa taarifa ya *TANROADS* inayoishia mwezi Machi, 2011 madeni waliyokuwa wanadaiwa na Wakandarasi pamoja na fidia kwenye miradi mbalimbali ya Barabara yalikuwa yamefikia kiasi cha Shilingi bilioni 446.47 (US\$297.6m), ongezeko la sawa na 38.8% katika robo hiyo ya mwaka na hii ina maana kuwa ongezeko hili la madeni lilikuwa ni kwa wastani wa US\$1m kila siku (takriban shilingi bilioni moja na nusu kila siku).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa *TANROADS* tarehe 19 May 2011, madeni yaliongezeka zaidi (*certified financial claims*) ya yalivyokuwa yameripotiwa kwenda Wizara ya Fedha mwezi Januari yalikuwa Shilingi bilioni 454, kiasi ambacho ni kikubwa kuliko kile kilichoripotiwa mwezi Machi. Kwa mujibu wa taarifa ya wataalam wa Jumuiya ya Ulaya, mpaka tarehe 18 Mei, madeni kwa wakandarasi na fidia ilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 289.095.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kutimiza wajibu wake kuhusiana na kiasi cha dola za Kimarekani milioni 74 kutoka mfuko wa *MCC* ambao jumla ya dola milioni 372 zimetengwa kwa ajili

ya miradi ya miundombinu. Ahadi hii ya Serikali imefikiwa wapi katika utekelezaji wake uko wapi?
(Makofi)

Kambi ya Upinzani inaona kuwa katika hali kama hii, ni dhahiri kuwa Wizara pamoja na TANROADS wameonesha udhaifu mkubwa sana. Narudia, Kambi ya Upinzani inaona kuwa katika hali kama hii, ni dhahiri kuwa Wizara pamoja na TANROADS wameonesha udhaifu mkubwa sana katika kuongoza kwani inawezekanaje kwa Serikali moja kutoa taarifa tofauti kila wanapohitajika? Tunataka kupata majibu, je, wakandarasi mpaka sasa wanaidai Serikali kiasi gani? (Makofi)

Pia, taarifa hii inaonyesha wazi kuwa, Wizara ilikuwa inasaini mikataba na Wakandarasi ilihali wakijua kabisa kuwa kuna ukomo wa bajeti na kuna madeni, hivyo, miradi mingi husainiwa bila kuonekana kuwa itaendelea kwa muda mrefu na hivyo wananchi kubakia wakiwa na matumaini hewa. Tunataka kujua ni utaratibu gani huwa unatumiwa na Wizara pamoja na TANROADS katika kuingia mikataba mbalimbali na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara zetu. (Makofi)

Kambi ya Upinzani inataka kujua, je, Wizara na Serikali imechukua hatua gani dhidi ya wale wote waliohusika katika kuingia mikataba hii wakati wakijua kuwa hakuna fedha zilizotengwa kwenye bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo? Kambi ya Upinzani inaona kuwa ni dhahiri kuwa Wizarani kumekosekana kwa mfumo wa umakini wa ufuatiliaji wa bajeti. Je, Serikali inakuja na mkakati gani katika kuhakikisha kuwa mfumo makini unawekwa katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, tunataka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali aifanyeie ukaguzi maalum TANROADS na hasa kwenye fedha za mwaka 2009/2010 ili kuweza kupata ukweli halisi wa taarifa hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Benki ya Dunia iliyoitwa *Transport sector support project NO. 53 152-TZ* ya tarehe 4 Mei, 2010 ilionesha kuwa Serikali ilikuwa imeingia mikataba na wakandarasi kwa ajili ya kujenga kilomita 1,200 zenye jumla ya US\$ bilioni moja na kuwa fedha zitaanza kutolewa mwaka huu wa fedha. Kambi ya Upinzani inahoji kama ripoti hii ya Benki ya Dunia ni sahihi. Je, bajeti hii imezingatia kwa kiasi gani miradi husika na je, ni miradi mipya mingapi itajengwa mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara inahusika pamoja na masuala mengine matengenezo ya kawaida ambayo ni yale yanayofanyika mara kwa mara yakihusisha kazi za kufyeka nyasi kandoni mwa barabara, kusafisha mifereji, kusafisha makalavati na madaraja, kurekebisha alama za barabarani, kuziba mashimo, kuziba nyufa kwenye lami, kupaka rangi kwenye barabara za lami na kuchonga barabara zisizo kuwa na lami.

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya muda maalum (*periodic maintenance*) ni yale yanayofanyika baada ya miaka kadhaa yakihusisha kazi za kurudishia upya tabaka la lami (miaka saba mpaka 14) au changarawe (miaka mitatu mpaka mitano).

Mheshimiwa Spika, ukarabati (*rehabilitation*), unahesabika kama kazi za maendeleo zikihusisha ujenzi mpya wa barabara baada ya kuachwa bila matengenezo ya mara kwa mara na ya muda maalum kiasi cha kuharibika kabisa. Kwa kawaida gharama zake ni mara tatu hadi nne ya gharama za matengenezo ya kawaida na muda maalum.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Barabara kwa mwaka wanakusanya kiasi cha zaidi ya dola 200 milioni na ni miongoni mwa mifuko mikubwa sana barani Afrika. Ila pamoja na Mfuko huu kukusanya fedha nyingi, takwimu zinaonesha kuwa Serikali za Mitaa, ambao wanasimamia asilimia 66 ya barabara wanapewa asilimia 30 tu ya mgao huu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine la ukarabati wa barabara ambazo zipo chini ya usimamizi wa Halmashauri za Miji na Majiji kwani kiwango cha pesa wanazopewa ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi na wingi wa barabara zilizopo na hivyo kusababisha foleni na msongamano mkubwa wa magari maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hii na ili tuweze kuendelea kukarabati na kujenga barabara na hasa za vijijini na mijini, Kambi ya Upinzani tunatoa mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, tubadilishe mfumo wa fomula ya mgawo wa fedha za Mfuko wa Barabara ili tuweze kuongeza fedha kwa ajili ya Halmashauri zetu na sasa uwe 60% badala 30 ya fedha zielekezwe kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara za vijijini ili kuweza kukuza uchumi wa vijijini.

Pili, kwa maeneo ya mijini fedha zinazopatikana kutokana na kodi ya majengo (*property tax*) asilimia 60% zielekezwe kwenye Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kujenga na kukarabati barabara za mijini ili tuweze kukabiliana na tatizo la foleni na msongamano mkubwa wa magari .

Tatu, Mfuko wa Bodi ya Barabara kwa kushirikiana na Halmashauri uweke utaratibu wa kufungua barabara za pembezoni mwa miji ili kuhakikisha kuwa tatizo la foleni linamalizika na kupunguza muda mwingi unaopotea kwa wafanyakazi na wanafunzi wa maeneo husika.

Nne, Serikali ifikirie kuanzisha Wakala wa Barabara za Vijijini katika kila Mkoa (*rural roads agency*) ili kuwa na jukumu la kisheria kujenga na kukarabati barabara za vijijini na kuondoa jukumu hilo katika mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii itaongeza ufanisi na utaalim na pia kupunguza kwa kiasi kikubwa gharama za ujenzi wa barabara badala ya sasa ambapo kila Halmashauri katika Mkoa inajijengea barabara bila kuwiana na mipango ya maendeleo ya mikoa. Ushauri huu unaimarisha *d by d* badala ya kuua kwani bado jukumu la Baraza la Madiwani litakuwepo lakini Wakala huu utafanya kazi chini ya Bodi ya Barabara ya Mkoa na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu misamaha ya kodi, mashangingi, posho na ujenzi wa barabara. Misamaha ya kodi inahusisha kiasi kikubwa cha fedha, kwa mfano, mwaka 2009/2010 peke yake, asilimia 2.3 ya pato la Taifa au TZS 695 bilioni zilitolewa kama misamaha ya kodi, mwaka 2008/2009 misamaha ilikuwa jumla ya Sh.752,398,800,000/=. Kiasi hiki ni zaidi ya nusu ya TZS 1.3 trilioni ambayo Serikali ilipanga kukopa kutoka taasisi za fedha za nchi za nje kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa miundo mbinu mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, hali hii ya kusamehe zaidi ya nusu ya pesa tunazokwenda kuomba huko nje sio dalili njema hata kidogo kwani inalifanya Taifa letu kupoteza ile heshima yake ya kuwa Taifa linalojitegemea na kuwa Taifa linaloomba omba na hivyo kupoteza ushawishi wake kwenye nyanja ya Kimataifa wakati tunawasamehe watu na Makampuni ya Madini. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kupunguza misamaha hii na fedha hizo ziweze kutumika kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu na hasa za vijijini ili tuweze kukuza kasi ya kukua kwa uchumi wetu na hivyo kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Serikali kuhakikisha kuwa viongozi na watendaji mbalimbali wa Serikali hawatumii mashangingi yanayouzwa kwa zaidi ya shilingi milioni mia mbili na sitini (260,000,000) kwa gari moja na ambayo yametengewa kiasi cha sh. 74,637,915,279/= kwa ajili ya kuyahudumia, (kwa ajili ya kununua mafuta, *oil* na vilainishi na kufanya matengenezo, (kasma 220300 na 230400). (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inaishauri Wizara iandae utaratibu madhubuti utakaowawezesha viongozi na watendaji kupata usafiri wa gharama nafuu badala ya utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia kwa wananchi. Katika kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara hapa nchini, nyumba nyingi za wananchi zimekuwa zikivunjwa na kusababisha wananchi hawa kuishi bila makazi ya uhakika na kusababisha malalamiko mengi miongoni mwa wananchi wetu. Pamoja na umuhimu wa kuwa na barabara kwa ajili ya kuweza kuharakisha upatikanaji wa maendeleo ya Taifa letu. Kambi ya Upinzani tunaishauri Serikali kuwa iachane na utaratibu wa kuvunja ama kubomoa nyumba za wananchi wakati bado haijawalipa fidia wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nyumba za Serikali, katika mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya shilingi 1,899,600,000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kujenga nyumba na kumalizia nyumba za watumishi mbalimbali wakiwemo Majaji. Pia zimetengwa kiasi cha sh. 949,800,000/= kwa ajili ya nyumba za *OCD, DSO, DAS*, na *DMO* katika Wilaya sita za Tanzania Bara. Pia zimetengwa 918,140,000 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mifumo ya ulinzi, uboreshaji wa mazingira pamoja na uzio kwa nyumba za viongozi zilizojengwa Mikocheni, Kijitonyama na Msasani *Peninsular Dar es Salaam*.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri Mkuu akihitimisha hoja yake ya bajeti alikataa ushauri uliotolewa na Kambi ya Upinzani kuwa Serikali itangaze Dodoma kuwa ni Jiji la Bunge na Elimu na iachane na mpango wa kuhamia Dodoma na alisema, nanukuu: "Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, 2010 hadi 2015 inafafanua kwa kina uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma.

Ibara ya 212 inasema, nanukuu: "Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010 – 2015) Chama cha Mapinduzi kitaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa Mpango thabiti wa kuhamia Dodoma hatua kwa hatua. Katika Mpango huo, Mpango Mji wa Dodoma (Master Plan) utazamwe upya ili kuhakikisha kuwa Majengo ya Serikali yanajengwa upya Chamwino kwa kuanzia na Majengo ya Ofisi na Makazi ya Rais (Ikulu).

(b) Kutunga Sheria ya kutambua Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi.

(c) Kuanzia sasa Majengo mapya ya Wizara za Serikali yajengwe Dodoma badala ya Dar es Salaam".

.....Kwa maelekezo haya ya Mheshimiwa Rais uamuzi wa kuhamia Dodoma hauna budi kutekelezwa. Kwa maana hiyo, hata kama fedha zimetengwa, napenda kuwahakikishia kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu itajengwa Dodoma. Aidha, Wizara zote ambazo zimetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi zianze kujenga Dodoma".

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya ya Waziri Mkuu na agizo la Rais pamoja na ukweli kuwa tamko lilishatolewa hapa Bungeni. Kambi ya Upinzani, tunataka kupata majibu ya maswali yafuatayo:-

(i) Je, ni kwa nini Wizara ya Ujenzi inaomba fedha kwa ajili ya kujenga nyumba 47 na kati ya hizo 28 zinajengwa Dar es Salaam wakati Dodoma zinajengwa nyumba mbili tu?

(ii) Kwa nini baadhi ya nyumba za viongozi zilizouzwa awali zisirejeshwe ili viongozi hawa waweze kupata nyumba za kukaa?

(iii) Ni Wilaya gani hizi ambako nyumba za *DSO, DAS, OCD*, na *DMO* zitajengwa?

(iv) Je, Serikali itahamia Dodoma wakati nyumba zao zipo Dar es Salaam ni kusema kuwa Wizara ina mpango wake na Waziri Mkuu ana mpango wake na huku agizo la Rais likielekeza vinginevyo na utekelezaji ukitekeleza vingine?

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za kimkakati. Hapo mwaka 2008 kwenye hotuba yetu tulishauri kuwe na mkakati mpya wa ujenzi wa miundombinu ya nchi. Hapa tungependa kushauri kwa upande wa barabara ili kuhakikisha mkakati mpya unaoweza kurejesha gharama za ujenzi baada ya muda mfupi. Mkakati mpya uzingatie kuunganisha mikoa ifuatayo kama hatua ya haraka kwa barabara za lami.

(a) Mkoa wa Mbeya na Mwanza kwa maana ya barabara ya Chunya -Tabora – Mwanza.

(b) Mkoa wa Mbeya na Kigoma kwa maana ya barabara ya Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma.

(c) Mkoa wa Mtwara na Ruvuma kwa maana ya barabara ya Mtwara – Tunduru – Songea – Mbamba Bay.

(d) Mkoa wa Arusha na Iringa kwa Maana ya barabara ya Arusha – Babati – Kondoa – Dodoma – Iringa.

(e) Mkoa wa Kigoma na Dar es Salaam kwa maana ya barabara ya Dodoma – Manyoni – Itigi – Tabora – Urambo – Kigoma.

Mheshimiwa Spika, barabara hizo nilizozitaja ni za kimkakati kiuchumi. Mkopo wowote utakaochukuliwa kwa ajili ya barabara hizi unaweza kulipika kwa muda wa miaka 20 mpaka 30 na mkopo unaokubalika kwani utachochea ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kuongeza shughuli za kiuchumi na hivyo kupelekea nchi kupiga hatua na kutumia vizuri fursa ya kijiografia.

Mheshimiwa Spika, Daraja la Kigamboni ni suala linalotajwatajwa kila mwaka. Tunaomba Waziri wa Ujenzi alieleze Bunge hili ni lini tutaacha kusema na kutenda kuhusiana na suala hili. Hali hii inathibitishwa na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya mradi huo mwaka huu wa fedha kwani kwenye kitabu cha maendeleo (Juzuu iv) zimetengwa kiasi cha sh. 316,600,000/= (kasma 4167). Pamoja na kuwepo taarifa kuwa daraja hili litajengwa na *NSSF* kama ambavyo Bunge limekuwa likielezwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu kuhusu fedha hizi ni kwa ajili ya kufanya kazi gani? Kwani itakumbukwa kuwa Serikali ilishawasilisha taarifa kuwa upembuzi yakinifu ulishakamilika, sasa hizi ni fedha kwa ajili ya kujenga daraja hilo? Ama Serikali inatoa kauli gani kuhusu daraja hili kwa wananchi, hasa waishio Kigamboni, ambao wamekuwa wakipewa matumaini kila mwaka kuwa daraja litajengwa? Kuna kigugumizi gani katika kutekeleza ujenzi wa mradi huu ambao umekuwa ukisemwa miaka nenda miaka rudi? Kama *NSSF* wanayo fedha iliyobaki itapatikana lini?

Mheshimiwa Spika, *TEMESA* ni chombo muhimu sana katika kuongeza pato la Serikali. Ili Wakala huyu aweze kuwa endelevu, lazima viongozi wake na hata Serikali kwa ujumla wake wabadili fikra na kufanya kazi kwa misingi ya kibiashara katika soko huria na kuepukana na kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, *TEMESA* inadai fedha nyingi kutoka kwa Mashirika, Wizara na taasisi mbalimbali hapa nchini. Kutokana na madeni hayo, chombo hiki cha uwakala kitashindwa kabisa kujiendesha. Tunaitaka *TEMESA* iache kutoa huduma kwa wadaiwa sugu mpaka walipe madeni yao kwanza. Wale wote ambao wanataka huduma, ama walipe kwanza au mara tu baada ya kupata huduma wasiondoke na chombo husika mpaka walipe gharama za matengenezo yake.

Mheshimiwa Spika, kuna Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali ambazo zimekuwa zikitengenezesha magari katika karakana binafsi. Kwa mujibu wa ripoti ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya 2009/2010, matengenezo ya magari ambayo hayakupitia *TEMESA* yaligharimu kiasi cha sh.176,722,089/= ikiwa ni matengenezo ya magari katika karakana binafsi bila kupitia Karakana Kuu ya Serikali. Mkaguzi na Mdhidhi Mkuu alishauri taasisi za Serikali kuzingatia kanuni namba 59(1) na (2) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 kwa kuhakikisha kuwa matengenezo ya magari lazima yaidhinishwe na Wakala wa Ufundi, Umeme na Mitambo (*TEMESA*) kabla na baada ya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, ni vema *TEMESA* wajifunze kutoka kwa wenzao *Toyota* wajue ni kwa namna gani wanavyokusanya madeni yao. Pamoja na kupata uelewa huo, njia nyingine ambayo inaweza kuwasaidia kukusanya madeni yao ni kumwajiri Wakala wa kukusanya madeni sugu, mpango ambao unatumia na taasisi nyingi katika kukabiliana na wadeni sugu.

Mheshimwa Spika, kwa kuwa Wakala *TEMESA* wanao wataalam wa kutosha, hapana budi kufanya uchambuzi wa kazi zao ili wapate dira madhubuti inayoeleweka, kadhalika Serikali iwapatie fedha za kutosha ili Wakala waweze kutekeleza majukumu yao kama wanavyopanga.

Mheshimiwa Spika, suala la kukaimu nafasi za uongozi ndani ya Wakala ni vema lifikie kikomo ili kuongeza kiwango cha ufanisi na uwajibikaji. Wale ambao wanakaimu na wenye sifa na uwezo ni vema wathibitishwe ili washike dhamana zao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatekeleza wajibu wake wa kidemokrasia wa kutoa maoni na hoja ili Kambi ya chama kinachotawala ifanyie kazi kwa maslahi ya Taifa. Nawatahadharisha wenzetu kuwa hali ya kisiasa ya nchi imebadilika sana na kwa kasi. Iwapo walio na Serikali watahindwa kutekeleza mabadiliko muhimu ya kisera ili kuendana na upepo wa mabadiliko ya kiuchumi, wananchi watawapumzisha. Sisi tunasubiri tupewe ridhaa na wananchi ili tutekeleze mipango hii ambayo wenzetu mmeshindwa kutekeleza. Mawazo mbadala tunayo, nguvu ya kutekeleza mawazo haya tunayo na tunaweza!

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Ndio wajibu wa Kambi ya Upinzani na ndio wajibu wa Kambi Tawala. Basi mfanye kazi mtoe maoni yaliyo sahihi kwa wananchi ili waweze kuelewa.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana wasemaji wa mwanzo, Mtoa Hoja, Wasemaji wa Kambi ya Upinzani na Kamati inayohusika. Sasa tunao wachangiaji hapa, kuna wale wachangiaji ambao hawajawahi kuchangia kabisa humu ndani, nao ni Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa Rosemary Kirigini.

Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Abia Nyabakari.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda niwashukuru wananchi wa Mkoa wa Rukwa na hasa akinamama walionifanya kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Si hivyo tu, napenda nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutupatia barabara Wanarukwa ya kutoka Tunduma mpaka Kasanga. Pia siachi kumpongeza, huwa namwita Nahodha, Jemadari na aliye hodari katika kundi, Mheshimiwa John Magufuli. Nampenda sana kwa sababu ni mchapa kazi, inapobidi kulala huko anafanya kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwasahau Wahandisi wa Mkoa wa Rukwa, Meneja wa *TANROAD* pamoja na kikosi chake chote; kufuatana na mmomonyoko wa udongo ulioko Rukwa, usiku na mchana huwa wanakesha wakati wa masika wakitengeneza madaraja na barabara. Pamoja na kuwa tumepewa barabara ya lami katika Mkoa wa Rukwa, lakini bado barabara ni mgogoro katika Mkoa wa Rukwa. Kweli, barabara hiyo ya lami inakuja lakini viunganishi hatuna vitakavyoweza kuifikia ile barabara ya lami ili iweze kutumika vizuri kama Serikali ilivyolenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Rukwa, kuna barabara moja inaitwa Karambanzite inayokwenda Ilemba, kilometa 24 kutoka hiyo barabara ya lami. Barabara ile ni ngumu kuweza kutengenezwa na Halmashauri, yaani inahitaji pesa nyingi. Ni kilima cha ajabu, wengine huwa tunakiita *slaughtering place!* Watu wanafia pale kila kukicha! Siku moja gari la kwanza lilipanda, likaanguka chini! Gari la pili lilipopanda, likaanguka chini! Gari la tatu lilipopanda, likaanguka! Siku moja magari matatu! Lakini Serikali imekaa kimya ikiangalia! Ni mabonde, yaani kile kilima kina mawe, kina mashimo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kipindi kimoja hata Mheshimiwa Waziri alipokuwa akija kutembelea kule chini, hakuweza kupita kile kibarabara, aliogopa. Kilometa 24 akaamua kuzunguka kupitia Chonga, kilometa 150! Ni mtu mmoja tu aliyethubutu kupita barabara hiyo, Rais

Benjamin Mkapa na alipofika kule watu walifanya sherehe kubwa kukutana na mpendwa wao Rais! Hakuna mtu mwingine aliyekwenda kule! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba barabara hii iwekwe mikononi mwa Serikali. Nitaeleza ni kwa nini naomba barabara hii. Moja, barabara ile ni kiunganishi cha watu kutoka Kipeta, kutoka Mto Wiso, ndio karibu kwa kupitia kuja Sumbawanga. Huwezi ukamwambia mtu wa Kipeta, azunguke mpaka Mto Wiso mpaka Muze, ndio apande kwenda Sumbawanga Mjini, ni kitu ambacho hakiwezekani! (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Machali, sio sahihi ulichokifanya.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba barabara hii ikichukuliwa na mikono ya *TANROADS* kwanza kabisa pia nitaomba iwekewe lami. Kwa nini naiombea barabara hii iwe barabara ya lami! Moja, asili ya udongo wa Mkoa wa Rukwa, ni wa mmomonyoko, kwa hiyo, hata wakitengeneza barabara kiasi gani lazima barabara zitaendelea tu kuharibika. Mbili, kilima kile cha Karambanzite ni sehemu ya kifo! Angalau kiwekewe lami kama vile Kaburiwazi walivyofanya. Kuna Kaburiwazi kuna *slaughtering place!* Watuwekee angalau zege kama itakuwa imeshindikana kuchukuliwa, Serikali itengeneze na kisha iirudishe mikononi mwa Halmashauri. Kuipa ile barabara Halmashauri, ni kuitwiga mzigo mkubwa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Rukwa, kama mnavyojua, watu wote wa Ukanda ule ni wakulima. Wanalima mipunga na hata hivi mnavyoonona mpunga unaletwa huku mnasema umetoka Mbeya! Mwingi umetoka Bonde la Rukwa, ni wakulima wa mahindi, hiyo ni sababu ya tatu. Ya nne, mkiweka barabara hii ya lami itaunganisha Mkoa wa Katavi kuanzia Stalike mpaka Mkoa huu wa Rukwa, halafu ni vijiji vingi vinavyopitia pale. Si hivyo tu, itakuwa ni njia ya mkato kwa watalii kwenda kuangalia viboko, mamba katika Ziwa Rukwa! Kuna viboko wengi kuna mamba wengi, ukifika pale utaona maajabu. Kwa hiyo, hicho kitakuwa ni kivutio kimoja kwa watalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ni bado tuna mbuga za wanyama Katavi, ni lazima watalii wafike pale kwa kupitia barabara wanayoitaka. Hii ni njia ndefu ambayo inaunganisha watu. Halafu vilevile ile njia inawapeleka watu kwenda kuchimba dhahabu na si hivyo tu, kule walimu hawawezi kwenda kwa sababu, hakuna barabara ya kuwapeleka kuchukua mishahara! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuliangalie hili sasa katika Mkoa wa Rukwa kwamba, hii barabara inatakiwa kuangaliwa. Pamoja na kusema Mheshimiwa Magufuli, terehe 22 Julai, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mipata, alisema kwamba, Serikali imetoa bilioni 600 kwa ajili ya utengenezaji wa barabara mkoani Rukwa, hatuwezi kujenga tena barabara za Rukwa! Msema kweli ni mpenzi wa Mungu, labda baadaye! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali hii hii ndio imetucheleweshwa miaka 50 bila kutuletea barabara ya lami! Halafu inasema hatuwezi tena kuahidi barabara ya lami! Ni haki yetu ya msingi kudai barabara za lami! Tunahitaji viunganisho, sisi ni wakulima stadi katika Mkoa wa Rukwa. Katika mikoa yote ya Tanzania, wamelima wamepata tani 12,810,000 lakini sisi peke yetu tulilima tani 2,000,000! Ulaji wetu, tani 300,000 tunailisha hii Serikalii! Kwa nini, itunyime barabara za lami? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima mfikie mahali mrudi nyuma mwangalie. Boi anayekufanyia kazi unatakiwa kumheshimu, sisi tumekuwa maboi tusiokuwa na malipo! Hiki chakula tunachokilima bado kinatolewa ushuru, unaendeleza kwingine, kwa nini? Sisi tuendeleze kuwa maskini! Hatuwezi kupata walimu Mkoa wa Rukwa, kwa sababu hakuna barabara zinazowaleta huku! Hatuwezi kuwa na umeme kwa sababu, hatuna barabara! Hatuwezi kuondoa ujinga na maradhi tukafuta kwa sababu hatutapata waganga na walimu wa kwenda huko vijijini! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba barabara hii iwekewe lami kama kiunganishi kikubwa. Kuna barabara nyingine kutoka Legeza Mwendu kupita Mwambekeya, Urumi, Mwindi, Katavi, Mwazi, Ilula na Kaingesa, naomba pia barabara hii ni ndefu mno! Inakusanya vijiji vingi ambavyo viko

huko nyuma, watu wanatoka sehemu za mbali jamani! Mkifika Rukwa, mtaona watu wamekuja na Lori! Yaani ukiwaangalia, mpaka Mzungu anashangaa! Wazungu gani hawa! Wametoka wapi? Meno ni vumbi! Uso, yaani macho mekundu! Wangekuwa Mwanza, wangekuwa wanachomwa moto! Sababu ya miundombinu iliyo mibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna barabara pia ya kutoka Nkundi inapita Kate kwenda Wampembe, Serikali yako imetengeneza barabara imechepuka pale kwenda Namanyere! Naomba barabara hii inayoshuka pale Wampembe, angalau ichukuliwe na *TANROADS*, kuna kilima kikali jamani, sisi watu wa Rukwa hatutaendelea kama *TANROADS* haitachukua barabara ili tuweze kusafirisha mazao yetu yaende kuuzwa mahali husika. Jambo hili halitufurahishi sisi watu wa Rukwa, tunakaa kilometa 100, kilometa 120, hatuwezi kula samaki waliotoka katika Ziwa Rukwa! Wanafika saa nane, samaki wamesharibika! Inzi wa chooni ndio wanaruka pale! Na mtu anayepeleka wakati mwingine gari kule, anakwenda kusema sasa ni mswalie Mtume, wakati mwingine wanamwaga sababu ya barabara zilivyo mbaya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wa Rukwa hatuwezi kuendelea. Mtu anaingia baharini anakutana na miundombinu mibaya ya majini, vifua vilishatanuka utafikiri tembo, unakuta anafika nchi kavu anauza samaki kumi kama mkono wangu 500/=! Huyu mtu atasomesheje mtoto? Ataendeleaje? Shida kwetu! Umeme shida! Hatutegemei kupata umeme watu wa Rukwa katika maisha yetu! Serikali ituambie ili tujenge fikra za kujitegemea. Haiwezekaniki sisi tulime, tunatoa tani, watu wamekaa maofisini wanakula, sisi tunalima, halafu wasitutengenezee barabara! Kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri mngeangalia. Mkoa wa Rukwa, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Mheshimiwa Spika, hata ungetoka uwanja wa ndege kwenda pale tu kilometa kama kumi kwenda Wipanga, hakuna barabara! Ukienda na pikipiki utarudi umebeba kichwani! Kilometa 10! Kuna watu Mkoa wa Rukwa, hawajui hata barabara ni nini? Ukienda kwa mfano Nondo, sehemu za Kasanga, hakuna barabara! Hakuna daraja! Kwenda jirani, kilometa moja! Lakini hakuna daraja! Kwenda huku, mtu analazimika kutembea kwa mguu! Yaani kilometa 30 kwenda kupata matitabu! Halafu mnasema hatuwezi kuendelea kuweka barabara! Ni muda muafaka, miaka 50 hatuambiri! Tunahitaji barabara za lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuipongeza Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano siwezi kuipongeza kwa sababu hata barabara tuliyopata, Mheshimiwa Rais Kikwete mkombozi, asingetamka tusingewekewa hiyo barabara! Naomba msiweke vicingi kwa watu wa Rukwa, wanafanya kazi ngumu! Wanaishi katika mazingira magumu! Punda kama anakubebea mizigo, usimpige hovyoy! Watu wa Rukwa, hatuwezi kuishi kwa kubeba mizigo kutoka Rukwa, kuipeleka mpaka Sumbawanga, kwa punda jamani, tukapata maendeleo! Tukajenga nyumba, na sisi tunahitaji kujenga majumba ya ghorofa na sisi tunahitaji umeme na sisi tunahitaji maji, tutayapataje bila barabara kuja? Tutawezaje kulipia huu umeme na maji kama hamkuanza kututengenezea barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaambie ndugu zangu, nina sababu nyingi za kuweza kudai barabara za lami, moja, Mkoa wa Rukwa una aina ya udongo wa mmomonyoko! Mbili, sisi ni wakulima stadi! Tatu, vifo vinatokea kwa watu! Nne, akinamama hawapati matibabu mahali husika kwa muda muafaka wanapokuwa na mimba, wanapoteza maisha yao na watoto! Si hivyo tu, sisi ni wavuvi, Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika na bado tuna samaki wa mapambo na tena siku nyingine nitauliza watuambie, wale samaki wanaovuliwa Rukwa wa mapambo, tunabaki na kitu gani sisi pale Sumbawanga? Hivi wako Katavi wanavua! Na si hivyo tu, sisi tuna *Kalambo Falls!* Tunahitaji watalii waje kuangalia hilo shimo la ajabu, waje pale kwetu na sisi. Sisi ni wachimba madini ya vito na dhahabu! Ni kwa nini sisi tusipate wawekezaji? *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, nafikiri...

SPIKA: Asante, tumesikia. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Zabein Mhita na Mheshimiwa Andrew Chenge, ajiandae.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Subhanah Wataala, kunijalia afya njema na kuweza kuwa hapa leo na kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Naanza kwa kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ama kwa hakika alitakalo Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala*, ni *Kun-Faya-Kun*, kuwa na linakuwa, ndio Rais, narudia *Kun-Faya-Kun*, kuwa na linakuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha naomba niwapongeze Viongozi wote waliochaguliwa katika nafasi mbalimbali. Nitakuwa mwizi wa fadhila iwapo sitawashukuru wananchi wa Jimbo la Kondo la Kaskazini, ambao walinichagua kwa kura nyingi, kwa kura za kishindo. Kwao nawaambia, *Jazakallah kheiri* na *Inshallah*, nitaendelea kuwatumikia kwa uwezo wangu wote kama ilivyo kawaida yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa bajeti nzuri waliyoandaa na bajeti ya kisayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza kuunga mkono hoja. Nimekuwa nikichangia katika Bunge hili kuhusiana na barabara ya kutoka Dodoma kwenda Babati, kujengwa kwa kiwango cha lami kwa miaka mingi. Lakini sasa angalau naanza kuona mwanga... *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Kombo, sio unavyotakiwa. Kanuni inakuambia usikatishe kati ya Msemaji na Spika! Angalia uliko wewe, unachokifanya sasa! Msemaji yuko wapi na mimi niko wapi? Sasa rudi nyuma, unarudi ulikotoka.

Haya, Mheshimiwa Mhita, endelea.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Angalau tumeanza kuona mwanga katika ujenzi wa barabara hii ya kutoka Dodoma kwenda Babati. Ni jana tu nimepita kuikagua barabara hii kama ilivyo kawaida yangu, lakini kwa kweli nimeona kazi imeanza. Barabara hii imeanza kujengwa kutokea pale Mzakwe kuelekea Mayamaya. Nimeona mwenyewe barabara ya mchepuo imeshaanza kujengwa. Nimeona barabara yenyewe imeanza kutifuliwa. Sasa nasema kwa kweli, naona mwanga mbele yangu baada ya ahadi za miaka mingi. Naamini hata wananchi wa Jimbo la Kondo la, wameshaanza kupata faraja. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imepata Waziri, Wizara imepata Naibu Waziri. Vilevile barabara ya kutoka Babati kwenda Bonga, nayo pia imeanza kutengenezwa, hiyo ni faraja, tunashukuru sana sana. Kutoka Dodoma mpaka Mayamaya na kutoka Babati mpaka Bonga jumla ni kilomita 62.25 sina tatizo hapo, kwa sababu wakandarasi wapo kazini na pesa imetengwa, Mungu atupe nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo lipo kutoka Mayamaya kwenda Bonga kilomita 198, nimeangalia katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kilomita hizi 198 hazikutengewa pesa, kilomita hizi hazina mkandarasi. Sasa nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli wakati anapohitimisha hotuba yake, sehemu hii iliyobaki pesa zake zitatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipande hiki ambacho kimebaki ndiyo kipande ambacho kipo katika Jimbo la Kondo la Kaskazini, lakini bado nafarijika kwamba fedha itatengwa, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri naomba mnipe kauli na wananchi wa Jimbo la Kondo waone vipi barabara hii itakamilika. Lakini vilevile kuna kipande cha barabara kutoka Bicha kwenda Kondo la Mjini tulishaahidiwa kwamba pesa ipo na mkandarasi amekwishapatikana. Kipande kile sijaona chochote kinachofanyika, nimepita kule sijaona mambo ambayo nimeyaona kutoka Dodoma kwenda Mayamaya, wala mambo niliyoyaona kutoka Babati kwenda Bonga, Bichi kwenda Kondo la hakuna kitu.

Mheshimiwa Spika, nitaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana *wind up* anifahamisha je, kipande kile mpango wake ukoje? Kuna barabara inatoka Katesh katika wilaya ya Hanang, Katesh mpaka Kondoa barabara hii kutoka Katesh mpaka Mtiryangwi imekwishachukuliwa na *TANROADS*, mpaka kutoka Mtiryangwi kuja Kondoa.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa katika kikao cha bodi ya barabara tuliambiwa kwamba sehemu ya kutoka Mtiryangwi kuja Kondoa nayo pia Serikali imekubali, imeinuliwa na itakuwa inahudumiwa na *TANROADS*. Lakini sijaona pesa yake, je barabara hii nayo hatma yake nini, nitamuomba Mheshimiwa Waziri anapokuwa ana *wind up* atueleze kusudi tuendelee kupata faraja, na mimi kidogo nipumzike kwenda kwenye ofisi zao maana kuna wakati wafanyakazi walifikiri mimi ni mfanyakazi wa Wizara ile, kumbe mimi nakwenda kuwafuata Waheshimiwa Mawaziri kuzungumzia kuhusu barabara yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile mwaka jana wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, alipokuwa akitokea Galapo wilaya ya Babati Vijijini alipofika Hurui alitoa ahadi kwamba barabara ya kutoka Galapo kupita Huruhi mpaka Ntundwa, nayo pia itachukuliwa na kuhudumiwa na *TANROADS*. Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anapofanya majumuisho atueleze je, barabara ile nayo hatma yake nini, ni barabara muhimu sana kama zilivyo barabara nyingine ambazo nimezungumzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafahamu kengele ya kwanza imegonga na nisingependa nigongewe kengele ya pili, kwa kumaliza nachukua nafasi hii kuwatakia Watanzania wote heri ya Mfungo Mtukufu wa mwezi wa Ramadhani na kuwaomba *maghufira* kwa Mwenyezi Mungu *Inshallah*. Kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunitambua, nimshukuru Waziri Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa hotuba nzuri sana na niwashukuru sana, nimshukuru msaidizi wake Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Katibu Mkuu Balozi Mrango, Msaidizi wake *Engineer* Nduguru na timu yote ya Wizara na upande wa *TANROADS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina kila sababu ya kujivunia mafanikio ambayo tunayaona hivi sasa kwa kufungua nchi yetu, nimesafiri sana katika nchi hii na bahati mbaya wale wanaosema hakuna kinachofanyika mimi ninaamini kwa sababu hawapati nafasi ya kutembea sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumefungua sasa Ukanda wa Kusini, tukimaliza sehemu ya Ndundu - Somanga, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri mwenyewe kipindi kile unatoka na *taxi*, Mtwara kuelekea mpaka Mtukula. Tuna kazi kubwa ya kufanya, pesa ni kidogo lakini niwashukuru pia washirika wetu wa maendeleo kwa jinsi walivyotusaidia na kutuamini na Serikali naiomba itambue hilo, lakini pia niombe Serikali tuna pesa nyingi zipo nje tukitaka kuishirikisha *private sector* na nafasi tunayo na barabara hizi ambazo zinafunguka sasa ni sehemu kubwa sana katika chachu ya maendeleo ya uchumi wetu na ndiyo maana naishukuru Serikali kwa kuunganisha nchi yetu kwa barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami na nchi jirani nane hizi. Naomba sana sehemu ya Mangaka - Mtambaswala kwenda Daraja la Uhuru kwenda Mueda upande wa Mozambique tuhangaie, tutafute pesa kwa barabara hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kazi inayofanyika kwa upande wa Kaskazini Mashariki, sehemu ya Tanga, Horohoro, Lungalunga kwenda mpaka Malindi Kenya. Tuna sababu zetu kwa nini tunafanya hivyo ni kufungua ukanda huu wote. Lakini nataka pia tuhangaie barabara ya Tanga, Pangani tunakuja mpaka Bagamoyo kupitia Saadani. Yote hayo ukiunganisha mpaka Msata unafanya kazi ya uhakika katika kufungua ukanda huo. Lakini pia tufanye jitihada kwa upande wa Arusha, Holili hadi Voi tuna sababu zetu tukiyafanya haya tutaona ukanda huo tunakuwa tumemaliza. Lakini pia kwa upande wa Kusini *Mtwara corridor* hivyo tujitahidi sehemu ya kutoka sasa kutoka Mbinga kwenda Mbambabay, itakuwa tumemaliza kazi ya huko.

Mheshimiwa Spika, upande wa Magharibi kule kazi nzuri inafanyika hongereni sana lakini tujitahidi sana kwa barabara hii inayotoka Mbeya, kuja Chunya Makongorosi mpaka Ipole, Sikonge, Tabora, Nzega unaunganisha na hii barabara inayotoka Dar es Salaam kwenda Mwanza mpaka Mtukura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba sana Serikali, mimi nashukuru kwamba barabara ya kutoka Lamadi, Bariadi, Maswa, Mwigumbi inajengwa kwa kiwango cha lami, utajiri wa sehemu hiyo upo katika maeneo hayo. Lakini sioni sababu ya barabara ya kilomita 171 ijengwe kwa miaka kumi. Ningependa sehemu ya Mwigumbi kuja Maswa kilomita 50 mwaka kesho tuiweke kwenye Bajeti na ile ya sehemu ya Maswa kwenda Bariadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona *activities* kubwa zinazofanyika, lakini barabara nyingine ambayo mimi nasema lazima tufanye kila linalowezekana kwa sababu pesa za *private sector* zipo tuiseme tu kwamba tunaipenda *private sector* lakini hatuonekani kwenda kushirikiana nayo. Hii barabara ya kutoka Kigoma Kidakhwe kwenda Kasulu, Kibondo mpaka Nyakanazi, tumeanza na Nyakanazi kuja sehemu ya Kibondo, sawa lakini tunaweza tukafanya kwa uharaka zaidi ya hapo kwa kutokutegemea pesa za Serikali ili tuweze kumaliza kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukishatoka pale tumeanza vizuri tu kutoka Tunduma, Ikana pale unakuja Laela Sumbawanga tunaona vitabu vinasema vyenyewe lakini unataka sasa ukifika Sumbawanga kuja Mpanda kupitia Chizi, Kibaoni na Sitalike iwe sehemu ya kutoka Mpanda kwenda Kigoma kupitia Uvinza na Kidakhwe mimi naomba sana Serikali tuone uwezekano wa kushirikisha *private sector*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1997 Mheshimiwa Waziri alikuwa Naibu Waziri katika Wizara hii, nashukuru Rais imempendeza amekurejesha tena sasa kama Waziri pale. Ukiangalia mkoa wa Shinyanga ulivyokaa, utadhani mtu amelala. Miguu iko upande wa Magharibi yaani ni Kigoma na Kagera, makalio yako Tabora na sehemu ya mgongo na shingo vipo upande wa Singida na Arusha, halafu huku Mara na Mwanza tumbo lipo Mwanza ni eneo kubwa kweli hili lakini kipindi kile Serikali ilikuwa na mawazo mazuri sana ya kusema hebu tufungue barabara hii unatoka pale *Odean junction* unakuja Mang'ola, Matala, unakuja nayo mpaka Bukundi, unaingia Mwanuhuzi, Mwanuhuzi unaondoka unaenda Kishapu, Mhuze, Kishapu mpaka Kolandoto. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, *actually* mwaka 2008/2009 nakumbuka tulikuwa tunafanya kazi ya upembuzi yakinifu kwa sehemu ya Kolandoto kuja mpaka Mwanuhuzi. Sasa sioni kabisa tangu mwaka jana. Sasa hawa wajanja wajanja wametoka wapi ambao wamesema sehemu hiyo haifai tena kuendeleza katika ujenzi wa kiwango cha lami. Ningependa nipate maelezo, Kolandoto mpaka Mwanuhuzi kupitia Lalagwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine sasa hivi tunakuja na tunaanzisha maeneo mapya ya utawala. Shimiya inakuwa mkoa mpya. Kuna barabara hii kutoka Mwanuhuzi ukishafanya haya ambayo nimeyasema leo ambayo yalikuwepo katika mipango ya Serikali tangu zamani, sasa hivi unaweza ukatoka pale Mwanuhuzi ukaenda Kisesa kwa Mheshimiwa Mpina, ukaenda Gambasingi, kwa Mheshimiwa John Cheyo, unakuja Bariadi, unateremka unaenda Ngulyati, Kasoli, unaenda Salama pale kwa Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, unaingia Magu. Kwa hiyo, umefungua sehemu hiyo kuanzia upande wa Arusha kwa rafiki yangu Mheshimiwa Mustapha Akunaay, ukanda wote wa utajiri ule na ndiyo maana ya barabara hizi tunazojenga zina sababu zake siyo tu kuunganisha makao yetu ya mkoa kwa ...lakini tunazifungua barabara hizi kwa sababu ya uchumi na kwa faida ya maendeleo ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimelisema hilo kwa sababu ningependa Waziri atueleze kwa nini *concept* iliyokuwepo mwaka 1997 imekuja kuminywa minywa. Lakini mimi nasema tukirudi kwa utaratibu huo tutakuwa tumefungua tena hayo maeneo kama tulivyofanya kwa maeneo mengine. Lakini lipo eneo hili lingine kutoka Nyamuswa hapa unakuja mpaka Bunda, unaenda Kisorya mpaka Ukerewe na hii barabara ni muhimu sana kwa ukanda huo, mimi nasema tuyafanye haya kwa faida ya kuonekana kwamba tunafanya kazi kwa faida ya Taifa na hakuna eneo nasema wao wamesahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini twende mwaka kesho kweli tuone hii barabara ya kutoka makutano kwenda Nata - Mgumu - Fotikoma, uje mpaka Loliondo kuja mpaka Mto wa Mbu kweli tuonekana kwamba tumefanya, tuiseme kwamba tumefanya usanifu tu lakini kweli tufanye kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nasema barabara hizi tunazijenga kwa gharama kubwa sana mimi ningependa sana tuone upande wa *maintenance*, kweli tuweke mikakati mizuri ambayo itahakikisha barabara hizi zinadumu, *otherwise* ni hatari kubwa. Lakini pia tufikirie kuishirikisha sekta binafsi katika kusimamia baadhi ya barabara hizi katika matengenezo na matunzo. Waswahili tunasema kitunze kidumu na tukiweza kufanya hivyo mimi naamini tutafanikiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba ndugu zangu nchi yetu ingekuwa na uwezo wa kuyafanya haya kwa pamoja, mimi naamini hatungekuwa tunagombana gombana sana haya kwamba mbona sioni barabara yangu.

Mheshimiwa Spika, lakini nimemshukuru sana Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake na kutoa hiki kiambatanisho cha sita kuiona nchi hii kila mkoa, barabara ambazo ni barabara kuu na barabara za mkoa na zipi ambazo katika kiwango cha lami tayari na vipo ambavyo tuna mipango nayo maana watu wengine wanasema mbona sisi tumesahaulika? Ndugu zangu kuna maeneo ambayo kweli yalikuwa yamesahaulika na sasa yanakuja vizuri. Naomna tujione kama nchi moja kwamba tunachokifanya tunajenga nyumba moja hakuna haja ya kugombania fito. Lakini tuhakikishe kwamba rasilimali hii tunaigawanya kwa uwiano mzuri kwa nchi yetu ili wote tujisikie kwamba tupo pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia nipate maelezo kwa barabara hiyo ya kutoka Arusha ambayo ndiyo kiunganisho katika mkoa wa Shinyanga na mkoa wa Arusha ni kwa nini iliondolewa? Lakini uwezekano sasa wa Wizara kuanza kuwa na muono mpya kwa kutambua kwamba kuna mkoa mpya unakuja wa Shimiyu basi tuone uwezekano sasa wa kutoka Mwanuhuzi unakuja Kisesa, unapita Gambasingu, unakuja Bariadi, unateremka kwenda Ngulyati mpaka Magu upandishe na mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sipendi nigongewe kengele ya pili, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niwatakie ndugu zangu waislamu mfuno mwema, tuombeane, Taifa letu liendeele kuwa na mshikamano, lakini niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Bariadi Magharibi kwa kuendelea kuniamini pamoja na yote ambayo yametokea tushikamane, tufanye kazi kwa faida ya Taifa letu, tumepata wilaya mpya ya Itirima, imezaliwa na Bariadi na tumepata mkoa wa Simiyu, hongereni sana fanyeni kazi ya kujiletea maendeleo, niko pamoja na ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natamka kuwa naunga mkono hoja hii ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Chenge alikuwa Waziri wa mambo haya, kwa hiyo ndiyo maana unakuta kawatajieni nyie wote kwa majina, kwa hiyo aliwahi kuwa Waziri mmoja mahiri katika eneo kabla ya Mheshimiwa John Magufuli, kwa hiyo alichukua viatu vyake naye akavivaa vimemtosha. Kwa hiyo namuita Mheshimiwa Rosemary Kirigini, nadhani kwa mchana huu ndiyo atakuwa wa mwisho. *(Makofi)*

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana naomba nianze kwa salamu za rambirambi...

SPIKA: Naona umechanganya sasa! *(Makofi/Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Spika siyo Naibu Spika!

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa sana naomba nianze na salamu za rambirambi kwa niaba ya Wabunge wote wa Mkoa wa Mara kwa kufiwa na Mwenyekiti wetu wa UWT wa Wilaya ya Serengeti, tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. Amin!

Lakini pia pamoja na salamu hizo za rambirambi naomba nichukue fursa hii ya kipekee kuwapongeza sana na kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mara kwa kunichagua tena kwa mara ya pili kuwa Mbunge wao, naomba kwa kupitia Bunge hili niwaahidi kwamba

nitafanya kazi yangu kwa umakini na umahiri mkubwa na kamwe hawatashuhudia nikitolewa nje kwa maana naelewa kabisa ni vipi kiongozi au Mbunge anatakiwa awe na vilevile naziwelewa kabisa Kanuni za Bunge letu Tukufu na hivyo wasitegemee kabisa kuniona kupitia luninga wala kusikia kwenye Tv au redio au magazeti kwamba Mbunge wao Mheshimiwa Rosemary Kirigini ametolewa nje. *(Makofi)*

Baada ya utangulizi huo kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli mimi binafsi leo amenigusa kuliko siku zote nilizoweza kumuona. Kwanza kwa umahiri alivyoweza kuisoma hotuba yake, nilikuwa najaribu kumfuatilia kwa makini lakini alianza nyuma akaja katikati halafu akamalizia na mwanzo. Kwa kweli ameonyesha umakini mkubwa. Lakini vilevile nimevutiwa kwa namna alivyoweza kutumia teknolojia ya kisasa na ningewaomba Waheshimiwa Mawaziri wengine waweze kuiga kwani tumeweza kushuhudia Mawaziri wengi wakija na makaratasi, mengine yakianguka na kupotea, kwa hiyo, naomba waige mfano wa Mheshimiwa Magufuli wa kutumia hiyo teknolojia ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imejielekeza katika suala zima la kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami. Mimi nimesikiliza wapinzani, wao bado hawaridhiki. Lakini tunajifananisha Tanzania na nini? Wao wanasema Malawi imeweza, Zambia imeweza na Msumbiji imeweza. Lakini tuangalie ukubwa wa eneo letu, ukiangalia Tanzania ni mara elfu saba na zaidi ya hizo nchi wanazozitaja. Kwa hiyo, mimi nadhani tuna haja ya kujipongeza na kutembea kifua mbele kwamba tumeweza na bado tunaendelea kuweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikakati iliyotajwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni mizuri sana napenda kupongeza hilo na kama itatekelezeka ipasavyo kwa maana wamepewa fedha za kutosha basi ni matumaini yetu kuwa ule usemi wa Mheshimiwa Magufuli kwamba utatoka Mtwara mpaka Dar es Salaam kwa *taxi* itawezekana na mimi nimeshuhudia kwamba kwani mimi siku hizi ninatoka Dar es Salaam mpaka Musoma, natoka Dar es Salaam saa 12 asaubuhi na ninaingia Musoma saa moja usiku. Kwa hiyo, hivyo ni vitu vya kujivunia na inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi napenda niongelee kidogo suala la vivuko. Hapa kwenye vikuko mimi nina matatizo, kivuko cha Lugezi - Kisolya kimetajwa kwa miaka mitano nikiwa hapa hapa Bungeni. Kila mwaka wa fedha kivuko hiki kinatajwa na mwaka jana mwezi wa nne niliuliza swali na nikaahidiwa na Waziri mhusika wakati ule akiwa Mheshimiwa Shukuru Kawambwa kwamba ifikapo mwezi wa kumi Kivuko cha Lugezi - Kisolya kitakuwa kinazinduliwa rasmi lakini mpaka leo tunavyoongea kivuko kile kina hali mbaya sana kwani kinavutwa na kamba na wakati mwingine kinapotelea majini na abiria.

Sasa leo hii bado sijaona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ikisema ni lini kivuko hiki cha Lugezi - Kisolya kitakamilika. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha aniambie sasa kwa mara ya mwisho maana yake miaka mitano yote tumeahidiwa, watu wetu wapo katika hali mbaya sana. Leo aniahidi je, kivuko hiki kitakamilika lini ili tuweze kupata amani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimemsifia lakini nasikitika kusema sijamsikia akiongelea barabara zilizoahidiwa na Mheshimiwa Rais. Kwa mfano, barabara ya Bunda - Kisolya, barabara hii inaanzia Nyamswa - Bunda kwenda Kisolya.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa naomba niongelee barabara hii kwani inapita kwenye Jimbo la Mwibara. Jimbo hili halina barabara, halina kivuko na limewekewa nguzo za umeme kwa takribani miaka mitatu wenyewe wanalinda tu nguzo lakini hawana umeme. Mheshimiwa Rais ametuahidi mara tatu na sisi Wabunge tumefuatilia miaka mitano lakini barabara hii usanifu anaouongelea Mheshimiwa Waziri umeanza kwa upande wa Nyamswa kuja Bunda.

Kwa upande wa Bunda kwenda Kisolya hatujaona lolote na ninasikitika kusema tarehe 18 Julai Mheshimiwa Machemli aliuza swali hili hili lakini yeye aliendeleza mpaka Ukerewe yaani barabara hii kwenda Ukerewe na Mheshimiwa Waziri alitupa majibu mazuri sana hapa na

Mheshimiwa Mbunge alimpongeza sana Waziri kwa jibu hilo. Lakini tulivyokwenda kwenye vitabu vya maendeleo hakuna fedha za kujenga barabara hii, lakini Waziri siku hiyo ya tarehe 18 Julai alituahidi kwamba barabara hii itakamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012. Namuomba atakapokuwa anafanya majumuisho atueleze sisi wananchi wa Mara na Jimbo la Mwibara kwa ujumla barabara hii itakamilika lini? Na hizo fedha anazitoa wapi? Zipo kwenye fungu lipi? Maana yake kwenye fungu la maendeleo fedha hizi hazipo.

Mheshimiwa Spika, niunganishe vilevile na barabara muhimu sana ambayo Waziri anaifahamu vizuri sana nayo ni barabara ya kutoka Musoma kwenda Mgango, kwenda Makojo, kwenda Bukima, kwenda mpaka Busekela kilomita 94. Barabara hii ni muhimu sana kwani vijiji hivi vinakaa kandokando ya ziwa, tumeshindwa kujenga viwanda vya samaki kukuza uchumi wetu. Barabara hii ni mbaya sana na Mheshimiwa Rais ametuahidi mara kwa mara, sasa mimi nashangaa Rais anaahidi Waziri hazungumzii ahadi zozote za Rais. *(Makofi)*

Mimi ningependa kufahamu ahadi hizi za barabara za Mheshimiwa Rais zinashughulikiwa na nani? Kwa sababu sisi wananchi wa Mkoa wa Mara tunaiona barabara hii ya kutoka Musoma kwenda Makojo, kwenda Bukumi ni barabara muhimu mno, mvua ikinyesha waliopo Musoma Mjini wanabaki mjini na walioko Bukumi na Mgango wanabaki Mgango. Tunamuomba Mheshimiwa Waziri atueleze barabara hii inajengwa lini na kama haiwezekani basi angalau iweze kujengwa kwa kiwango cha changarawe na yale madaraja yote ambayo hayapitiki kipindi cha mvua yaweze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya barabara hizo ningependa pia kuongelea barabara ya Musoma - *Fort Ikoma*. Katika kitabu cha Bajeti cha mwaka jana barabara hii inatajwa kama Nata - *Fort Ikoma* na kitabu hicho cha Bajeti cha hotuba ya mwaka jana kimeripoti barabara hii kwamba upembuzi yakinifu umekamilika tangu mwaka 2006 na fedha za ujenzi wa kiwango cha lami zinatafutwa. Kwa mwaka huu barabara hiyo hiyo imejatwa Nata - *Fort Ikoma* kilomita hizo hizo 114 lakini hakuna chochote kilichozungumziwa kwamba fedha zimetengwa sasa barabara hiyo inaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tufikirie kama barabara ilitakiwa kukamilika tangu mwaka 2006 mpaka leo hii Waziri hana mawazo ya kuifikiria barabara hii kujenga kwa kiwango cha lami je, haoni kwamba hata ule upembuzi yakinifu uliofanyika utakuwa ni bure? Ni sawasawa na kuchukua fedha na kuzitupa kwenye choo cha shimo? Lakini vilevile nampongeza sana Waziri, leo mimi nilikuja hapa nikiwa nimepania sana na ndiyo maana sijaongea tangu Bajeti imeanza, nilikuwa nimepania sana Wizara hii. Lakini leo Waziri ametufurahisha wananchi wa Mkoa wa Mara kwa kututajia hii barabara ya Makutano - Nata - Mugumu - Loliondo mpaka Mto wa Mbu na kilichonifurahisha zaidi katika hii shilingi bilioni 1.6 zilizotengwa ujenzi upembuzi yakinifu unaanza kwa upande wa Makutano mpaka Nata kama shilingi bilioni 700 kwa upande wa usanifu na bilioni kama 800 kwa upande wa ujenzi wa kiwango cha lami. Kwa kweli tumefarijika sana kama yaliyoandikwa hapa yatatekelezeka basi na sisi kwa miaka yote hiyo tuliyokaa tukiwa watazamaji humu ndani na kuitaja barabara hii miaka hadi miaka na haijengwi hatimaye leo imetajwa na imetengewa fedha, tunaishukuru sana Wizara na tungeomba barabara hii iweze kukamilika haraka iwezekanavyo kwani barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia Mheshimiwa Waziri atupatie ufafanuzi, katika kurasa mbalimbali za hotuba yake kwenye ukurasa wa 28 wa hotuba yake, ameitaja barabara hii kama kilomita 452 lakini kwenye ukurasa mwingine wa 63 ameitaja barabara ya Nata - Mugumu - Loliondo mpaka Mto wa Mbu kilomita 328. Sasa tungependa, maana yake tunafuatilia kwa makini sana, tungependa Waziri katika majumuisho yake atueleze barabara hii ni kilomita ngapi? Maana yake imetajwa kilomita tofauti tofauti, tunaomba atueleze barabara hii ina urefu wa kilomita ngapi?

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuzungumzia suala la thamani ya ubora wa barabara zetu za Mikoa. Kwa kweli ni hali ya kusikitisha sana, nimefurahi sana kuona hotuba nzima inazungumzia kwamba fedha zilizotafutwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara nyingi ni fedha zetu za ndani. Kwa hilo nawapongeza sana kwa sababu tumeona huko nyuma tulikuwa tukitegemea

fedha nyingi sana kutoka nje lakini hatukuzipata kwa wakati na ilipelekea miradi mingi ya barabara kukwama lakini kwa kipindi hiki mimi mmenifurahisha sana kwani fedha nyingi zinazotumika kujenga barabara ni fedha zetu za ndani yaani za walipa kodi. Sasa naomba Bunge lako Tukufu kwamba fedha hizi zitakapokuwa zinatumika basi wajaribu kuangalia kwa kuwapa fursa wakandarasi wetu wa ndani. Lakini niseme pia wakandarasi wetu wa ndani wamejenga baadhi ya barabara lakini kwa masikito makubwa barabara nyingi zimeonyesha kuwa chini ya kiwango yaani hazina ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuchukulie mfano tu wa barabara za hapa Dodoma, tunazona kwani hazina ubora, wakandarasi wetu wa ndani wanalalamika sana kwamba hawapewi kazi, lakini hawaonyeshi mfano, wanapopewa kazi hawaonyeshi mfano kwa kweli. Yupo mkandarasi mmoja hapa ananitazama vibaya lakini habari ndiyo hiyo! Hawatuonyeshi mfano na wanatuangusha vibaya mno, barabara nyingi ziko chini ya kiwango. Kwa hiyo, ningeiomba Wizara kupitia kwa wakala wake *(TANROADS)* wajaribu kuangalia namna gani wanaweza kuongeza usimamizi katika eneo hili. Kama mtu anapewa barabara basi huyo mkandarasi aweze kujenga katika ubora unaotakiwa. Kuwe na *value for money* na kama hakuna *value for money* basi yule mkandarasi aweze kuwa *blacklisted* na siku nyingine asipewe kazi nyingine yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kupitia Bunge hili nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkandarasi mmoja anayejenga barabara ya *Bahari Beach* – Ununio – Boko mpaka Mbweni. Mkandarasi huyu mimi binafsi ananifurahisha sana kwanza kwa ile kasi ya ujenzi lakini pia kiwango. Mimi ninaitembelea barabara ile kwa sababu ninaishi maeneo ya *Bahari Beach* kwa hiyo, ninaitembelea mara kwa mara. Mkandarsi yule ni mzawa lakini kwa kweli hajatuangusha na ninaomba kwa kweli wakandarasi wote wa Tanzania waige kutoka kwa mkandarasi yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa unikalische, naomba kuunga mkono hoja na ninawapongeza sana Wizara na wataalamu wote. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, umeshawaambia watu wako kwamba huvunji kanuni. *(Makofi)*

TAARIFA

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, taarifa!

SPIKA: Hiyo ni ya kwako humwambii huyu, haya sema taarifa yako!

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anasema...

SPIKA: Utoe taarifa tu usimpe mtu yeyote maana yeye ameshamaliza kuzungumza.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, ni kwamba barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisolya katika ukurasa wa 141 kwenye Bajeti ya Waziri imetengewa fedha na upembuzi yakinifu ni dalili kwamba ni lami inawekwa. Kwa hiyo, siyo kwamba imesahaulika. *(Makofi)*

SPIKA: Tunashukuru kwa Taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa kama walivyosema wasemaji wachache, tunaomba tuwaombe wenzetu walioanza mwezi wa Mtukufu wa Ramadhani mfungo mwema na wenye baraka kwetu wote. *(Makofi)*

Kama nilivyotangaza asubuhi Wenyeviti wote wa Kamati tunakuwa na kikao sasa hivi ili kuweza kuangalia ratiba ya kipindi hiki kwa ajili ya kuwawezesha wenzetu hawa waweze kufanya kazi hiyo ya kufunga vizuri. Kwa hiyo, kutakuwa na kikao sasa hivi saa saba na kama hakuna Mwenyekiti basi Makamu wake aweze kuja.

Sina matangazo mengine zaidi ya kusema tulikuwa Uingereza kwenye Mkutano wa *Commonwealth Parliamentary Association*, Wabunge wote duniani ambao nchi zao zilikuwa chini

ya Jumuiya ya Madola tuna umoja unaitwa Chama cha Wabunge wote wa Jumuiya ya Madola yaani *Commonwealth Parliamentary Association*. Mwaka huu imetimiza umri wa miaka 100 toka kianzishwe wakati huo na kwa mara ya kwanza Katibu Mkuu Mtendaji ni Mwafrika mweusi na anatoka Tanzania naye ni Dkt. William Shija. *(Makofi)*

Sasa katika nafasi ile ile Tanzania ni mwenyeji au tuseme ni *Secretariat* ya *Commonwealth Parliamentary Association* Kanda ya Afrika, sisi ni wenyeji wa Mkutano huo yaani *Secretariat*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika amemaliza kipindi chake alikuwa ni mwakilishi wa Kanda ya *East Africa* katika hii *Association* na amemaliza katika mkutano huu sasa nafasi hii imechukuliwa na Uganda. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tulikwenda kule na kulikuwa na uchaguzi pia wa Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji yaani *Executive Committee*, mara ya mwisho ilikuwa Malaysia yaani mara mbili imekuwa kule lakini kwa safari hii kwa sababu ya kufanya kazi pamoja na wenzetu maana yake kuna nchi zilizoendelea na zisizoendelea kwa hiyo, kulikuwa na kampeni kubwa sana na bahati nzuri Mwingereza amechukua kiti hicho na ni Mwingereza aliyekuwa Mbunge katika *House of Commons* ambao hao waliokwenda kufuatilia zile fedha zilizoendelea za rada ameshiriki sana kuunganisha Wabunge na kuitisha ile *public hearing*. Kwa hiyo, sisi tulikuwa na sababu zote za kuhakikisha huyu anapita na kwa kweli ujumbe wetu uliokwenda kule umefanya kazi kubwa sana na yule amechaguliwa kuwa ndiye Mwenyekiti wa *Executive Committee* kwa miaka mitatu ijayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tumewawakilisha kule na tunaendelea na wiki ijayo kutakuwa na mkutano wa *Commonwealth Parliamentary Association* wa Maspika wote na huu utafanyika Malawi. Kwa hiyo, hiyo ndiyo taarifa tuliyonayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema sina taarifa nyingine naomba nitishe shughuli mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11. 00 jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mheshimiwa George B. Simbachawene) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge)

HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 150 naomba kwa ruhusa yako Bunge lako Tukufu likubali kutengua Kanuni ya 28(2) kutokana na maelezo ya asubuhi ya Mheshimiwa Spika na kutokana na ukweli kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu wako kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Naomba kutengua Kanuni ya 28(2) ili marekebisho machache yafanywe katika muda wa kuanza Bunge kwa saa za mchana, badala ya kurudi saa 11.00 jioni turudi 10.00 jioni na muda wa kumaliza Bunge jioni iwe saa 12.45 jioni badala ya saa 1.45 usiku ili wenzetu wawezeshwe kuwahi kufuturu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki! *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Bunge liliafiki Kutengua Kanuni zilizotajwa)

MWENYEKITI: Hoja imepita kwa hivyo kuanzia leo hadi tutakapomaliza mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa ajili ya kuwawezesha wenzetu waweze kufanya ibada vizuri, kwa wakati wa jioni tutaanza 10.00 jioni na kumaliza 12.45. Huo ndiyo uamuzi tulioufanya kwa pamoja. Naamini kwamba italeti fursa nzuri kwa wenzetu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii ni Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu ya Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wasomaji wa Biblia, nimesema Biblia, maana yake Watanzania wanasema Bibilia, siyo Bibilia, Biblia. Kwa wasomaji wa Biblia, Agano la Kale, Kitabu cha 1Wafalme 3:4 – 27 wanamuongelea Mfalme Suleimani. Mfalme Suleimani alirithi kiti cha baba yake, Mfalme Daudi na aliposimikwa kuwa Mfalme aliamua kwenda kwenye mji unaitwa Gideoni ambao uko juu katika milki ya falme yake, kwa lengo la kutoa dhabihu kwa Mwenyezi Mungu. Akaenda kule na watu wake akamtolea Mwenyezi Mungu dhabihu, akamtolea shukrani, akateketeza sadaka chungu mzima, maelfu kwa maelfu, akafurahi, akaridhika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jioni wakati Mfalme Suleimani amelala, Mwenyezi Mungu akamtokea kwenye ndoto akamwambia, Suleimani sema utakacho nitakupa! Suleimani akasema; Mwenyezi Mungu umemkarimu sana Baba yangu Daudi, amekuwa Mfalme kwa miaka mingi sana, umempa hekima na maarifa, ametawala miaka mingi, amewatawala watu wako vizuri sana na vilevile mimi mtoto wake ukanifanya niwe Mfalme kwenye nchi yako hii, umenipa watu chungu mzima wa kuwatawala, nakuomba Mwenyezi Mungu mimi unipe adili nijue kuhukumu, nijue mema na mabaya, ndiyo alichomba Mfalme Suleimani. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: *Good!*

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mwenyezi Mungu akafurahi sana, akamwambia lah! Suleimani, nilidhani ungeomba utajiri, ungeomba maisha marefu, ungeomba roho za adui zako, lakini wewe umeomba adili ya kuhukumu watu wangu na kujua mema na mabaya. Tazama nitakupa! Nitakupa adili ya kuhukumu kwa haki, nitakupa mali, nitakupa maisha marefu, akampa vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suleimani alipotoka hapo na akawa amerudi kwake akapata mtihani wa kwanza, wakaja mbele yake wanawake wawili makahaba wameshika mtoto mmoja mchanga wa miezi miwili au mitatu. Mwanamke wa kwanza akasema; mfalme sisi tunakaa chumba kimoja wawili, tulikuwa tumejifungua watoto wawili kwa kupishana wiki moja tu, mwenzangu jana usiku alikuwa amelewa akamlalia mtoto wake akafa, akamchukua mtoto wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke mwingine akasema; hapana mtoto huyu ni wa kwangu mimi, siyo wa mwenzangu. Mfalme Suleimani akasema ahaa, ipo hivyo! Wewe unasema ni wa kwako, yule aliyekufa si wa kwako, na wewe unasema huyu mtoto ni wa kwako, aliyekufa si wa kwako. Basi watumishi leteni panga nimkate mtoto katikati vipande viwili ili kila mama aende na kipande chake. Yule mama ambaye mtoto siyo wake akasema ndiyo, haki itendeke, mtoto akatwe katikati kila mtu achukue kipande chake aende zake. Yule ambaye mtoto ni wake akasema; mfalme nakuomba sana mtoto aende naye huyo mama, asipigwe panga!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napoona wanasiasa Bungeni hapa tunahubiri chuki, vita, roho inaniuma sana. Ningekuwa na uwezo ungeniruhusu nilie hapa nilipo. *(Makofi)*

MHE. ANNE K. MALECELA: Hapana usilie mwanangu! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Usilie ila useme tu tukusikie! *(Kicheko)*

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasiasa wanaohubiri vita Tanzania ni sawasawa na mwanamke aliyesema mtoto huyu akatwe vipande viwili. Wanataka nchi yetu ya Tanzania yenye neema, utulivu, mshikamano, ikatwe vipande vipande kama alivyosema mwanamke yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, roho inaniuma sana. Nawaomba sana wanasiasa, nchi hii tumepewa na Mwenyezi Mungu bure. Ndiyo, mtoto huyu ndiye tuliyebaki naye peke yake. Tusitake akatwe vipande vipande Tanzania! Nafikiri nimeeleweka sitalia, nitaenda kulia nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie kidogo kwenye hoja ya Mheshimiwa Dkt. John Magufuli. Nataka niongelee hawa wahandisi washauri (*consultants*). Kwa kawaida kunapokuwa na mradi wa barabara au ujenzi wa jengo, Serikali au *client* anamuajiri mhandishi mshauri (*consultant*) asimamie kazi yake pale. Yeye ndiye anayemsimamia mkandarasi, kwa hiyo, inapofika wakati kipande cha kazi kimekamilika, huyu *consultant* ndiye anayesaini *certificate* kwamba kazi hapa imekamilika, huyu alipwe. Lakini bahati mbaya mara nyingi hawa ma-*consultants* hawalipwi vizuri na Serikali na kwa sababu hiyo wao sasa wanashirikiana na wakandarasi (*wana-collude*) wana-*cut corners*. Kwa hiyo, wanalipwa na wakandarasi. Nawaambia ma-*consultants*, jamani, hebu iangalie barabara ya Sam Nujoma! Iangalie umaliziaji wake barabara ile. *(Makofi)*

Kwanza, imechukua muda mrefu kumalizika, lakini angalia umaliziaji wake! Angalia *workmanship* yake! Angalia barabara ya Kilwa, angalia barabara ya Kilwa! Angalia barabara ya Nangurukuru, naambiwa kuna kipande fulani imebidi kirudiwe pamoja na kwamba mkandarasi alishalipwa. Imebidi kirudiwe! *Consultants*, jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa ndege wa Songwe ni habari mbaya zaidi. Uwanja wa Songwe mkandarasi yupo pale, *design* iliyowekwa ni kwamba unaweka kokoto halafu unaweka *fill* ambayo inakuwa ya mawe yaliyosagwa, ndiyo uweke lami juu yake. Kwa sababu unatakiwa uweke *fill* ya mawe yaliyosagwa, kwa hiyo unatakiwa uwe na *crasher* kubwa. Sasa huyu mkandarasi ambaye yuko pale Mbeya kwenye Uwanja wa Ndege wa Songwe, hana *crasher* pale *site* wala *in the vicinity* hamna *crasher*. Kwa hiyo, mkandarasi huyu hawezi kuweka jiwe lililosagwa kwa ajili ya kuweka *fill* ile inayotakiwa, amemua kuweka *cement pozzolana*, sasa ameweka sementi hiyo bei imepungua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu ni kwamba hiyo *base* aliyoitengeneza kwa zile kokoto na hiyo *pozzolana* ime-*crake* hata kabla lami haijawekwa. Jamani Uwanja wa Ndege wa Songwe, tunataka watu wa Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, ndiyo *gate way* yetu. Tunataka na sisi tupate masoko ya nje kupitia uwanja ule, inakuwaje *consultant* unamuacha mkandarasi anafanya hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa tena kwamba kuna *consultant* mmoja alikuwa pale anaitwa *Crown Take Consultancy Firm* ambaye anatokea Kijitonyama, baada ya kuona uchakachua huu amekimbia, ameingia mitini. Naambiwa hata barabara inayokwenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, inayotoka Tunduma kwenda Sumbawanga tayari *consultant* anashirikiana na mkandarasi kuichakachua. Barabara inayokwenda Ikulu anaichakachua! Jamani hawa ma-*consultants* hata kama hawaogopi kuiharibu nchi yetu ya Tanzania, naomba wamuogope Mungu. Naomba *consultants* muogopeni Mungu! Kwa sababu nyie wahandisi hamjui kwamba makosa yenu yanasimama kama *monuments*, tofauti na wenzenu madaktari ambao makosa yao yanazikwa. Ninyi makosa yenu yanasimama na kila mtu anaona. Naomba *consultants'* ioneeni huruma nchi hii, mnaikamua vibaya mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *wait a minute*, hivi elimu, uwezo na *experience* ambayo anayo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na elimu, uwezo na *experience* alionao Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwasambwiga Mwakyembe, mnashindwa kuwachakachua hawa ma-*consultants*? Wao wanaichakachua nchi, nyie mnashindwa kuwachakachua? Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, ninawaombeni sana muwachakachue hawa ma-*consultants*, wanaiharibu nchi vibaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pale *TANROADS* na *TBA* muweke vitengo vya *post contract audit* ili tujue kwamba barabara ya kutoka Mbeya – Chunya – Makongorosi, mkataba ulisainiwa kwamba utakuwa wa gharama ya shilingi bilioni 50 lakini mwisho wa siku imekuwa shilingi bilioni ngapi? Tujue kwa nini imekuwa hivyo. Tujue jengo la ghorofa 20 ambalo linajengwa mjini Mbeya mkataba ulisema litagharimu shilingi bilioni 20 lakini mwisho wa siku gharama ni shilingi bilioni 30 tujue ni kwa nini? Naombeni sana muweke vitengo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee barabara ya Mbeya - Chunya - Makongorosi, barabara yangu hii. Barabara hii imeanza kujengwa mwaka 2008. Alikuwa ni mkandarasi huyu huyu ambaye ndiye anajenga uwanja wa ndege wa Songwe. Toka mwaka 2008 mpaka leo hamna hata mita moja ya lami. Yeye alipewa kipande cha kwanza kutoka Mbeya hadi Lwanjilwa, lakini juzi nafurahi Serikali imeweka mkandarasi mwingine kutoka Lwanjilwa kwenda Chunya ameanza, lakini na yeye hajaanza kuweka lami na huku nyuma nako mmepata mkandarasi mwingine wa kurithi ile kazi ambayo alipewa mkandarasi wa kwanza, ambaye mmefukuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ina muda mrefu mno. Nimesoma vitabu vya Mheshimiwa Waziri, mwaka juzi ilipangiwa shilingi bilioni kumi, mwaka jana shilingi bilioni kumi, mwaka huu shilingi bilioni tano, nilitaka nitoe shilingi yako, lakini nimekusamehe kwa sababu najua ndiyo unaanza. Hilo la kwanza, kwa sababu unaanza, lakini pili kwa sababu wewe *Sanji* yangu. Hii shilingi bilioni tano haitoshi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujibiwa maswali mawili; kwanza hii barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi jamani itaisha lini? Barabara hii ndiyo *the great north road* ya kwanza ilikuwa inapita huku. Mbeya – Chunya – Makongorosi itaisha lini ili tuanze kuongelea habari ya kutoka Makongorosi kwenda mpaka Rungwe na twende mpaka Tabora? Mnijibu hilo la kwanza.

Swali la pili naomba mnijibu kwamba mkandarasi wa kuanzia Chunya - Makongorosi sasa wa mwisho atateuliwa mwaka huu? Maana yake tunaye wa kutoka Mbeya - Lwanjilwa, wa Lwanjilwa – Chunya tayari ameishaanza kazi. Je, wa kuanzia Chunya - Makongorosi atateuliwa mwaka huu? Naomba mnisaidie na wananchi wangu wa Chunya wamechoka sana kuniuliza na mimi mwenyewe nimechoka kuulizwa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi itaisha lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya kwa wananchi wa wilaya yangu ya Chunya wanaofunga Ramadhani nawatakia Ramadhani njema. Kwa Watanzania wote mnaofunga Ramadhani ninawatakia *Ramadhan Mubarak!* Kwa Waheshimiwa Wabunge mnaofunga Ramadhani ninawatakia *Ramadhan Karim!* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, nakushukuru Mheshimiwa Mwambalasa kwa kunisaidia muda hapa. Sasa nitamuita Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Mfaki na baadae Mheshimiwa Mariam Kisangi ajiandae. *(Makofi)*

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu na uhai mpaka jioni hii ya leo na mimi nikiwa katika Bunge lako hili Tukufu kuweza kuchangia hoja hii na pia kunikutanisha na mfungo wa Ramadhani mwingine. Namshukuru sana! *(Makofi)*

Pili, napenda kuchukua nafasi hii kuwatakia kheri waislamu wote katika swaumu zao. Swaumu iwe njema katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Nawatakia kila la kheri na nina imani Mwenyezi Mungu atawafungulia kila lililo la kheri. *(Makofi)*

Tatu, napenda kukushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza kabisa napenda kusema kwamba

Mheshimiwa Rais hakukosea Wizara hii kumrudishia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na akampa Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, kwa sababu nina imani wanazielewa sheria na Mheshimiwa Magufuli ni mzee wa takwimu, najua atakwenda vizuri kwa takwimu na kutekeleza yote aliyoyaahidi kwenye Bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na ombi la kwanza. Ninafahamu kabisa kwamba barabara ya Nyerere (*Nyerere Road*) iliyoko pale mjini Mwanza ambapo inaanzia na kwenda mpaka Musoma, ni barabara kuu. Lakini napenda kumuomba Mheshimiwa Waziri suala moja, pale eneo la Mabatini ni eneo kongwe, tunahitaji Wizara hii iweze kutuwekea daraja la juu kama lile la Manzese ili kuondoa usumbufu uliopo eneo la Mabatini mjini Mwanza, kwani kwanza hilo litachochea usalama wa wananchi kwa sababu watawuka bila wasiwasi na pia wanafunzi watapita bila wasiwasi kuliko ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni imani yangu kabisa kwa ombi hili na ninamuona Mheshimiwa Waziri anatingisha kichwa, ninajua amelikubali moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nilikuwa naiomba Wizara ya Ujenzi, imeweza kutuwekea matuta hasa katika hiyo barabara inayokwenda Musoma, ninafikiri siyo matuta ila ni *foundation* ya kujenga nyumba kwa sababu gari ndogo zinapita kwa shida. Wenye magari madogo wanashindwa kupitisha magari yao hasa eneo la Mabatini, Nyakato Sokoni yaani matuta yamekuwa... sijaelewa kwamba wanatumia vigezo gani kujenga matuta haya. Tungewaomba basi angalau hata kama wataweka matuta mawili au matatu kwa sehemu tofauti, lakini yasiwe makubwa kama waliyoyajenga. Nafikiri hatuhitaji kujenga nyumba katikati ya barabara, tunahitaji usalama wa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu nilikuwa napenda kuchangia suala moja la barabara ya *Airport* kwa sababu nina imani hii ni barabara ya Mheshimiwa. Kuanzia uwanja wa ndege kuelekea barabara inayoelekea Ihale, nafikiri sasa hivi inakaribia kufungwa. Mheshimiwa Waziri, maombi yetu yapo mezani kwako kuanzia mwaka 2009 ili tuweze kutafuta barabara mbadala ya kuwawezesha wasafiri au wafanyabiashara wanaokaa maeneo ya Sangabuye, Igombe waweze kupata barabara. Tulikuwa na pendekezo kwamba barabara hii ianzie eneo la Sabasaba, ipite Kiseke, ipite Kahama kwa kutokea Igombe na ielekee Kayenze, Kata ya Sangabuye na baadaye hata kama ikitokea Kisesa – Magu si hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu kwa sababu maeneo tunayoongelea uchumi wake unategemea uvuvi na kwa kuwa barabara hii ilikuwa ni ya *TANROADS* basi waichukue waweze kuitengeneza. Nafikiri tunasubiri amri tu kutoka kwa Mheshimiwa mkubwa, Waziri wa Ujenzi kwa sababu tumekwishaongea na Meneja wa *TANROADS* Kanda tumekubaliana lakini tulileta maombi yetu kuanzia mwaka 2009 yako mezani kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa umebadilika kutoka Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na kuja Wizara ya Ujenzi, lakini nafikiri Serikali ni moja, maombi haya yapo mezani kwako naomba tuyashughulikie ili tuweze kupata barabara mbadala mapema. Kwani barabara hizi sasa hivi ni finyu sana hii tunayokuambia ianzie Sabasaba kupitia maeneo yanakoelekea. Lakini tunasema tuna haja ya kupanua Jiji la Mwanza kwa kutengeneza barabara zenye upana mkubwa ili baadae watu watakapokuja kujenga zije zikagusa majengo yao, majengo ya watu yabaki salama na tuweze kupata barabara ya uhakika kwa hawa wafanyabiashara wanaoelekea maeneo ya Igombe na Kayenze pamoja na wakati wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea suala moja. Nilifurahi sana niliposikia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi anataja maeneo ambayo nyumba zinastahili kuwa na anataja ni umbali gani unaotakiwa, lakini nilikuwa napenda nimkumbushe kidogo wakati tunaelekea kubomolewa nyumba za Pasiansi pale karibu na Msikiti, kuna baadhi ya wananchi walilipwa waliokuwa wamejenga usawa ule ule, kuna baadhi ya wananchi walilipwa fedha wakapewa viwanja, kuna baadhi ya wananchi walipewa viwanja na kuna baadhi ya wananchi mpaka leo hii hawajapata chochote. Pamoja na kwamba aliniambia hawahitaji kulipwa lakini ninamwomba tena kiongozi aliye bora ni kiongozi anayefuatilia. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri ufuatilie kujua kwa nini wengine wamelipwa kwenye foleni hiyo hiyo na wengine mpaka leo hawajalipwa,

kulikoni kusema hatulipi hapa unakuja kuwaweka kwenye mkumbo ambao wapo na wasiokuwepo na ambao wanadai haki zao mpaka leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni hivyo basi nafurahi pia kusema kwamba Mheshimiwa Magufuli anasema kuna Sheria ya mwaka 1933 na nakubaliana nae kabisa na zinasema nini ambapo mimi na yeye tulikuwa hatujazaliwa, lakini wenye nyumba hizi walikuwepo wakiishi pale. Sheria hizi nafikiri zilitungwa na mkoloni na ziliandikwa lugha aliyokuwa anaifahamu mkoloni sidhani kama Masanja wa kule Mwanza alikuwa anaifahamu sheria hii na wala sidhani kama watu wote walikuwa wakifahamu sheria hii, lakini ni kwamba ule mji ulikuwepo siku zote, ni mji wa zamani na ni mji mkongwe. Naendelea kuomba Mheshimiwa Magufuli narudia tena kiongozi aliyebora ni yule aliyefuatilia je, pesa za wananchi hawa hazikulipwa zimekwama wapi? Nakumbuka wakati anamkabidhi Rais wa Awamu ya Tatu barabara hii alimwambia watu wote wamekwishalipwa, lakini ile kauli Mheshimiwa Magufuli napenda ujue kwamba haikuwa hivyo kama ulivyodhani ninafikiri sasa ni wakati muafaka wa kufuatilia ni nani alilipwa na pesa za nani zilikwenda wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi pia amesema katika Sheria ya mwaka 2007 Sheria Na. 13 inatakiwa wale waliokutwa kwenye mita 30 watalipwa na ambao wamevamia hawatalipwa kitu. Ningependa kuhoji kitu kimoja kwa kumbukumbu zangu ninakumbuka Misheni kulijengwa *petrol station* kubwa na nafikiri katika kufanya maamuzi uliyoyafanya ni kwamba ile *petrol station* ilikuwa ndani ya mita zako na *petrol station* ile ilibomolewa. Lakini basi ubavuni mwa *petrol station* iliyobomolewa kuna ghorofa mpaka leo je, tukisema kama tukaone mita unazozisema ndivyo zilivyo kwenye hilo ghorofa. Kwa sababu tunaposema sheria wananchi tutawahukumu hivi tujue na sisi tunayetunga sheria, je, tunaipindisha, je, tunaipeleka sawa sawa au je, sheria hii inatakiwa imguse nani. Pamoja na kusema kwamba kuna sheria lakini nina imani kabisa sheria hizi haziendi ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa kama ni kawaida najua katika Wizara ya Maji sitaongea imekuwa kama ni kawaida watu wanapohamishwa kutoka eneo fulani kwa ajili ya maendeleo fulani hatukatai maendeleo, lakini malipo yao yanakuwa ni magumu, malipo yao yanakuwa hayaendani na wakati. Kwa kuwa najua sitaongea katika Wizara ya Maji pale pale Butuja kuna watu wamehamishwa. Kwa hiyo, atakayekuja kunijibu kama ni Waziri wa Maji ataniambia kuna watu wamehamishwa pale Butuja, lakini hawakuweza kulipwa mpaka leo na wamepisha majitaka na wale wananchi wanahangaika.

Mimi naomba tusifanye Serikali yetu ikawa ni Serikali ya kulalamikiwa na wananchi kila kukicha wananchi wanalalamika, kila kukicha wananchi wanalalamika. Wananchi hawa ni maskini sana, wananchi hawa wanatumia muda mrefu kufanya yale wanayoyahitaji, lakini pale ambapo inapofikia kubomolewa nyumba zao hawaambiwi, hawalipwi na wanalipwa kwa ubaguzi hata hapo Butuje wanalipwa kwa ubaguzi. Wengine wamelipwa kiwanja na pesa, wengine wamelipwa pesa, wengine wamepeva kiwanja, wengine wamebaki hivyo hivyo. (Makofi)

Kwa hiyo, huu utaratibu umeonekana ni kama upo ndani ya Serikali yetu. Naomba huu utaratibu tuuache. Mheshimiwa Magufuli naomba tukitoka hapa mimi na wewe tukapime lile ghorofa liko mita ngapi pale Misheni tujue liko ndani ya *service road* lishuke. Kama ambavyo ilivyoshuka *petrol station*, lakini sio tunambomolea huyu, huyu tunamuacha, lakini napenda kusema kwamba kubomoa bomoa ambapo tunafikia sasa hivi tunaitia Serikali hasara.

Ninakumbuka kuna *petrol station* ya mwananchi imebomolewa na imelipwa shilingi bilioni tatu kama sijakosea, hii ni kuitia Serikali hasara, pesa hii ingeweza kufanya matatizo mengine na pesa hii ingeweza kuwafidia wananchi ambao wapo pembeni ambao mmewakuta wale mngewalipa na baada ya kuwalipa wale wananchi sasa hii ingefanya kazi nyingine. Kulikoni kushindana bomoa bomoa sawa, lakini mwisho wa yote kwa wale wajanja wanaitia Serikali hasara kwa ajili kwenda kushtaki, kuna kesi ngapi Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kesi chungu mzima za kubomolewa watu nyumba zao, lakini hao wasiokuwa na watu wa kuwaonyesha nenda Mahakamani wanalipwa na nani? Mimi

naomba tunaposema haki sawa sisi *CUF* tunaamini haki sawa na ndiyo sera yetu. Haki sawa iwe kwa maskini na tajiri pia, sio haki sawa kwa maskini, kwa tajiri isiwe haki sawa. Mheshimiwa Magufuli naomba tena tutakapoondoka na wewe twende pale Nera tuhesabu hizo *site* mita ulizosisema kutoka katikati ya barabara kama nyumba za Nera zipo sawa na hayo unayoyaongea kwa sababu naona kuna maghorofa mapya yameshaanza kuota kama uyoga na maghorofa hayo yapo barabarani, kwa hiyo, tunapoisema hii sheria inawagusa wenye nyumba za tembe iwaguse na wenye nyumba kubwa iwaguse na wenye pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache napenda kukushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kimwanga. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mariam Mfaki na Mheshimiwa Mariam Kisangi ajiandae. *(Makofi)*

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia jioni ya leo. Kabla sijaendelea ni vizuri kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote afya njema na kuwepo leo jioni katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukupongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa jinsi walivyoandaa hotuba yao hii. Mheshimiwa Magufuli tunamfahamu ni mchapakazi, ni mtu asiyechoka, ni mtu ambaye anaipenda kazi yake. Vilevile amepata Naibu Waziri ambaye wote sasa wamekutana wamekuwa kama watoto wa mama mmoja, baba mmoja. Mheshimiwa Magufuli chapa kazi na wala usitikisike na neno lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa ujumla wake kwa jinsi ilivyojitahidi kuweka mtandao wa barabara za lami na kuunganisha mikoa karibu yote ya Tanzania. Sasa nitashangaa sana kwa wale wanaosema kwamba Serikali haijafanya chochote hata kwa hili la barabara sina uhakika kama hawajui. Kwa hiyo, naomba wote tuwe wasema kweli kwa sababu wananchi wanatusikiliza, wanatuona na ni vizuri kuwa wakweli wakati wote. *(Makofi)*

Sisi Warangi tunasema mtu akisema jambo ambalo sio la kweli unamwambia tema mate chini. Kwa sababu ukitema mate chini unamtubia Mwenyezi Mungu na kumuomba radhi kwamba haya niliyoyasema sio sahihi. Kwa hiyo, unamkumbusha mwenzio kwa kumwambia tema mate chini ili hayo aliyoyasema ayatubie kwa Mwenyezi Mungu kwamba Mwenyezi Mungu nisamehe. Kwa hiyo, niwaombe sana wenzetu ambao wana utaratibu wa kuzungumza mambo ambayo sio ya kweli wawe wanatema mate chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Serikali kwa jinsi ilivyoamua kujenga barabara ya kati kutoka Dodoma kwenda Iringa na kutoka Dodoma kwenda Babati. Kwa kweli kwa hili sisi wa mkoa wa Dodoma tunaishukuru sana Serikali na tunamshukuru sana Mheshimiwa Magufuli na mwenzake kwa kuthubutu kuanza kujenga ile barabara kwa sababu barabara hii ilikuwa ni kitendawili miaka ya nyuma sisi sote tumejifunza katika historia, jiografia lakini bado ilikuwa haijaamuliwa kujengwa, lakini mwaka huu inajengwa. Tunasema ahsante sana Serikali, ahsante sana Magufuli na mwenzako Naibu Waziri tunawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niikumbushe Serikali ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara ya lami kutoka Mbande kupitia Kongwa kwenda Mpwapwa. Naomba barabara hii msisahau kwa sababu ni katika zile ahadi za Mheshimiwa Rais. Lakini siku mkiamua kujenga ikafika Mpwapwa msisahau kwenda mpaka Kibakwe. Hili ni ombi rasmi na kuikumbusha Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ni ombi sawa sawa kabisa mpaka Kibakwe. *(Makofi)*

MHE. MARIAM S. MFAKI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Nitaendelea kuisemea mpaka nitakapomaliza Bunge hili miaka mitano yote. Nilichokuwa naomba niipongeze Serikali tena hata barabara zetu katika Mikoa na Wilaya kwa kweli Serikali imejitahidi kuzitengeneza. Ni kweli kwamba hata kama yapo mapungufu lakini machache, lakini Serikali imetimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa naomba tu kwamba katika barabara hizi za Mikoa na Wilaya hasa za Wilaya kwenye Halmashauri, tunaomba pesa zinapotolewa ziwe zinafika katika muda unaotakiwa ili ziweze kufanya kazi inayotakiwa na kwa wakati unaotakiwa.

Baada ya kusema hilo niendeleo kuisemea barabara za Dodoma Mjini. Kuna Mheshimiwa mmoja amesema juu ya barabara za Dodoma Mjini. Sina uhakika barabara za Dodoma Mjini huwa zinajengwa kwa ajili ya majaribio ili siku nyingine zibomelewe zijengwe tena au inakuwakuwaje labda Mheshimiwa Waziri nadhani anaweza akatueleza baadae. Kwa sababu ukiangalia barabara zilizoko Dar es Salaam, Mwanza na Arusha ni tofauti na za Mkoa wa Dodoma Mjini. Kama mnavyoona na ninyi wote mnasema kwamba mji huu unakuwa haraka, sasa tena tuje badala ya kubomoa vitu vingine tuje tena tuanze kubomoa barabara kwa sababu zimejengwa sio imara na kila wakati inakuwa ni bomoa bomoa ninyi wenyewe ni mashahidi barabara hii ambayo ipo karibu yetu hapa ikipewa mkandarasi ni kubomoa kujenga kubomoa. *(Makofi)*

Mimi nadhani sote tunazifahamu kwa hiyo, tuiombe Serikali hebu ibadilishe mawazo yake inapojenga barabara za Dodoma Mjini basi ziweze kudumu kama zilivyo za mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vilevile ni vizuri Serikali ikaanza kuweka utaratibu mzuri kwa ajili ya ongezeko la magari ili barabara zetu ziweze kupanuliwa mapema na ziendane na hali halisi ya maendeleo ya mji huu. Nina uhakika kama hatutaacha huo utaratibu wa kufanya vitu vya muda kwa mjini hapa barabara za muda nina uhakika baadae italeti shida. Halafu lingine labda Mheshimiwa Waziri atakuja kusema baadae kwamba hapa mjini hakuna barabara ambayo imeandaliwa kwa ajili ya magari makubwa. Nadhani wote tunajua jinsi magari makubwa yanavyopita katikati ya mji.

Niimbe basi Mheshimiwa Waziri kama kuna mahali ambapo pameandaliwa barabara kubwa kwa ajili ya magari makubwa ya mizigo ni vizuri basi barabara ile ikajengwa, kwa sababu zinapopita katika hizi barabara ambazo kwa kweli ni rahisi kuchakaa na wewe mwenyewe unajua wajibu wako kwamba barabara huaribiwa na magari makubwa na ndiyo maana maeneo mengine zimewekwa mizani kwa ajili ya kupima magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana hilo huwa tunatafuta, hivi haya magari ni wapi. Mara tuambiwe pale karibu na Kituo cha Mafuta cha Shabiby kwa nyuma pale ndio barabara ya magari makubwa inapita, watu waliowekewa X hatujui kama wamelipwa au hawajalipwa na mpaka sasa mpango huo umekaa kimya. Tunaomba hili nalo lifahamike na tueleweshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alikuwa anaelezea juu ya matuta ambayo yanapaswa kuwekwa katika gari ili kuzuia kijana wangu Lusinde alisema kwamba kuwekwa kwa ajili ya madereva wakorofi, mmesema yanaitwa *raster*. Sasa kuna mengine ambayo yanaanzia hapa Ujenzi barabara ya Mailimbili pamoja na kwamba yalilalamikiwa na wananchi, watoto walikuwa wanagongwa sana, yakajengwa matuta sasa sijui yamejengwa kwa kuwakomesha madereva au kwa kukomesha magari maana yake ni makubwa hata gari ikipita pale hata wewe mwenye gari unaumia.

Kwa hiyo, tunaomba haya matuta kama ni kurekebishwa yarekebishwe, yajengwe matuta ambayo kwa kweli ni usalama kwa wananchi na ni salama kwa wenye magari. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hili nalo aliangalie na aweze kulifanyia kazi ili matuta yale yarekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nizingumzie suala la ujenzi wa nyumba katika barabara na hasa wale ambao inashababishwa wakati mwingine kubomolewa. Kuna kitu ambacho kidogo huwa kinashangaza, mtu anaanza kujenga mpaka anafikisha mpaka nyumba inapauliwa, inakaliwa watu wanaiona, hakuna hata mmoja anayekwenda kumwambia wewe mwananchi unajenga mahali sipo ili kama ni kupata hasara apate hasara kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunamwacha anajenga, anamaliza kazi yake kama ni kazi ya biashara anafanyia biashara nyumba yake baadae anakuja kuambiwa wewe umejenga mahali ambapo sipo. Wananchi wetu bado kwa kweli sheria hazijawakaa kichwani na inawezekana kabisa wengine hawajui. Sasa niombe Serikali katika utaratibu wake kwamba kama kuna mtu anafanya makosa ya kujenga mahali sipo basi akatazwe mapema ili kumnusuru huyu mwananchi hela yake ambayo alitaka kukamilisha nyumba yake asikamilishe pale ahame akajenge mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja mia kwa mia na tutakiane kila la kheri katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan, sisi sote waislamu na wakristo wote ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi mchana wa leo nami niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza kabisa, napenda nitoe salamu zangu na kuwatakia heri Waislam wote duniani katika mfungo mwema wa Ramadhan. Pia nawatakie kheri Wabunge wote na viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi wa kitaifa heri ya Ramadhan, nawaambia *Ramadhan Karim*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema hayo, kwanza napenda ni-*declare interest* kwamba mimi ni mwathirika wa bomoabomoa ya Wizara ya Ujenzi katika eneo la Mbagala. Napenda kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa hiki kitabu chenye mipango mingi na iliyofafanuliwa vizuri. Kwa kweli mipango ni mingi na mambo ni mengi, bajeti ni kubwa na mambo yake sijui kama yatakuwa makubwa au madogo. Mwenyezi Mungu atajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi kwa Serikali yangu na Wizara ya Ujenzi, naomba salamu za kipekee ziwandee Waheshimiwa Wajumbe wangu wa *UWT* Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuweza kunichagua, siyo kwa ubora wangu, siyo kwa uwezo, bali Mkoa wa Dar es Salaam kwa dhamira wakisema mwaka huu Temeke lazima tuwape mwakilishi mwanamke na mwakilishi mwenyewe ni mimi Mariam Kisangi. Watu wa Mkoa wa Dar es Salaam walifanya hilo jambo, hawakufanya kwa makosa na mimi nawahakikishia kwamba nitawafanyia kazi kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika maeneo mawili. Nitachangia katika bomoabomoa na ushauri. Lakini pia naipongeza Serikali yangu kwamba angalau tatizo la Kivuko cha Kigamboni limepungua kwa kiasi kikubwa sana. Kwa kweli napenda nitoe pongezi zangu za dhati kwa hilo. Lingine, napenda niipongeze barabara ya Mandela. Barabara ya Mandela inaendelea kufanyiwa ukarabati mzuri na kama Wakandarasi wote tungewapata kama aliyekarabati barabara ya Mandela nafikiri Jiji letu la Dar es Salaam lingekuwa zuri sana. Lakini mimi nina masikitiko makubwa. Bajeti ambayo Mkoa wa Dar es Salaam umewekewa ya shilingi bilioni tano, *I don't know* au mimi sijui ni triloni kwa mipango ile iliyowekwa ya kuondoa msongamano Mkoa wa Dar es Salaam, pale hakuna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa sana, Mkoa wa Dar es Salaam. Tatizo la kubomoabomoa, Wizara hii nina imani kwamba ina washauri wazuri sana na imeajiri wahandisi wengi na ni wazuri. Lakini kabla *project* yoyote haijaanza, watu wanafanya utafiti. Hivi jamani, ule utafiti, si mnaweka kuna *plan one, two three, four!* Lakini nashangaa Wizara hii *plan one* bomoa, *plan two* bomoa, *plan three* bomoa, *plan four* bomoa. Jibu bomoa bomoa bomoa. *No*, haiwezekani. Kwa kweli hili suala la kubomoabomoa Serikali yetu tunaitia hasara kubwa sana na tunaweka manung'uniko makubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa kusini moto unapowaka tunakata majani mabichi kwenda kuzima moto. Sasa moto unaotuwakia sisi viongozi na wakazi wa *Kilwa Road*, sisi miti ya kuzimia moto ule unaowaka, imekwisha. Tunaiomba leo Serikali yetu ya kizalendo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyo makini leo ionyeshe umakini wake hapa kwa kuwataja wananchi ambao wamelipwa fidia kwenye barabara ya Kilwa na wale ambao hawajalipwa fidia kwenye barabara ya Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa, unaambiwa mtu kaifuata barabara, mimi ni mzaliwa wa Dar es Salaam. Nikianzia Kilwa Road pale bendera tatu, pale kuna majumba ya watu wa Serikali unapandisha mpaka Saba Saba, ukipandisha Saba Saba unakutana na nyumba ya akina Aziz Ali ambayo ilikuwa barabarani ndiyo wenye mji ule. Nataka nione kwenye orodha, ukoo wa Aziz Ali umelipwa? Lakini ukitoka pale kuna Sharrif Mwarabu, yeye yuko pale toka mimi niko mdogo nasoma Shule ya Msingi. Ukipandisha Mwembe Madafu kuna ukoo wa akina Shahame, wako barabarani, wamevunjiwa mpaka makaburi yao na nyumba zao kujenga barabara ya Kilwa na ukitoka pale ukipandisha Mtoni Mtongani kuna akina Mipango pale Msikitini. Hawa watu mimi nataka kuuliza, wamelipwa lini? Lakini ukishuka Mtoni pole bondeni, Mbagala Misheni lilikuwa shamba la mpunga la babu yangu Mzee Mwilu, Mwalimu wa Kwanza wa Kanisa la Katoliki lile la Mbagala. Shamba lile liko mpaka barabarani. Bibi yangu amedai haki yake Mahakamani mpaka kafa kaicha. Barabara imepita katikati ya shamba lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale Mbagala Saba Saba upande mmoja *KTM* upande mwingine kuna mzee mmoja kada sana, anaitwa Mzee Kapinga. Hawa watu wamelipwa? Ukipandisha pale Mbagala St. Anthony kuna ukoo wa Zame ambao ndiyo wenye eneo lile. Upande mmoja Shule ya Sekondari St. Anthony, nauliza kwenye hiyo orodha ambayo watu wamelipwa, hao watu wamo? Ukija Mbagala Kizuiani, wenyewe ni akina Safi ambao Mji wao ndiyo ule toka enzi za ukoloni. Nataka leo niulize Wizara hii imewalipa hawa? Lakini ukishuka ukija Mbagala Rangi Tatu kuna Mzee Ngulangwa yupo pale miaka na miaka mimi nazaliwa nakua namwona. Mji wao ni Mbagala Rangi Tatu barabarani, hawa wamelipwa? Lakini pia familia ya Kisangi ipo hapo barabarani, nyumba tumeachiwa urithi na baba yetu, yeye amekufa mwaka 1989 utaniambia mimi nimeifuata barabara? Nauliza leo hapa Wizara hii leo injibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mzee Sinde ambao wao ni wenyeji wa mji ule, tunaambiwa watu wamefuata barabara. Nataka niulize mimi hizi familia ambazo nazitaja zimelipwa, kwa sababu wazee wametuachia majumba yale wenyewe wamekufa. Sasa leo nataka niombe Serikali yangu ambayo ni sikivu, hebu leo itoe jibu moja la msingi. Tumechoka kuzungushwazungushwa, tukija huku tunaambiwa tulifuata barabara, tukija huku tumefuata barabara. Hatutaki! Leo tumechoka kuzima moto! Leo ukimwona mwenzio ananyolewa na wewe tia maji. Watu tumesema Bungeni, hatupati jibu la msingi, matokeo yake wanaona Mbunge hafai, wanaona Diwani hafai. Kwanini Serikali yetu wenyewe inatufanyia vitu vya aina hii? Hii ni dhambi ya kubaguana ambayo aliisema Mwalimu Nyerere. Hii ni dhambi mbaya kwa sababu leo wanamkataa Mbunge eti kwa sababu hasemi Bungeni suala lao. Kumbe Wabunge tunasema, uamuzi hakuna. Tufanye nini? Lakini leo msimwone Mbunge anakataliwa au Diwani wangu Mama Macha anakataliwa na huyo anayesababisha haya mambo iko siku. Hayana mmoja haya ndugu zangu. Leo mimi naiomba Serikali, nataka wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam ambao hawajalipwa fidia zao walipwe na leo Serikali hii itoe jibu ambalo litawafanya watu wafunge Ramadhan zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nataka nitoe ushauri. Ninakariri Hotuba ya Mheshimiwa Rais alisema Wizara zote zifanye kazi kwa pamoja na kwa ushirikiano. Lakini leo watu wanaambiwa, umebomolewa nyumba nenda Mahakamani. Jamani mimi Mahakimu wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam wamechoka na watu wanajaa kibao Mahakamani, hata Hakimu anakosa hewa. Hivi kwanini nyie wenye Wizara hii msitafute usuluhishi mpaka mnamamisha vitu huku mnapeleka huku? Hatuoni kama tunaiingizia Serikali hasara? Jamani nawaomba, hebu tuwe na uchungu na hii nchi na tuwe na uchungu na hawa watu wetu. Hawa watu sisi wengine ndiyo waliotuleta hapa madarakani. Tumekuja hapa madarakani ili tuwatetee. Sasa tunapouliza jambo tujibiwe kwa umakini, tusijibiwe kama unanijibu mimi Mariam Kisangi. Leo wakazi wote wako kwenye *screen*, wote wameagiza na wanataka jibu na nina *message* zaidi ya 200. Wanasema leo hatima yao iko mikononi mwenu Wabunge.

Mheshimiwa Dr. Ndugulile ni Mbunge wangu mahiri, kijana mdogo, kaingia juzi, leo afanyiwe fujo, kwanini? Mheshimiwa Mtemvu ni kaka yangu anaeleza, lakini kila analosema linashindikana, watu wafanye nini? Wanakimbia mara hawa wanakwenda kwa Rais, mara wapi, kwanini tunamwongezea kazi Rais wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Wilaya ya Kinondoni nimesoma hapa, barabara ya Kawawa itatengenezwa na kuna fungu la kulipa fidia. Haya maneno yawe ya kweli, tutakuja kugombana hapa. Nasema hivyo kwa sababu *Kilwa Road* iliambiwa hivyo hivyo kwamba barabara ile na wakazi wote watalipwa fidia. Hatujaiona mpaka leo na haya huku Kinondoni nataka yawe ya kweli. Vinginevyo kitabu hiki mimi nitabaki nacho mpaka mwakani nije niulize.

Pia naomba ule upanuzi wa barabara za pembezoni, ile barabara ya Mbezi – Malamba mawili mpaka Majumba Sita, kwa kweli barabara ile ni nzuri sana iwapo itaboreshwa. Hata sisi wenyewe Wabunge itatusaidia tunapotoka Dodoma, msongamano wa magari mkali, unakata huko dakika zako tano uko *airport*. Lakini pia ile barabara ya *Jet* nayo naomba iongezwe kasi na ikiwezekana iongezwe, itokee Kilungu mpaka Zansa Mbagala. Kwa sababu Mbagala kama darajani pale pana *shortage* ya aina yoyote hakuna kwenda mjini, vinginevyo tupate hilo Daraja la Kigamboni au uzunguke kule. Ni sehemu ambayo ni hatari. Lakini hiki kibarabara kikitengenezwa vizuri hicho cha kupita Nzasa – Jet – Buza mpaka *Airport* itasaidia.

Pia niombe Serikali yangu katika kuadhimisha miaka 50 ya Uhuru basi ile barabara ya Uhuru nayo tuipe kipaumbele. Imebeba jina na dhana yenyewe ya Uhuru. Ifanyiwe marekebisho hasa ili tuangalie hiyo dhana ya miaka 50 tumeifanya kweli. Lakini pia niombe Serikali yangu sikivu, hebu tujaribu, kila Wizara ina Maafisa Uhusiano sijui Maafisa Ushauri, hivi kwanini wanashindwa hata mtu mmoja kwenda kutusaidia kuuzima ule moto wa Mbagala kule? Wanashindwaje wakati ndiyo kazi yao walioajiriwa? Nishauri sasa, cha msingi sasa hivi kuna kozi za usuluhishi wa migogoro katika Vyuo vyote Vikuu. Naomba mkawajengee uwezo wale Maafisa Uhusiano, wawe wanakuja kusaidia hizi kesi badala ya kupeleka Mahakamani. Mahakimu wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam wanachoka na kesi za kujitakia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba leo hapa ni Mheshimiwa Waziri anipe jibu moja. Nataka uniambie *Kilwa Road* italipwa leo au hailipwi? Vinginevyo Mheshimiwa Waziri, mshahara wako unaondoka, shilingi leo inaondoka, hapa hakitabaki kitu. Mheshimiwa Waziri usicheke, leo mambo hapa! Nakuomba chondechonde, au nilie? Nakuomba uwafanyishe watu waweze kufunga Ramadhan vizuri na Mungu akipenda wacheze Idd, wafurahie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitimiziwe haya mambo yote. Nikitimiziwa haya mambo yote ninayoyataka au nikisikia jibu japokuwa kasungura kadogo, lakini watu wanahitaji jibu lenye faraja. Nikiona hivyo, hapo nitauunga mkono hoja yako. Lakini kwa sasa hivi Mheshimiwa Waziri uliangalie hilo na lingine nimeona huku kuna wengine wanajengewa stendi. Hivi pale Mbagala mwisho mnakuonaje? Vurugu tupu, lakini na mimi nalala palepale wataniua. Mbunge wa Kwanza kutoka Wilaya ya Temeke mwanamke, lakini naweza kuwa wa kwanza kufa kwa sababu ndiyo nawakalia hapo hapo hao wenye shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, muda wako umeisha. Kweli leo Mariam Kisangi huko *TMK* bila shaka wamekusikia. Maana unazijua koo zote za kule na wewe ndiyo mwakilishi wa kweli. Sina hakika kama Mheshimiwa John Mnyika anaweza kutaja hata koo mbili za Ubungo. Tuendeleo, Mheshimiwa Ole Sendeka.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Ole Sendeka.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68. Nimesimama kuomba mwongozo wako katika hatua hii.

MWENYEKITI: 68 ngapi?

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7). Nimesimama kuomba mwongozo wako kufuatia Hotuba ya Waziri wa Ujenzi - Dr. John Pombe Magufuli ya mwaka huu inayoashiria na kuweka rekodi ya kuendelea kuonyesha ubaguzi katika ugawaji wa barabara za lami katika nchi hii na kudhihirisha wazi kabisa kwamba Serikali inavyofanya kazi sasa na kwa miaka ya karibuni, inafanya kazi katika mtizamo unaoonyesha kwamba Serikali imeanza safari kuelekea kwenye kifo chake.

Kutokana na sifa moja kubwa nitakayoitaja, kwamba barabara zilizogawanywa katika nchi hii zinatazama maeneo walikotoka viongozi wakubwa na walioko katika vikao vya maamuzi na wanakotoka Watendaji Wakuu wa Serikali na ukitaka nitatoa mfano. Ndiyo maana nathubutu kusema Serikali inafanya kazi kana kwamba imeanza safari ya kuelekea kwenye kifo chake na kusahau barabara inayokwenda Butiama na kusahau barabara inayotoka KIA inakwenda Mererani kujengwa kwa kiwango cha lami. Lakini ukienda kwa jirani zangu Mkoa wa Kilimanjaro karibu kilomita 300 zinajengwa kwa kiwango cha lami katika mazingira ambayo Mkoa wenyewe una ukubwa wa Wilaya ya Simanjiro. Lakini kilomita tano, kumi za kutoka KIA kwenda Mererani kwa kiwango cha lami, barabara inayokwenda Butiama kwa Mwalimu Nyerere hazipo kwenye mpango. Inaashiria wazi ubaguzi uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelekezo yako kwamba katika hatua hii ambayo bajeti haikidhi matarajio ya Watanzania, imekaa kibaguzi. Tuchukue hatua gani ili tuweze kuifumua bajeti hii izingatie maslahi mapana ya nchi, izingatie maslahi ya maeneo mengine ambayo wanatoka pia watu wasiokuwepo kwenye vikao vya maamuzi kwenye Serikali hii? Nimesimama kuomba mwongozo huu kwa sababu hotuba hii inakera na inaonyesha kiasi gani ubaguzi uliokithiri katika Wizara hii na hasa katika Sekta ya Miundombinu na TANROAD walivyogawana miradi kutokana na wao wenyewe walikotoka na wanakotoka wakubwa wa Serikali ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mwongozo nilioombwa leo ni mkubwa kuliko wa siku zote, lakini maamuzi kuhusu mwongozo huu yatatolewa wakati wowote kadri tutakavyoona inafaa. Inaweza ikawa siyo leo, inaweza ikawa hata kesho. Tuendeleo.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mwongozo, Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kanuni ya 68 kuhusu utaratibu na mwongozo wako kwamba...

MWENYEKITI: Utaratibu na Mwongozo haviombwi kwa pamoja.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wako samahani. Kwamba je, tunaruhusiwa katika Bunge hili kuweka vitambaa juu ya meza kama kile kinachoonekana na sisi kama CHADEMA tuje na vitambaa vyetu tuweke juu ya meza? Naomba Mwongozo wako kuhusu hilo.

MWENYEKITI: Mwongozo nitautoa baadaye, tuendeleo. Mchangiaji anayefuata ni Mahmoud Mgimwa.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kidogo katika Wizara hii ya Ujenzi. Awali ya yote naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Mufindi kwa ushirikiano wanaonipa wakati wa kutekeleza majukumu yangu ya kibunge katika Jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wa Wizara hii ya Ujenzi kwa kazi nzuri ya kusimamia vyema Sera na Ilani ya Chama chetu. Sasa hivi Tanzania inapitika katika Tanzania yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali yetu kwa jinsi ilivyoweza kuboresha barabara nyingi katika nchi hii. Kwa mfano, zamani ilikuwa kazi ngumu sana na ilikuwa safari ndefu kutoka Iringa kwenda Dar es Salaam, ilikuwa inachukua zaidi ya siku moja na nusu, lakini sasa hivi tunahesabu masaa saba tu. Hayo ni mafanikio makubwa na ni mafanikio ya kujivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kumpongeza sana na kumshukuru Rais wetu mpendwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutimiza ahadi yake wakati wa kujinadi mwaka 2010 alituahidi kutuletea lami katika Wilaya yetu ya Mufindi. Nataka niseme, hili jambo linatekelezwa na sasa hivi lami inaletwa katika Wilaya yetu ya Mufindi. Nashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri Serikali yetu iliyotufanyia, bado zipo changamoto. Napenda kuzungumzia barabara kuu tatu ambazo zipo katika Jimbo letu la Mufindi Kaskazini. Barabara ya kwanza ni ya kutoka Kinyanambo 'C' kupitia Itimbo, Ihalimba, Usokami, Mapanda mpaka Msusa, Wilaya ya Kilombero Mkoa wa Morogoro. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Kwenye barabara hii ndipo tuna sehemu kubwa ya msitu, barabara hii ndiyo inayotuongoza kutupeleka bwawa la Kihansi, kwenye barabara hii kuna utalii mkubwa kwani kuna vyura ambao hawawezi kupatikana katika sehemu yoyote duniani, lakini jambo la kusikitisha, barabara hii imesahaulika na imeachwa kabisa haishughulikiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejitahidi kuuliza swali katika siku zilizopita lakini majibu ya swali lile yalikuwa ya kisiasa zaidi, kwa wakati wangu nilimfuata Naibu Waziri wa Ujenzi Dkt. Mwakyembe nikamueleza hali halisi iliyopo katika barabara hii, mpaka leo sijapata majibu ya kueleweka. Nataka niseme kwamba watu wa maeneo yale wanapata shida kubwa sana, wanatembea zaidi ya kilomita 50 kwenda kutafuta usafiri, wanasafirisha maiti kwa kutumia pikipiki kwa sababu barabara haipitiki mwaka mzima. Kwa hiyo, ni lazima nikiri na lazima niseme kwamba sitakuwa tayari kuiunga mkono hoja hii mpaka nipate maelezo ya kina, *otherwise* na-*declare* kwamba nitatoa shilingi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya pili ninayopenda kuizungumzia ni barabara inayotoka Kinyanambo 'A' kwenda Sadani mpaka kwenda Madibila Mkoa wa Mbeya. Barabara hii iko kwenye mradi wa kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini mwaka 2004 Serikali iliagiza nyumba zote ambazo ziko karibu na barabara zibomolewe kwa barua ya tarehe 26 yenye Kumbukumbu Namba *TRD.RM/IR/R10/145/71*, wananchi wengi wazalendo waliamua kuvunja sehemu ya yale maeneo waliyopewa maelekezo, lakini juzi umekuja mpango mpya kwamba wale ambao walikaidi kutekeleza zoezi hili Serikali imeamua kuwapa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea malalamiko ambayo yanatuletea taabu katika eneo lile, watu ambao waliamua kutoa nyumba zao kwa hiari yao wenyewe hawapati nafasi ya kulipwa. Kwa hiyo, namwomba Waziri aje kwenye eneo hili ili kusudi apate nafasi ya kuongea na wananchi, wawaeleze nini cha kufanya. Je, wana haki ya kupata fidia? Wale ambao kwa hiari yao waliamua kuanza kuzivunja zile nyumba inatuletea taabu sana jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya ni Lugoda, Lutali, Utosi, Tambala Ng'ombe na Kinyanambo. Namwomba sana Waziri na Naibu Waziri waje kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu nililotaka kulizungumzia ni barabara ya kutoka *Jos Coner* Mafinga. Barabara hii ni ya Mkoa na inafanyiwa matengenezo kila mwaka, lakini kuna jambo moja linasikitisha sana. Kama Serikali ingekuwa ina dhamira ya kweli kwamba kila mwaka ingekuwa inatengeneza hata kilomita mbili au kilomita tatu kwa kiwango cha lami, barabara hii ingekuwa imekwisha. Lakini tunatumia hela nyingi sana kila mwaka kufanya matengenezo yale yale. Hii imekuwa kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iache utaratibu huu kwa sababu eneo hili ni *very sensitive* ambalo lina viwanda vingi zaidi ya viwanda nane vipo katika eneo hili, ambavyo vinachangia hela nyingi sana katika pato la Taifa. Ninaomba Waziri na Naibu Waziri waliangalie sana jambo hili. Hatuhitaji barabara ile iendeleo kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara, tunataka barabara ile ianze kuchukua kipande kwa kipande. Wachukue kilomita mbili mwaka huu na mwaka unaokuja wachukue kilomita mbili na baada ya miaka mitano tutakuwa tumefika eneo kubwa la barabara ya lami ambayo itakuwa inaweza kupitika ambayo itakuwa haihitaji kuiingiza Serikali katika gharama yoyote. Inaonekana kwa njia moja ama nyingine pana utapeli unafanyika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ninalotaka kuzungumzia ni suala la stendi, Wilaya ya Mufindi ni Wilaya kubwa sana, lakini hatuna stendi. Kukosa stendi inatuathiri sana. Katika kitabu cha bajeti ya Waziri hakuna hata sehemu moja ambayo ametenga fedha kwa ajili ya Wilaya ya Mufindi. Hii inasikitisha na inatumiza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, natamka rasmi kwamba sitakuwa tayari kuiunga hoja mkono mpaka nipate ufafanuzi wa maeneo hayo husika. Hii imeonekana ni kero na inaonekana kuna upendeleo katika baadhi ya maeneo na kuna baadhi ya maeneo tunaonekana kama siyo Watanzania na kama siyo Wazalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwatakia kila la heri ndugu zangu Waislamu ambao wapo katika Mfungo wa Ramadhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mgimwa kwa kutumia muda vizuri. Sasa nitamwita Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumpongeza Waziri, lakini yapo mambo machache ambayo ningependa niyachangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti yetu ni nzuri, barabara zinazojengwa ni nyingi sana, lakini liko tatizo kubwa sana la madeni. Ningependa Waziri atakapokuja na kwa kweli Serikali, maana nikisema Waziri peke yake madeni tuliyonayo ni makubwa sana. Leo hii ukienda kuuliza pale tunadaiwa siyo chini ya Shilingi bilioni 434 na wakandarasi. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye maamuzi na ningependa nitoe mawazo kwamba tusiogope, twende tukakope kwenye mablenki ili tukalipe deni hili. Tusipolipa leo, kadri zinavyozidi kukaa, maana yake zinaendelea kuongezeka kwa maana ya *interest*, sijui kuna *idle time*, yote haya wanaoumia ni sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeiomba Serikali kwenye hili tufanye maamuzi hapa waende wakakope ili tulipe tuanze upya. Kwa sababu hali ni mbaya sana mimi ninavyoiona, tunapitisha bajeti hii, tunaisifia ni nzuri, lakini kwa ukweli inakwenda kulipa madeni yote. Kwa hiyo, ningeiomba sana Serikali itusaidie na ili tusipate madeni, tena ninawaomba wenzetu wa Serikali tuanze kuheshimu matumizi ya fedha. Kama hatuna fedha, hatuna sababu ya kusaini Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunavyoongea, kwa watu tunaokwenda Tabora wakandarasi wapo *site* kutoka Tabora kwenda Urambo, lakini kazi hawafanyi hawana pesa. Kuna kandarasi wanatokea hapa Manyoni kwenda Tabora, tunawashukuru, lakini wamepaki, hakuna pesa. Tabora-Nzega kuna wakandarasi, tunawashukuru, wamepaki hakuna pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana watu wa Serikali mumsaidie Waziri, zipatikane pesa, tulipe madeni haya na wananchi watatuelewa. *Otherwise* wataona kama tumeamua kufanya mchezo wa kuweka Wakandarasi waone Wachina wanaozunguka pale, lakini hakuna kazi inayoendelea. Naomba sana hili tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la kukuza uchumi wa nchi yetu, pamoja na kwamba tunajenga barabara, mimi naomba sana hili jambo ni la kisera tufanye maamuzi sasa. Sasa hivi tunajenga barabara nyingi sana kwa kutumia pesa za kwetu. Maana yake tunajinyima

kama Watanzania kutoka kwenye kodi ili tujenge barabara. Lakini tunachokifanya sasa ni kweli tunapata barabara, lakini zile pesa tulizojinyima tunazipeleka China, na tunapeleka nje. Maana yake ni nini? Inabidi utafute dola kuwalipa Wachina, matokeo yake Shilingi inaanguka kila siku, tunaulizana hapa, lakini haya ndiyo mambo yanayochangia kuanguka kwa shilingi kwa sababu inabidi ununue dola uweze kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepomba Serikali tuamue, tunasema kwamba wewe Mchina unataka kujenga hapa kwetu, ndiyo; lakini ni lazima uingie *joint venture* na mtu wa Tanzania, tukianzisha *joint venture* nyingi tukawapa Watanzania, pesa zitabaki hapa ndani, zitakuza uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, tutaanza kuwafundisha Watanzania hawa *culture* ya kufanya kazi. Maana wanakuja Wachina wanalala njaa, wanafanya kazi ili Waswahili waanze kuona umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii. Lakini pia kuna suala la kupata ujuzi, *technological transfer* hii ndiyo itakayoweza kuokoa na kuipeleka nchi yetu mbele sana. Namwomba sana Waziri tusifanyie mzaha suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema suala hili? Nchi zote, Taifa kubwa la Marekani juzi lilikuwa na mdororo wa kiuchumi. Moja ya njia ya kuokoa mdororo ule wa kiuchumi ilikuwa ni kujenga miradi mingi ya *infrastructure*, lakini wanaojenga ni watu gani? Ni Wamerekani wenyewe ili waweze kutoa kazi na hela zibaki pale ndani. Kwa hiyo, ningepomba sana Serikali watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, naipongeze Serikali kama mtu wa Kigoma, Serikali imefanya kazi kubwa kwa ajili ya Kigoma. Wapo wenzangu hapa, bahati mbaya Kigoma siku hizi...

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Samahani Mheshimiwa Mbunge. Mimi nadhani Mheshimiwa Mkono tungeacha amalize kuchangia, akishamaliza halafu utaomba hicho unachotaka kuomba. Mheshimiwa Serukamba endelea.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuishukuru Serikali kwa miradi inayoendelea Kigoma. Kigoma tupo wengi, kuna watu wanataka kusema ni wao, lakini maamuzi ya kujenga barabara za Kigoma yalifanyika mwaka 2006, tukafanya kazi, programu ya kazi ikaanza, na sasa unaweza ukaona tuna daraja la Malagarasi, kuna kilomita 48, tunajenga sasa kuja Tabora, tumekwenda Manyovu na sasa tumebakiza barabara ya kutoka Kidahwe kwenda mpaka Nyakanazi. Katika hili naomba niseme, Waziri atakapoamua kuanzia, tunachotaka sisi ni barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara ya kwenda Kanyani mpaka Mpanda, tunaomba na hiyo ianze, lakini pia tunayo barabara ya Kasulu kwenda Mnanira, barabara ile nitakwambia uzuri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfanyabiashara wa Burundi ukimwambia anatoka Dar es Salaam akifika Kasulu aende Mananira aende Burundi atakuwa ame-*serve* kilomita 150 kuliko kufika mpaka Kigoma. Kwa hiyo, kwa maana ya uchumi ni muhimu sana tuanze kujenga barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi Mzee Chenge alisema vizuri sana hapa, kwamba nchi hii tuiangalie, tuanze kujenga barabara kwa kuiunganisha, tuunganishe Mikoa, tuunganishe Wilaya. Lakini maana yake ni nini? Leo ukienda Rukwa, mahindi ni bei rahisi sana, lakini mahindi yale hayawezi kufika Tabora kwa sababu hakuna barabara, hayawezi kufika shinyanga, Mwanza kwa sababu hakuna barabara. Kwa hiyo, ni lazima barabara hii ya kutoka Rukwa uone umuhimu wake wa kuileta huku. Kule Kigoma ukienda Ilagala tuna mpunga, tuna kila aina ya mazao huwezi kuyafikisha kwa sababu hakuna barabara. Kwa hiyo, ni lazima sasa kwa maana ya maendeleo tuanze kuunganisha nchi hii katika mpango ambao hawa wanasaidia hawa ndiyo namna ambavyo tunaweza kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo mimi nimeli-*observe* ambalo ninaona taabu sana na sijui hili ni la kiserikali zaidi, ukiangalia Wizara ya Ujenzi na vitengo vyake, angalia *TANROADS*, mainjinia wale baada ya miaka minne ijayo asilimia 75 watakuwa wamestaafu. Kwa hiyo, naona taabu kama Taifa tunakwenda wapi, kwa sababu tulikaa muda mrefu. Ni lazima tufanye maamuzi sasa, kwamba tunafanyaje? Ukienda Wizara ya Kilimo wale ma-*researcher* wote wanakaribia kustaafu. Ukienda Maji mainjinia wote wa maji wanakaribia kustaafu. Hili ni jambo kubwa, tulifanyie kazi kama nchi, na ili tuendelee ni lazima uwe na *human resource* ya kukusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni suala la bei za barabara. Bei za barabara Tanzania ni kubwa sana ingawa zimeanza kushuka. Namshukuru Waziri, lakini naomba uangalie eneo moja, tunalo pale kwenye *design*, (*detail engineering design*) pale ndipo ambapo tunapopigwa bao. Wale ma-*consultant* tunaowapa kufanya kazi akishakwenda kilomita 100 anafanya *sampling* sehemu tatu, ana-*generalise*, lakini mwisho wa siku sehemu nyingine hakuna maji, sehemu nyingine kuna *swamp*, sehemu nyingine udongo mzuri, anakuambia kote hapa *a big part* kuna *swamp*. Matokeo yake gharama ya barabara inakuwa kubwa sana. Ninawaomba Watu wa Wizara ya Ujenzi, wako vijana wengi wamesoma, kila *design* ikishaletwa kabla hatujatangaza tuifanyie *review*, waende wakaone hayo maeneo. Upo uwezekano unaweza ukaambiwa kuna madaraja kumi, kumbe yatakatoyojengwa ni manane. Tuta-*serve* pesa nyingi sana kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi nina-*dought credibility* ya mainjinia, la hasha. Lakini ninachokiongelea mimi, nataka tuanze kwenda vizuri ili pesa kidogo tulizonazo tuweze kufanya maeneo mengi sana. Unaweza ukaona Wabunge wote hapa kila mtu anataka barabara. Kwa hiyo, ni lazima sasa tuanze kuangalia kila maeneo tunapoweza kupunguza tupunguze ili tuweze kupata barabara nyingi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwenye eneo hili, ni la muhimu sana na huku ndiko ambako kote, maana wao wanajua yule aliyefanya *design* unaweza kukuta mwingine ndiyo huyo huyo anakuja ku-*supervise*. Kwa hiyo, anajua anakwambia hapa niliweka hiki, lakini kama tutakuwa tume-*review* sisi, unasema *no*. Barabara hii tutafute namna tunavyoweza ku-*maximize* ile *engineering design* ili tuweze kupata barabara nzuri na barabara zetu ziweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali mwaka huu kabla haujakwisha, barabara ya Kigoma kwenda Nyakanazi na yenyewe tuwe tumetangaza ili tupate mtu wa kujenga barabara hiyo. Naomba kabla ya mwaka huu haujakwisha, ikiwezekana barabara ya Kasulu kwenda Mnanila kilomita 42 ambazo ni chache sana ninaamini ukiamua unaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nampongeza Waziri kwa kazi kubwa, lakini naomba mambo hayo niliyoyasema yafanyiwe kazi ili tuweze kuona tunavyoweza kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

TAARIFA

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(8): "Vile vile Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa na kwa ruhusa ya Spika, atatoa taarifa au ufafanuzi kwa Mbunge anayesema ambapo Spika atamtaka anayesema aketi kusikiliza taarifa hiyo."

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge endelea.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mbunge anaeleza hoja yake hii, Mbunge msemaji wa mwisho aliyemaliza kusema, alisema anaomba Serikali iwape fedha waweze kumaliza miradi fulani fulani. Kwa taarifa zilizotoka nyuma huko, Rais alisema kwamba nchi hii inakopesheka. Wanaandaa mkakati wa kupata *Bond* za kuweza kukopa aweze kufanya miradi mbalimbali. Kwa kuwa, barabara ya kutoka Makutano kwenda Serengeti kupitia Butiama

imebaki pale kwa miaka zaidi ya 40: Je, isingekuwa wakati muafaka sasa kukopa hizo fedha ili waweze kujenga barabara waliyomuahidi Mwalimu tangu akiwa hai mpaka leo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, sasa hii taarifa sijui anapewa nani. Lakini bila shaka Mheshimiwa Serukamba ameipokea taarifa na Serikali imepokea taarifa hii. Waheshimiwa Wabunge tuendeleo.

Sasa nitamwita Mheshimiwa Fatma Mikidadi bila shaka kama nitabakiwa na dakika chache, basi nitamwita Mheshimiwa Mntangi.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia mada iliyopo mbele yetu hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani za dhati kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa namna moja au nyingine wameniwzesha mimi kuwa Mbunge na kuwepo hapa leo, na kuwa mtu mbele ya watu na wote mnafahamu hilo, ahsante sana. Vile vile namshukuru mama kwa kunivumilia wakati wote nipo huku, yeye anaumwa, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nianze kwa kumshukuru Rais kwa kupata Urais na kuweza kuongoza nchi hii kwa makini kabisa na nampa hongera nyingi sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kazi kubwa anazozifanya katika nchi hii za barabara. Wote mnashuhudia jinsi gani sasa hivi ambavyo barabara zinaendelezwa katika nchi hii vile vile kwa kuleta hii bajeti nzuri sana. Bajeti nzima imejaa takwimu karibu nusu nusu, nusu maelezo, nusu takwimu, kwa kweli amefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishukuru Serikali, kwa kweli imefanya kazi kubwa sana ya kutengeneza barabara za Mkoa wa Lindi. Siku za nyuma kwa kweli Lindi tulikuwa hatuwezi kufika kwa siku moja. Lakini siku hizi tunaweza kufika kwa siku moja. Lakini naomba Serikali kipande cha Kibiti – Lindi, kipande kidogo cha kilometa 60 Ndundu – Somanga mpaka sasa kile kipande hakijakwisha na hivyo kuifanya safari ya kutoka Lindi kuja Dar es Salaam kuwa ndefu sana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali sana kipande hiki cha kilometa 60 kilichobaki cha Ndundu – Somanga kiweze kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningiomba Serikali isimamie kwa dhati kabisa kipande hiki kwa sababu ni kipande korofi, kwa sababu ndiyo kipande kilichobakia, ndio kipande chenye majambazi wengi. Kwa hiyo, naomba Serikali isimamie kwa dhati kabisa kuwasimamia wale wanaotengeneza barabara ile korofi kwa sababu imechukua muda mrefu tangu mwaka 2008 mpaka leo kipande cha kilometa 60 tu kimebaki. Sasa tunaomba Serikali isimamie kwa dhati kwa sababu inapofunguka barabara ya Kibiti – Lindi itafungua sehemu zote Kaskazini mpaka Kusini, Mashariki mpaka Magharibi. Vile vile itafungua biashara ya Kusini, Afrika Kusini, watakuwa wanakuja katika nchi hizi bila wasiwasi kupitia *shortcut*. Nchi nyingine za Zimbabwe na Malawi na *Mozambique* watakuwa wanakuja kwa urahisi katika maeneo mengine nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali isimamie kwa dhati sana kipande hiki cha Kibiti – Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije sasa kwenye ahadi za Rais. Kulikuwa na ahadi wakati wa uchaguzi na ningiomba sana ahadi za Mheshimiwa Rais na ahadi za *TANROADS* ambazo zimeahidiwa katika Mkoa wa Lindi, hata kama siyo kwa mwaka huu, lakini bajeti ijayo waweze kutifikiria kwa sababu Wilaya nyingi za Mkoa wa Lindi hazina lami. Tuliahidiwa Ruangwa Mjini, lami kilometa mbili. Tuliahidiwa Nachingwea Mjini lami kilometa tatu, tuliahidiwa Nachingwea Masasi lami, vile vile tuliahidiwa Kijiji kimoja kinaitwa Singino kwenda Hospitali ya Kilwa Kinyonga, pia tuliahidiwa. Vile vile *TANROAD* waliahidi lami pale Rwangwa Mjini, ukiachia ahadi ya Rais, Ruangwa Vijijini. Kwa hiyo, tunaomba ahadi hizi ambazo zilitolewa kwa Mkoa wa Lindi ambao ni Mkoa masikini tunaomba tusaidiwe angalau ziweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye suala la barabara za *OPEC*, nchi zinazouzwa mafuta duniani ziliahidi kusaidia nchi maskini duniani (*HIPC*) *Highly Indebted Poor Countries* katika nchi hii. Mikoa hiyo naomba ninukuu, ilikuwa ni Lindi, Singida, Rukwa, Kagera, Kigoma. Hizi ziliahidiwa barabara kiwango cha changarawe. Mkoa wa Lindi tuliahidiwa kilometa 200. Lakini kutokana na kuchelewa kwa kufunguliwa kwa tenda na mambo mbalimbali bei za vitu zilipanda bei. Kwa hiyo, kutokana na hilo sasa, barabara hizo hazikuweza kwisha kutengenezwa. Kuna baadhi tu, kuna kilometa chache tu ambazo ziliweza kutengenezwa. Sasa tunaomba kilometa zilizobakia ambazo mpaka sasa zipo hazijawekwa changarawe. Tunaomba tafadhali barabara hizi zimalizike. Bado Tingi – Kipatimu bado kilometa 18 bado Nachingwe – Kilimarondo kilometa 30 bado Liwale – Nachingwe kilometa 17.

Hii ya Ruangwa ingawa imekwisha, lakini bado ina mashimo na siyo nzuri. Sasa tunaomba hizi barabara katika Mkoa wa Lindi za *OPEC*, *HIPC* basi ziweze kumalizika. Tafadhali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye suala la barabara zilizopandishwa daraja. Mwaka 2007 tulitunga sheria ya kupandishwa hadhi. Sasa barabara hizi bado siyo nzuri ingawa zimepandishwa daraja. Tunaomba sana barabara ya Kilanjelanjie inayokwenda mpaka Nanjilini mpaka Ruangwa hii barabara kwa kweli pamoja na kwamba imepandishwa hadhi, lakini hela zinazotolewa kwa ajili ya kutengeneza barabara hii ni kidogo tu. Tunaomba tupewe nyingi ili iweze kupitika kifuku na kiangazi kwa sababu ni barabara ambayo ina mazao mengi kama ufuta, *gypsum* ina mambo mengi tu katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika upandishaji hadhi wa barabara, hapa tunapandisha barabara zile tu ambazo zinaunganisha Wilaya kwa Wilaya, lakini hili liangaliwe upya. Kuna barabara nyingine ambazo haziunganishi Wilaya hadi Wilaya, ambazo ni nzuri, ni kubwa zinaleta mazao, zinaleta vitu vingi, lakini hazipandishwi daraja. Kwa hiyo, tungeomba suala hili liangaliwe upya. Siyo lazima ziunganishe Wilaya hadi Wilaya au Mkoa hadi Wilaya. Tuangalie barabara zile ambazo zina manufaa kwa wananchi ndipo tuweze kupandisha daraja. Kwa mfano, kuna hii barabara ya Nachingwea – Chiola – Ruangwa, tungeomba ipandishwe hadhi. Kuna barabara ya Nyangedi – Rondo – Mandawa tunaomba barabara hii ipandishwe hadhi vilevile. Kuna barabara ya Mchinga – Kijiweni, Jiwe la Mzungu, Rushungi, barabara ya Liwale – Kilimalondo, Tunduru tungeomba sana ipandishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika madaraja. Sasa hivi magari ni mazito, madaraja yanayojengwa kwa mbao inakuwa ni matatizo sana. Tungeomba sana tuangalie madaraja yetu yajengwe kwa sementi na nzege badala ya kujengwa kwa mbao. Hasa barabara za vijijini. Hilo ni ombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nije kwenye suala la msongamano wa watu barabarani Mjini Dar es Salaam. Pamoja na jitihada za Serikali za kuweza kutengeneza barabara za *flying over*, nafikiri tungeweza kutumia njia zile ambazo wenzetu wa Afrika Kusini, Harare wanazitumia, reli ingetusaidia sana kwa sababu miundombinu tunayo, tunazo *stations*, tunayo mabehewa, tunavyo vituo mbalimbali, tungetumia reli kwa maeneo kama Miji ya Ubungo, Tabata, Mabibo, Buguruni, Yombo Vituka, Tabata Reli angalau asubuhi na jioni kwa kutumia reli. Kwa sababu miundombinu yote ipo, kwa nini tusifanye hivi wakati tunasubiri masuala ya *flying over* na mengineyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie suala la barabara za vijijini. Barabara za vijijini ni barabara zinaleta manufaa makubwa sana. Tuangalie tena upya tuwawezeshe wenzetu wa Halmashauri waweze kuziangalia barabara za vijijini kwa mfano barabara za kwetu Lindi barabara za vijijini ndizo zinazotumika kuleta mazao ya korosho, ufuta, mbao, samaki, chumvi na barabara za vijijini ndizo barabara wanazokwenda watu kwenda kuchimba dhahabu, kwa mfano Rwangwa, wanachimba *gypsum*, wanachimba *green to maline* dhahabu, wanachimba *sapphire* na barabara ya Kilwa wanachimba *gypsum*, *gas*, kwa hiyo, hizi barabara kwa kweli ni muhimu. Sikutaja barabara nyingine kwa mfano Liwale kuna uwindaji wa *Selous*, uwindaji wa kitalii, kuna utalii mzuri sana. Wanakwenda huko vijijini, lakini barabara ni mbaya, Halmashauri mzigo mzito hawawezi kumudu fedha wanazopewa. Tungeomba sana waongezewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ukurasa wa 83 imezungumzia habari za vivuko. Lindi sisi tuna vivuko, tuna Kivuko kutoka Lindi Mjini kwenda Kitunda. Watu wako huko Kitunda tungeomba sana Kivuko cha Lindi Mjini kwenda Kitunda kifikiwe vile vile ili wananchi wale wanaokaa Kitunda waweze kuja Lindi Mjini kwa mahitaji mbalimbali kama vile hospitali. Utakuta akina mama wanajifungulia njiani kwa sababu hakuna kivuko maalum. Kuna mitumbwi midogo midogo ambayo wakati mwingine huhatarisha maisha ya wananchi, wanatumbukia wanakufa mle, hakuna kivuko maalum. Tungeomba Serikali sasa waangalie upya suala la kivuko cha kutoka Lindi Mjini kwenda Kitunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza haya machache ambayo nimeweza kuzungumza, nasema ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tumesaliwa na dakika 10 kwa mujibu wa makubaliano yetu. Sasa Mntangi hizo zinaweza zikakutosha?

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo Kanuni ya 68 (7) kama ulivyosema atatoa majibu uunganishe na hili. Juu ya Mikoa au nchi kwa ujumla kwa namna ambavyo nimeona tunaendelea hapa ndani, Kusini hakuna mahali ambako kumechoka kama Kusini kwa ujumla. Hivi leo hii mtu anataka kwenda kwa ndege atatua wapi Kusini? Mimi nilipata mfadhili mwaka jana kutoka Uingereza anataka kuja kwetu Iringa, alisema hawezi kuja kwa sababu ni kilometa 700 kutoka Dar es Salaam mpaka Iringa, mpaka mtakapokuwa na viwanja vya ndege. Mkoa wa Lindi na Mtwara jamani, hebu angalieni Wabunge tukifika mahali tukaanza kuzungumzia habari ya maeneo, Mkoa wa Lindi na Mtwara ni Mikoa ambayo kwa kweli imechoka kabisa.

Ruvuma, leo ni barabara gani unazungumzia ambayo inatengenezwa zaidi ya barabara iliyokuwepo kutoka Dar es Salaam kwenda Tunduma, kutoka Makambako kwenda Ruvuma kuna barabara gani ambazo zinatengenezwa? Hivi zinawekwa, inakuwa nongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwongozo wako naomba juu hili, kwamba tumepitisha bajeti juu hapa na viwanja vya ndege vitano, mabilioni ya fedha, naomba tujenge upendo sisi wote ni wamoja hapa ndani, turudishe upendo miongoni mwetu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwanza kwa mujibu wa utaratibu tulioupitisha leo kwa ajili ya kutoa fursa kwa wenzetu waliofunga Ramadhani waweze kufanya ibada yao vizuri na baadaye kufuturu, kwa leo tutaishia saa moja kasoro robo. Kwa hiyo, muda wetu mtaona umekwisha na hivyo hakuna mchangiaji atakayeendelea ingawa kwa kesho kwa muda wa jioni tutaanza saa 10.00 lakini yako mambo mengi yamejitokeza, nadhani kuna haja jambo hili likafikiwa. Tena naamini tukirudi tutakuja na jibu zuri zaidi. Kwa hiyo, suala la muda liko hivyo.

Lakini nimeombwa mwongozo na wachangiaji kadhaa humu ndani, sasa hivi Mheshimiwa Deo Sanga, ameungana na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, hoja yao inaonekana inafanana. Kama nilivyokuwa nimesema wakati kwamba jambo hili linahitaji fursa ya kutosha kulifikiri na kwa hiyo, mwongozo wake utatolewa muda itakapoonekana, nafaa na ikibidi sasa kesho mapema. Lakini Mheshimiwa Suzan Kiwanga alikuwa ameomba Mwongozo pia juu ya vazi la Askafu linalovaliwa na Mbunge mwenzetu ambalo anapenda kuvaa skafu ya bendera ya Taifa, ingawa kwa mujibu wa kanuni ya 146 (2) (b) (i) hadi (v) halijasemwa kama ni miongoni mwa jambo linalozuiwa. Sisi Wanasheria kama kitu hakijazuiwa, maana yake kinaruhusiwa, ndio tafsiri ya Kisheria. Lakini busara hiyo ya Kisheria itawale kwa Bunge kwa sababu najaribu ku-*imagine* kama watu wote watavaa skafu hizo, hali itakuwaje? Kwa hiyo, nadhani pia na lenyewe hilo ni jambo ambalo linahitaji tafsiri nzuri ya hasa kile kifungu cha (v) kikipata tafsiri yake vizuri basi jibu lake linaweza likatolewa vizuri jibu lake. Lakini kwa kweli vazi hilo halijazuiwa wala halijaruhusiwa. Kwa hiyo, tutaliweka vizuri, lakini muda utakapoonekana unafaa au kwa sababu anayeavaa ni mmoja tutamshauri asifanye hivyo humu ndani, ni jambo jepesi tu. Jambo hili linahitaji busara tu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala lina sheria yake na sheria hiyo inaitwa Sheria ya Nembo za Taifa Sura ya 10 ya Sheria za Tanzania. Nembo za Taifa ni pamoja Bendera ya Taifa. Mheshimiwa Nchemba nilishamweleza siku nyingi kwamba kuvaa Bendera ya Taifa kama skafu ni kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria ya Nembo za Taifa. Sasa taarifa yangu ni hiyo kwamba anachokifanya, anadharau Bendera ya Taifa, anaigeuza kuwa vazi wakati Sheria ya Nembo za Taifa kifungu (6) (1) (c) kinatakaza, na ni kosa la jinai. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ni kweli iko Sheria ya Nembo za Taifa ambayo katika sheria hiyo, inaitaja pia hata Bendera ya Taifa. Lakini mtakumbuka wakati tunaanza awamu ya nne, Mheshimiwa Rais alisema, hivi kwa nini Bendera ya Marekani watu wanatembea nayo, hata wasukuma mikokoteni? Kwa nini Mtanzania asijivunie Utanzania wake kwa kuwa na nembo fulani? Mimi naona sasa hivi ziko Bendera za Taifa mahali popote watu wanafunga hata kwenye baiskeli. Kwa hiyo, tuko mbele zaidi hata hatua ya sheria hiyo Mheshimiwa Mbunge, unayoisema na hata kulitokea mjadala humu ndani Bungeni kwamba kwa nini Bunge letu lina kapeti ambalo lina rangi za Bendera ya Taifa na tunakanyaga, kwa hiyo, tuko zaidi ya pale Mheshimiwa Mbunge na pengine mwenzetu Nchemba anaweza akawa ni mzalendo namba moja. Kwa hiyo, tuliangalie vizuri jambo hili kwa sababu pamoja na hapo, lakini tuko mbele zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine napenda nichukue nafasi hii kuahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.37 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 2 Agosti, 2011 saa Tatu Asubuhi)